

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 16 Julai, 2004

(Mkutano Ulianze Saa Satu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza ningependa kutambulisha wageni wa Kimataifa katika *Gallery* ya Bunge leo tuna Waheshimiwa Wabunge wanne wa Bunge la Malawi pamoja na Katibu wa Bunge hilo. Tunawakaribisha. *(Makofi)*

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. JINA KHATIB HAJI (k.n.y. MHE. SOPHIA M. SIMBA)
MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:-**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 256

Uzibaji wa Barabara za Pembezoni

MHE. AZIZA SLEYUM ALI (k.n.y. MHE. SOPHIA M. SIMBA) aliuliza:-

Kwa kuwa kumezuka tabia ya kuziba barabara za pembezoni (*Service Roads*) kwa kuweka vizingi vya chuma katika Jiji la Dar es Salaam:-

- (a) Je, wanaofanya hivyo si wanavunja sheria kwa makusudi?
- (b) Je, kwa nini Serikali inafumbia macho ukiukwaji huo wa sheria?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara za pembezoni zilizozibwa na vizingi vya chuma ni za watembea kwa miguu na baiskeli (*walks ways*).

SPIKA: Redio Tanzania inatangaza moja kwa moja yanayotokea humu ndani. Kwa hiyo, kukiwa na mazungumzo ya chini kwa chini nayo yanaingia kwenye redio vile vile. Tafadhalii tumsikilize Mheshimiwa Waziri akijibu swalii. Ungeanza upya Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara za pembezoni zilizozibwa na vizingi vya chuma ni za watembea kwa miguu na baiskeli (*walks ways*). Hali hiyo iko kwenye barabara za Morogoro, Ali Hassan Mwinyi na Kawawa katika Jiji la Dare es Salaam. Vizingi vimewekwa kwenye njia za waenda kwa miguu ili kuzuia magari yasipite kwenye njia hizo ambazo magari hayaruhusiwi kupita. Hii ni kwa ajili ya usalama wa raia wa endao kwa miguu na wala siyo uvunjaji wa sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa njia zilizowekwa vizingi vya chuma ni za waendao kwa miguu na baiskeli, nafasi ya kutosha imeachwa kati ya kigingi na kigingi ili watu wapite. Hivyo siyo kwamba Serikali inafumbia macho bali ni jambo linalosaidia kudhibiti usalama wa waendao kwa miguu. Pia kwa kuweka vizingi njia hizo zinalindwa dhidi ya uzito wa magari yenye kusababisha uharibifu wa njia hizo.

MHE. PETER KABISA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Naomba niulize swalii moja dogo la nyongeza. Kwa vile kuna maeneo mengi katika Jiji la Dar es Salaam ambayo kuna utaratibu au kuna uzoefu wa watu kufunga barabara kwa kuweka vizingi kama hivyo ambavyo vinasababishwa usumbufu wakati wa kuteremsha au kupakia mizigo hasa kwa maeneo ya katikati ya Jiji la Dar es Salaam na sehemu za Ofisi za Balozi za Jijini Dar es Salaam. Serikali inasemaje kwa hilo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya maeneo katikati ya Jiji la Dar es Salaam yamewekewa vizingi katika maeneo ya barabara. Hili limekwishatolewa maelekezo kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake kuhakikisha kwamba wale wote waliokiuka sheria, vizingi hivyo viondolewe. (*Makofî*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa maeneo hayo ya pembezoni yameachwa kwa ajili ya watu wanaotembea kwa miguu na katika baadhi ya sehemu za barabara kuu kwa ajili ya watu wanaoendesha balskeli, Mheshimiwa Waziri ana maagizo gani kwa watu ambao wamekuwa na tabia ya kwenda watu kama sita bega kwa bega na kuzuia watu wengine inabidi waingie kwenye barabara? Je, kukomesha tabia hiyo Mheshimiwa Waziri ana maagizo gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nadhani hili ni suala la ustaarabu na la kuelimishana na jamii tu kwamba siyo vizuri watu kutanda katika barabara na kuzuia wengine wanaotumia barabara hiyo, kwa hiyo, tutaendelea kuelimishana.

Na. 257

Kituo cha Afya Nkomolo

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA (k.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI) aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya Nkomolo kilichopo Mjini Namanyere kimekuwa kinasaidia sana wananchi ambao wengi wao hawana uwemo wa kifedha; na kwa kuwa Kituo hicho kimeanza kutoa huduma ya kulaza wagonjwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa majengo ambayo hayajakamilika na pia kukipanua Kituo chenyewe kwa ujumla?

(b) Je, isingekuwa vizuri kwa Serikali kukiongezea madawa Kituo hicho muhimu sana kwa wananchi wasiojiweza?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Kituo cha Afya Nkomolo kinasaidia wananchi na hivi sasa kimeanza kulaza wagonjwa baada ya Serikali kuendelea na mpango wake wa kumaliza ujenzi wa Kituo hicho. Majengo ambayo tayari yamekamilika ni:-

- Sehemu ya wagonjwa wa nje (*OPD*);
- Sehemu ya kliniki ya mama na mtoto;
- Jiko na jengo la kufulia nguo;
- Nyumba tatu za waganga na wauguzi; na
- Wodi ya wanawake, wanaume na watoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kujenga majengo ambayo bado hayajakamilika kwa kutenga fedha kila mwaka katika kifungu cha maendeleo. Majengo hayo ni pamoja na kitengo cha Meno (*Dental Unit*), jengo la *X-ray* na jengo la upasuaji. Kwa kipindi cha miaka mitatu 2003/2004 hadi 2005/2006 Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi imepanga kutumia kiasi cha shilingi 30,000,000/= kukamilisha ujenzi ikiwa ni jitihada za Serikali kukipanua Kituo hiki.

(b) Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa upanuzi wa Kituo hiki utakapokamilika, mahitaji ya dawa na vifaa mbalimbali yataongezeka ili kutosheleza mahitaji ya wananchi wengi watakaopata huduma katika Kituo hicho. Aidha, kuititia mpango wa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Serikali itaendelea kukipata Kituo hicho dawa zinazohitajika kama ilivyo katika vituo vingine vya Afya.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ukarabati na ujenzi wa vituo vya Afya vingi nchini unakwenda pole pole mno kiasi ambacho wananchi wanapojoitolea wanaona Serikali inachelewa sana kuwapatia msaada wanaohitaji kama ilivyo katika Kituo hiki cha Nkomolo?

(b) Mheshimiwa Waziri vipo vituo vingine vya Afya kama kile cha Matai, Olumi na Mtohisa ambavyo vinahitaji ukarabati, lakini kila wakati tunapoomba fedha kwa ajili ya ukarabati wa vituo hivyo tunaelezwa tusubiri. Je, ni lini Serikali itajitahidi kuweza kukarabati vituo hivi ili navyo viweze kuwahudumia wananchi katika Mkoa wetu wa Rukwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli ukarabati wa Vituo vya Afya unakwenda taratibu, lakini hili linatokana na uwezo wetu wa kifedha hatuwezi kutumia fedha ambazo hatunazo.

Kwa hiyo, kwa kutumia juhudi za wananchi na vile vile kutumia wahisani waliopo namwomba Mheshimiwa Mbunge azidi kushirikiana na wananchi katika

kuwahamasisha wale wote ambao wana nia njema ya kuwasaidia wananchi ili tuweze kuharakisha ukarabati wa vituo vyote vya Afya.

Na. 258

Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya Sera za Serikali katika kuwapatia wananchi wake maendeleo ni ubinafsishaji wa baadhi ya Mashirika yake hasa yale ambayo hayafanyi vizuri katika kuleta tija; na kwa kuwa Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) ambalo ni mkombozi wa wanyonge, tayari lipo katika orodha ya Mashirika ambayo ni *specified*:-

(a) Je, kwa nini Serikali haifanyi juhudini za makusudi za kuliboresha Shirika hilo kabla ya kulikodisha au kulibinafsisha?

(b) Je, Serikali haioni kwamba inakwenda mwendo wa kasi katika kubinafsisha baadhi ya Mashirika?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inafanya juhudini za makusudi kuboresha Shirika la Reli kabla ya kulibinafsisha kwa njia ya kukodisha. Tayari imeshafanya mazungumzo na Benki ya Dunia kupata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 33 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu ya reli. Benki ya Dunia imekubali kutoa asilimia 25 sawa na Dola za Kimarekani milioni 8.25 kuanzia Julai, 2004 na pesa hizi zitatumika kugharimia ukarabati wa njia korofii za reli yenye urefu wa kilometra 25 kati ya Itigi na Tabora kabla ya kukodisha Shirika. Pia Serikali imetoe shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kuendesha shughuli za reli.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Shirika la Reli liki katika hali mbaya hasa vitendea kazi kama vile vichwa vya treni na mabehewa ya mizigo yapatayo 300. Aidha, mahitaji ya Shirika katika kipindi kifupi ni kiasi cha shilingi bilioni 70 sawa na Dola za Kimarekani milioni 63 ambacho ni kikubwa sana. Serikali haitaweza kumudu gharama hizi kwa kuzingatia kuwa ina majukumu mengine muhimu ya elimu, barabara, afya na huduma nyininge. Kwa hiyo, litakuwa jukumu la mwekezaji kutafuta fedha hizo. Ni ubinafsishaji pekee utawezesha upatikanaji wa nyenzo muhimu kama vile vichwa vya treni na mabehewa ambayo gharama ya kuvinunua inakadirwa kuwa dola za Kimarekani milioni 150.

(b)Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba zoezi la ubinafsishaji linafanyika kwa haraka. Serikali imechukua hatua madhubuti kuhanikisha kuwa zoezi la ubinafsishaji linafanyika kwa uangalifu mkubwa, ndiyo maana mwaka 2003 Serikali ilahirisha zoezi la ubinafsishaji wa *TRC* baada ya kuona kuwa hapakuwa na ushindani wa kutosha baada ya mzabuni kubakia mmoja. Hali hii ingeweza kusababisha kupata mikataba isiyo imara na makini.

Aidha, zoezi la ubinafsishaji linaendeshwa kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa. Hivi sasa zoezi la ubinafsishaji wa shirika limeshakamilishwa mchuko wa awali na kuwapata wawekezaji walioonyesha nia ya kushiriki katika kukodi shirika. Tayari kampuni sita zilizojitokeza zimeandikiwa barua kuleta zabuni kwa ajili ya kukodi Shirika. Mwisho wa kuleta zabuni ni mwezi Agosti, 2004.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina swalii dogo fupi tu la nyongeza. Kwa kuwa ni wazi kwamba baada ya kukamilika kwa barabara ya lami kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, ni kwamba Shirika hili litakabiliwa na ushindani wa kibiashara. Sasa swalii kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba Shirika la Reli katika uboreshaji wake limeliangalia suala hilo ikiwa ni pamoja na kuboresha reli hiyo iweze kuwa na treni za *speed* ya hali ya juu ili kuweza kumudu ushindani? (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara ya lami kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza itakapokamilika Shirika la Reli litawenza kupata ushindani wa kibiashara. Lakini vile vile kutokana na nia ya Serikali ya kuboresha Shirika hili la Reli kuitia ubinafsishaji tuna uhakika kwamba litafanya kazi kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile barabara ya lami kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza peke yake haitatosha, kwa sababu dira yetu tunavyoendelea huko mbele ni kuendelea kukuza *economy base* ya nchi yetu kwa hiyo, kutakuwa na bidhaa nydingi ambazo zitakuwa zinatoka Mwanza kwenda Dar es Salaam na Dar es Salaam kwenda Mwanza.

Vilevile ikizingatiwa kwamba Bandari ya Dar es Salaam inashughulikia mizigo ya nchi jirani ambazo tunashirikiana nazo kiuchumi.

Na. 259

Historia ya Viongozi Wakuu wa Taifa

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Kwa kuwa ni jambo zuri na muhimu sana kwa wananchi hasa wa vizazi vijavyo kujua historia ya nchi yao na ya viongozi Wakuu wa Kitaifa waliowahi kuongoza nchi yetu na wanaoendelea kuliongoza Taifa hili wakiwemo, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Hayati Edward Moringe Sokoine na Hayati Dr. Omar Ali Juma na kadhalika:-

(a) Kati ya viongozi hao niliowataja, je ni yupi ambaye hajaandikiwa kitabu cha kumbukumbu ya historia yake na mambo aliyoyafanya wakati wa uongozi wake?

(b) Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuandika historia ya viongozi wetu ili vizazi vijavyo viweze kuwatambua pamoja na michango yao kwa Taifa hili?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, kuwa ni muhimu sana kwa wananchi na vizazi vijavyo kujuu historia ya nchi yao na viongozi wakuu wa Kitaifa waliowahi kuongoza nchi yetu na wanaoendelea kuliongoza Taifa hili. Kutunza kumbukumbu za nchi na hususan za viongozi wa kitaifa, ni jambo la msingi na la kawaida katika nchi nyingi duniani kwani kumbukumbu za nchi na viongozi zinatoa mwelekeo wa historia kwa nchi kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mazingira mazuri ya utunzaji kumbukumbu zake kwa kuanzisha Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Mambo ya Kale na Makumbusho ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ya jumla, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo:-

(a) Kati ya viongozi waliowataja ni Hayati Dr. Omar Ali Juma pekee ambaye bado hajaandikiwa kitabu cha kumbukumbu ya historia yake na mambo aliyoyafanya wakati wa uongozi wake. Historia ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere imeandikwa na watu mbalimbali ikiwemo *biography* yake iliyoandikwa na Bwana William Smith. Historia ya Sheikh Abeid Amani Karume imeandikwa na bwana R. K. Manjisi na lililokuwa Shirika la Habari Tanzania liliandika historia ya Hayati Edward Moringe Sokoine. Aidha, historia ya Sheikh Thabit Kombo imeandikwa na Bi. Minael-Hosanna O. Mdundo. Vitabu hivi vinapatikana katika maduka ya vitabu.

Hivyo, napenda kuwapongeza Waandishi hao kwa kuchukua dhima hiyo ya kuweka kumbukumbu za viongozi wetu hao Wakuu katika maandishi. Aidha, napenda kutoa wito kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge kutumia hazina iliyopo ya nyaraka na kumbukumbu za viongozi wetu kuandika vitabu juu ya historia ya nchi yetu pamoja na viongozi wa nchi kwa manufaa ya vizazi vijavyo. (*Makofit*)

(b) Katika juhudini za kuhakikisha kuwa historia ya viongozi wetu na kudumisha michango yao inarithishwa kwa vizazi vijavyo, Serikali inaandaa utaratibu wa kisheria utakaojenga mazingira ya kuwa na utaratibu wa kudumu wa kuthamini na kutunza kumbukumbu za viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa na kuweka udhibiti wa kisheria ili kuhakikisha kuwa hazina waliyonayo viongozi wetu hawa haipotei na kwamba inakuwepo kwa ajili ya vizazi vijavyo. Tayari tumepata uzoefu wa nchi mbalimbali katika suala zima la kuenzi viongozi wetu.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia majibu mazuri.

(a) Kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekiri katika jibu lake kwamba ni Marehemu Dr. Omar Ali Juma, pekee ambaye alikuwa Makamu wa Rais wa nchi hii ndiye ambaye hajaandikiwa historia yake. Je, ni sababu zipi zilizopelekea mpaka sasa hivi nauliza swali hili hajaandikiwa historia yake na yeze alikuwa ni kiongozi muhimu katika nchi yetu?

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha kitengo maalum cha wataalam waandishi wa kuandika historia za viongozi mbali na wale watu binafsi wanaoandika historia za viongozi? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, hapo awali hapakuwa na utaratibu wala Taasisi ndani ya Serikali ambayo ilikuwa inashughulikia suala la uandishi wa historia za viongozi wetu. Hili limekuwa likifanywa na wanahistoria binafsi ikiwemo *University of Dar es Salaam*. Lakini kama nilivyojibu katika jibu la msingi, Serikali inaandaa Muswada ambao pengine utaruhusu katika kanuni zake kuwa na kitengo ambacho kitaandika historia hizo.

Vile vile natoa wito kwa waandishi zikiwemo *University* mbalimbali kujitokeza kuandika historia za viongozi wetu kwa kutumia kumbukumbu zao ambazo ziko kwenye Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kama nilivyojesta awali Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ya Kuenzi Waasisi wa Taifa na katika utaratibu na kanuni tutajaribu kuona kwamba hayo aliyoyaomba au aliyoyataka Mheshimiwa Mbunge yanazingatiwa.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala mama alilouliza Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, alikuwa anahitaji kujua historia ya Wakuu wa Kitaifa waliowahi kuongoza nchi yetu na wanaoendelea kuliongoza Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa uelewa wangu ni kwamba viongozi hao ni vilevile Waheshimiwa Mawaziri Wakuu waliopita akiwemo Mheshimiwa Dr. John Malecela na

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Aboud Jumbe, kwa sababu haikuelezwu kwamba ni wale waliofariki, waliowahi kuongoza, sasa je, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini kuhusu viongozi hao wa nchi? (*Makofsi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, pengine ni bahati mbaya tu nilitaja majina ya marehemu viongozi wetu. Lakini jibu langu linajumuisha viongozi wote ambao wamekuwahi kuwepo Tanzania. Mimi ningependa kutoa wito na kwa vile Mheshimiwa John Malecela yuko humu ndani kwamba watatusaidia na wao wakianza kuandika *memory* zao lakini si lazima. Ahsante sana. (*Makofsi*)

Na. 260

Majengo ya Gereza Kuu - Isanga

MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Dodoma unakua kwa kasi kubwa sana; na kwa kuwa Gereza Kuu la Isanga lipo karibu sana na Mji huo na hali ya majengo yake ni mbaya sana na yameshapitwa na wakati:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Gereza jipya nje kidogo ya Mji wa Dodoma na kuhamishia shughuli zote za Gereza lililopo kwenye Gereza hilo jipya?

(b) Kama mpango wa kulihamisha Gereza hilo upo, je, Serikali ina mpango wa kujenga nini kwenye eneo hilo baada ya Gereza kuhamishwa?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Chuo Kikuu kwenye eneo hilo kama ilivyoainishwa katika *Master Plan* ya Mji wa Dodoma?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Gereza la Isanga ni mojawapo ya Magereza kumi yenye ulinzi mkali nchini (*Maximum Security Central Prisons*). Gereza hili lilijengwa kwa kuzingatia *Master Plan* ya Mji wa Dodoma ya wakati huo na lilianza kutumika mwaka 1951. Tangu mwaka 2001/2002 hadi 2003/2004 Serikali imekuwa inatekeleza mpango wa kukarabati magereza yote yenye ulinzi mkali kwa lengo la kuyaboresha na kuyaimarisha. Chini ya mpango huo, Gereza la Isanga limekarabatiwa kwa kiwango kikubwa na sasa majengo yake ni imara na yana sura ya Gereza jipya. Kwa sababu hiyo Serikali kwa sasa haina mpango wowote wa kujenga Gereza jipya nje kidogo ya Mji wa Dodoma na hivyo haitarajii kuhamisha shughuli za Gereza la Isanga.

Kuhusu mpango wa kujenga Chuo Kikuu katika Mji wa Dodoma inawezekana Wizara husika pamoja na *CDA* wanao mpango huo na eneo bila shaka litapatikana kwani Mji wa Dodoma bado una maeneo mengi ya wazi.

MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake.

(a) Pamoja na kuwa jengo hilo limefanyiwa ukarabatiwa, lakini hali yake bado ni mbaya sana; na kwa kuwa uchakavu wa jengo la Gereza la Isanga unasababisha wafungwa waishi katika hali ya unyama kitu ambacho kinatuondolea sisi sifa ya ubinadamu na utu ambao tunajivunia. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni ya kuwa kuendelea na hali hiyo Serikali inakiuka mikataba ya Kimataifa inayohusiana na Haki za Binadamu ambayo sisi tuliiridhia?

(b) Kwa kuwa uamuzi wa kuhamishia Serikali Dodoma na kuifanya Dodoma kuwa ni Makao Makuu ni azma ya Chama cha Mapinduzi ambayo iliridhiwa na wananchi wote wa Tanzania na ndiyo maana tumekuwa na *Master Plan*.

SPIKA: Sasa uliza swalii.

MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF: Swalii, kutohamisha Gereza la Isanga kutoka hapo lilipo na kuachia eneo hilo kuwa wazi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba Wizara yake inakuwa kikwazo katika kutimiza azma hiyo ambayo imo katika Ilani ya Uchaguzi ambayo sisi sote pamoja na yeche tuliiitetea wakati wa Uchaguzi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kwamba hali ya Gereza la Isanga ni mbaya sana si kweli, bila shaka hajalitembelea hivi karibuni ili kuona ukarabati mkubwa sana ambao umefanyika, tumetumia karibu zinakaribia shilingi milioni 200 kuliboresha lile Gereza. Sasa hivi ni gereza bora. Maisha ya wafungwa vile vile tumeyaboresha mle ndani aende atakuta wafungwa sasa hivi wanakula chakula kizuri, wanapata *diet* nzuri na kamili, ugali, wali, nyama, maharage na matunda. Mpaka tunaanza kuogopa kwamba baadhi ya watu wanaweza sasa wakafanya makosa ili waende wakale chakula kizuri kuliko wanachokula nyumbani kwao. (*Makofit/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwa taarifa tu ya Mheshimiwa Mbunge baada ya siku chache zijazo tunaleta magodoro katika Gereza la Isanga badala ya kulala kwenye virago watalala kwenye magodoro. Katika miezi michache ijayo wataanza kuvali, *Kaunda suit*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kusema kwamba tunavunja Haki za Binadamu baada ya kufanya yote haya kusema kweli siyo sahihi. Tunastahili kwa kweli Jeshi la Magereza kuwapa pongezi badala ya kulaumiwa. (*Makofit/Kicheko*)

Kuhusu kwamba gereza lisipohama linakwamisha utaratibu mzima wa kuhamisha Makao Makuu Dodoma. Kwa kweli si sahihi, haiwezekani lile Gereza liwe ndicho

kikwazo cha kuzuia mipango ya kuhamia Dodoma, si kweli. Lile Gereza tunaamini kwamba halidhuru chochote na eneo Dodoma bado ni eneo kubwa sana kusema kweli, yeoyote atakayetaka kuwekeza, anayetaka kujenga, eneo bado ni kubwa kabisa.

Na. 261

Ajira ya Vijana Ndani ya Jeshi la Polisi

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA aliuliza:-

Kwa kuwa ajira ya vijana ndani ya Jeshi la Polisi kama ilivyo katika mambo mengine nyeti lazima ishirikishe vijana wa pande zote mbili za Muungano:-

- (a) Je, ni vijana wangapi kutoka Tanzania Zanzibar wameajiriwa ndani ya Jeshi la Polisi kuanzia mwaka 1999 hadi 2003?
- (b) Je, kati ya hao walioajiriwa, ni vijana wangapi walitoka katika Mkoa wa Kaskazini Pemba?
- (c) Je, ni taratibu zipi zinazotumika katika uajiri huo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo na Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ajira za askari wa Jeshi la Polisi kama ilivyo kwa Wizara zingine za Muungano zinapaswa kushirikisha vijana wa pande zote mbili za Muungano yaani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Hivyo ndivyo inavyofanyika katika ajira za askari katika Jeshi la Polisi. Utaratibu unaozingatiwa katika kuajiri askari Polisi ni ule ulioelezwa katika kanuni za Jeshi la Polisi (*PGO*) Na. 54. Kwa mujibu wa kanuni hizo kabla ya kuajiri, Jeshi la Polisi hutangaza nafasi za ajira na wale wanaotaka kutoka Tanzania Bara na Zanzibar hutuma maombi. Baada ya kufanya uchambuzi wa waombaji, wale wenye sifa huitwa kwenye usaili na wanaofaulu usaili huchaguliwa na kujiunga na mafunzo ya msingi ya uaskari. Baada ya kumaliza mafunzo, wahusika huajiriwa katika Jeshi la Polisi na mwisho wake hupangiwa vituo vya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1999 hadi 2003 vijana 776 kutoka Tanzania Zanzibar wameajiriwa katika Jeshi la Polisi. Aidha, kati ya vijana hao, 156 ni toka Pemba, ambapo vijana 90 walijiriwa toka Kaskazini Pemba. (*Makofii*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, inaonekana nia ya Wizara katika jambo hili ni nzuri, lakini kwa kuwa katika hali halisi ya uajiri wa vijana hawa watendaji walioko chini hutoa masharti yenye kusumbua kidogo, je, hawaoni kwa sasa ni wakati muafaka kwa Wizara kuangalia kwa karibu suala la uajiri ili taratibu nzuri zilizowekwa zisivunjwe na watu kwa makusudi?

La pili, je, kama mtu atagundua kuwa taratibu zimevunjwa kwa makusudi, ni utaratibu gani atumie ili kulalamikia hali hiyo na waliohusika waweze kuchukuliwa hatua? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, masharti ya kuajiri vijana yaliyopo hayana usumbufu wowote kwa sababu matangazo yanatangazwa, wanaomba na katika kuwachuja wale wenye sifa hafanyi mtu mmoja inafanywa na Kamati.

Kwa upande wa huko Bara, kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama kuanzia kwenye miji anakoishi wanamjadili, wanakwenda kwenye Kata Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Kamati ya Ulinzi wa Usalama ya Mkoa. Kwa hiyo, ni Kamati hizo zinazochuja.

Kwa upande wa Tanzania Zanzibar ni kweli awali alikuwa anachuja Sheha. Lakini Kamati ya Pamoja ya Muafaka imeleta ombi na tumeshalikubali kuanzisha utaratibu. Sasa Sheha hatakaa peke yake, atakaa na wale wasaidizi wake. Ni utaratibu ambao umetuletea Kamati ya Muafaka, tumeshaukubali kwa hiyo, hatafanya mtu mmoja, atafanya na wale wasaidizi wa Sheha.

Sasa sehemu ya pili, anasema kama mtu akikiuka taratibu, sasa kama mtu atakiuka taratibu, utaratibu huo tuletewe kwa sababu utaratibu huu umeainishwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, mtu akikiuka ni kwamba amekiuka sheria, tuletewe na tutachukua hatua.

Na. 262

Madini Katika Milima ya Usambara Lushoto

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa inaaminika kwamba katika Milima ya Usambara kuna Madini mbalimbali na ushahidi upo kwa tukio la mwezi Februari, 2004 ambapo wananchi kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi waliingia katika Msitu wa Hifadhi ya Balangai, Jimboni Bumbuli na kuanza kuchimba Dhahabu:-

- (a) Je, katika Milima hiyo kuna madini ya aina zipi hasa?
- (b) Je, Serikali inatoa maelekezo gani kuhusiana na madini hayo?

(c) Kwa kuwa maeneo hayo yenye madini yapo kwenye hifadhi za misitu ya Taifa, je, ni mbinu gani zinazotumika ili maliasili ya madini yaliyopo yatumike kupunguza umaskini bila kuathiri mazingira?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kulingana na kumbukumbu zilizopo, kumbukumbu za utafiti wa kijioljia, Milima ya Usambara ina madini ya Dhahabu, madini ya vito ya aina ya *Garnets, Ruby, Sapphire, Zircon Green Tourmaline*. Aidha, milima hiyo pia ina shaba, chuma, *kynite, graphite* na ulanga.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sera na sheria ya madini, kampuni na watu binafsi wanaruhusiwa kuomba leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini katika milima hiyo. Hata hivyo, kwa uchimbaji wa madini ya vito, iwapo mwekezaji anatoka nje ya nchi, hapana budi aingie ubia na Watanzania kwa angalau 25% kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1998. Aidha, kwa baadhi ya maeneo ya uchimbaji, Waziri wa Nishati na Madini ana mamlaka ya kisheria kutenga maeneo kuwa maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo baada ya kushauriwa na Kamati ya Ushauri ya Madini iliyoundwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, utengaji huo ukishafanyika, eneo hutangazwa katika gazeti la Serikali na ugawaji wa viwanja kwa watakaojitokeza kuomba hushughulikiwa na Kamati ya ugawaji chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya. Wajumbe wengine wa Kamati hiyo ni pamoja na Mbunge wa eneo husika, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Afisa wa Madini na Wajumbe wengine watatu wa kuteuliwa.

(c) Mheshimiwa Spika, iwapo madini husika yamo ndani ya hifadhi ya msitu, kwa mujibu wa kifungu cha 95(1) (c) cha Sheria ya Madini, mwenye leseni ya madini hatakiwi kuanza kazi yoyote ya madini bila kwanza kupata kibali cha maandishi kutoka mamlaka husika na hifadhi hiyo itampasa kutekeleza masharti atakayopewa na Mamlaka inayosimamia eneo hilo ili shughuli zake zisiathiri mazingira. Endapo mashapo ya kutosha yatapatikana kwa uchimbaji mkubwa mwenye leseni pia atawajibika kuandaa na kuwasilisha Serikalini uchambuzi wa kina wa mazingira (*Environmental Impact Assessment*) na kuandaa mpango wa usimamizi wa mazingira (*Environmental Management Plan*) ili kuhakikisha kwamba shughuli zake haziathiri mazingira.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda niseme maeneo mengine ya milima ina vyanzo vya maji na ni marufuku kuchimba au kuvamia maeneo hayo yenye vyanzo vya maji kutokana na sababu muhimu zinazoleweka kwamba wataleta uharibifu mkubwa wa upatikanaji wa maji.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninalo swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa imedhihirika wazi kwamba milima hiyo ina madini mengi, je, Waziri atakubaliana nami kwamba kuna haja ya kupeleka *surveyer* wa madini (*Mineral Survey*) ili aonyeshe maeneo ambayo hayapo katika misitu ya hifadhi lakini yapo kwenye mashamba ya watu ili wananchi wasihangaike kufukua fukua na kutumia mali hiyo vizuri zaidi na kutunza mazingira?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kabisa Mheshimiwa William Shellukindo na kwamba tutafanya kama alivyoshauri haraka iwezekanavyo.

Na. 263

Vifaa Vya Kufundishia na Ukarabati wa Shule

MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA aliuliza:-

Kwa kuwa majengo ya Shule za Msingi za Nasuruli, Chamakapu na Buwela yapo katika hali mbaya ya uchakavu:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyakarabati majengo ya shule hizo?
- (b) Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa vya kufundishia katika shule zilizopo kwenye Jimbo la Mwibara?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ukarabati wa majengo ya Shule za Msingi ni jukumu la Halmashauri za Wilaya, Manispaa au Miji inayohusika kwa kushirikiana na Kamati za Shule na Serikali za Vijiji vinavyohusika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kwa wadhifa wake kama Diwani anaweza kuuliza swali hilo na kujibiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kuhusu Shule za Msingi alizozitaja za Nasuruli, Chamakapu na Buwela.

Hata hivyo, ndani ya Bunge hili napenda kumtaarifu kuwa katika mwaka 2003/2004 Serikali ilipanga kujenga madarasa 14,203 na kukarabati baadhi ya majengo ya Shule za Msingi katika Wilaya zote 113 ikiwemo Wilaya ya Bunda ambayo ilipangiwa kujenga madarasa 129 na kukarabati madarasa 31. Hata hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kwa kushirikiana na wananchi, imefanikiwa kuvuka malengo na kujenga madarasa 258 na imekarabati madarasa 16 badala ya 31. Nawapongeza sana kwa kazi hiyo nzuri. (*Makofii*)

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia, Serikali hadi Desemba, 2003 ilitoa ruzuku ya uendeshaji ya jumla ya shilingi 164,307,100/= zikiwemo fedha za ununuzi wa vitabu, vikasha vya sayansi na vifaa vingine vya elimu. Suala la mgawanyo wa fedha na vifaa hivyo kwa shule mbalimbali ni la Halmashauri. Serikali itaendelea kutuma ruzuku na uendeshaji wa shule kwa kila Wilaya kulingana na idadi ya wanafunzi katika kila Wilaya na Halmashauri itazigawa kwa kila shule kufuata wingi wa wanafunzi. Hakuna mgawanyo kwa Majimbo ya Uchaguzi kwa sababu huo ni muundo au utaratibu wa kuwapata Wabunge wanaowakilisha Wilaya au Halmashauri moja.

MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa tunaboresha Elimu za Msingi, je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuna haja ya kupandisha mishahara ya Walimu ikiwa ni pamoja ya marupurupu yao ili waweze kufundisha vizuri?

Pili, kwa kuwa tumepeleka vifaa vya kufundishia ikiwa ni pamoja na *science kit* katika shule za msingi, je, Waziri haoni kuna haja ya kuweka fungu maalum kwa ajili ya kuwafundisha walimu hawa ili walijue vizuri somo la sayansi kwa ajili ya kuboresha elimu ya sayansi na teknolojia?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha mishahara ya walimu na mafao ya walimu kwa ujumla ni suala tunaloendelea nalo kila mwaka. Katika miaka hii miwili iliyopita tumechukua hatua nzuri ya kupandisha mishahara ya walimu na katika Bajeti hii Mheshimiwa Mbunge atakuwa ameona namna tunavyoweka mkazo hasa katika ujenzi wa nyumba za walimu ambayo nayo ni sehemu ya mafao ya walimu.

Pili, kwamba tunapeleka vifaa, tutenge fungu kwa ajili ya mafunzo ya walimu. Napenda kumkumbusha tu kwamba katika hotuba yangu ya Bajeti nimeeleza jambo hili na fedha zimetengwa kwa ajili ya *Inservice Training* tena kwa kiwango kikubwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, nilisema mwaka huu masuala ya mafunzo kazini yatawahuwa walimu wa shule za msingi 74,000 kwa lengo la kuwapa mafunzo yanayoongeza ujuzi wa masomo wanayofundisha na ni kwamba wale watakaofaulu watapandishwa kutoka madaraja ya B na C kwenda daraja la A kutokana na ujuzi wa masomo wanayofundisha. Kwa hiyo, hatua hizo tunazichukua. (*Makofifi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA : Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge angekuwepo wakati wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Utumishi tulionyesha kabisa kwamba katika Bajeti ya mishahara, kuna ongezeko la asilimia 54 ya Bajeti ya mishahara imeperekwa kwa walimu ambapo wao ni asilimia 49, hii inaonyesha ni umuhimu kiasi gani Serikali na kwa maagizo ya Chama cha Mapinduzi inavyowapa umuhimu walimu. (*Makofifi*)

Kituo cha Shule ya Awali

MHE. MARIA D. WATONDOHA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshaamua kuwa na Kituo cha Shule ya Awali katika kila Shule ya Msingi; na kwa kuwa Elimu ya Awali hutoa msingi mzuri kwa wanafunzi:-

(a) Je, Serikali imeandaa vyuo gani kwa ajili ya kuandaa Walimu wa Shule za Awali?

(b) Je, ajira ya walimu hao wa Shule za Awali itaanza lini ili kila shule nchini ipate Walimu wenyewe sifa?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ualimu wa Elimu ya Awali yanatolewa katika Vyuo vya Ualimu saba ambavyo ni Butimba, Tabora, Kabanga, Mpwapwa, Singachini, Songea na Kitangali. Wastani wa wahitimu kutoka vyuo hivyo ni walimu 210 kwa mwaka. Kwa utaratibu wa sasa wa kila Shule ya Msingi kuwa na madarasa ya Shule ya Awali hii haitoshelezi mahitaji ya Walimu hao. Wizara yangu imeangalia upya utaratibu wa kutoa mafunzo hayo, kwa kurekebisha na kuiboresha mihtasari ya Elimu ya Ualimu itakayotumika kwa vyuo vyote vya ualimu ikiwa ni pamoja na kuingiza mafunzo ya ualimu wa Elimu ya Awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu sehemu (a) na (b) ya swali kama ifuatavyo:-

(a) Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Awali sasa yanaingizwa katika mfumo mzima wa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya cheti. Kundi la kwanza la walimu wanafunzi au walimu wa tarajali watakaonufaika na utaratibu huu litaanza Januari, 2005.

Wanachuo wote watakaosomea ualimu ngazi ya cheti pamoja na masomo mengine watasoma pia masomo ya malezi ya Elimu ya Awali na mbinu za Kufundisha Elimu ya Awali. Vyuo vyote vinavyotoa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya cheti vitatoa mafunzo haya.

(b) Mheshimiwa Spika, mafunzo haya yameongezwa ili kuhakikisha kila anayeingia chuoni anapata mafunzo ya Elimu ya Awali. Kwa kuzingatia malengo ya MMEM, mafunzo haya yataanza na wanachuo 10,000 mwaka 2005 na yatafuatia na 9,000 mwaka 2006 na kuendelea kulingana na mahitaji ya walimu wa ngazi ya cheti.

Kwa hiyo, ajira yao itakwenda sambamba na ajira ya wahitimu wa mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti. Aidha, walimu wengine waliopo watapewa mafunzo hayo kwa njia ya mafunzo kazini. (*Makofî*)

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo na nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa shule za msingi ziko karibu kila Kijiji hapa nchini na kwa kuwa walimu hawatoshi na kwa kuwa Serikali ina lengo la kuboresha elimu na katika kuboresha elimu, Elimu ya Awali ni muhimu sana, je, kwa kuunganisha mafunzo ya cheti cha Ualimu daraja la A, Elimu ya Awali haoni kwamba maeneo mengine yatakosa kabisa walimu wa kutosha kwa sababu walimu hawatoshi?

Pili, kwa kuwa Elimu ya Awali tumeizungumzia siku nyingi na vipo vyuo binafsi katika majibu yake aliyonipa wakati wa Bajeti alisema vipo vyuo binafsi vinavyotoa mafunzo haya. Hawa wanaofunzwa katika vyuo binafsi wataingizwa vipi katika *scheme* ya Serikali?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, hili la kwanza kwamba tuna shule nyingi za msingi kwa hiyo, walimu hawatatosha. Hatua tuliyochukua ni kubwa sana kwamba kila tunapofundisha walimu wa cheti watapewa pia ujuzi wa kuweza kufundisha Elimu ya Awali. Kwa hiyo, kadri tunavyoongeza walimu kwa ajili ya shule hizo anazozisema nyingi ndivyo tutakavyozidi kuwapata walimu wa kufundisha Elimu hii ya Awali.

La pili, kuhusu namna ya kuwakubali na kuwaingiza katika utaratibu wa Serikali, walimu wanaosomea katika vyuo visivyo vya Kiserikali. Utaratibu unaohitajika kama unavyofahamu Mheshimiwa Maria Watondoha, kwa sababu amewahi kufanya kazi pale Makao Makuu ya Wizara. Cheti kinachotolewa na shule au taasisi yoyote isiyio ya Serikali kinahitajika kiwasilishwe Wizarani halafu kuna Kamati maalum ambayo itakifanyia tathmini na kuweza kukitamka kinalingana vipi na vile vyeti vya Serikali. Kwa hiyo, ndio utaratibu na wajibu wa kufanya hivyo ni wa wale wenye vyuo kwa sababu wakichukua hatua wale wenye vyuo vikatambulika na Wizara yangu basi na soko lao linaongezeka kwa sababu wale watajua kwamba wakisoma katika vyuo hivyo watapata ajira. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Maria Watondoha, kama anavijua vyuo hivyo, kama wana matatizo, awashauri walete Wizarani tuweze kuviweka katika tathmini kwa mujibu wa utaratibu.

Na. 265

Ukombozi wa Bara la Afrika

MHE. FRANK G. MAGHOBA aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi pekee ilijoitolea kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kuwa Bara la Afrika lote linakuwa huru; na kwa kuwa Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alijitolea Jeshi, fedha na chakula ili vitumike katika harakati za kuzikomboa nchi kadhaa za Bara hili la Afrika:-

(a) Je, ni faida gani ambayo Watanzania wamepata kutokana na kujitolea mhanga kulikomboa Bara hili?

(b) Je, ni wanajeshi wangapi walipoteza maisha yao katika harakati za ukombozi, walizikwa wapi na ni kiasi gani cha fidia kilitolewa kwa wanajeshi waliokufa kutokana na kulitetea Bara hili?

(c) Katika harakati za kulikomboa Bara letu la Afrika, tumetumia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu na kufanya Watanzania waishi maisha ya kubahatisha kutokana na kudidimia kwa uchumi wetu, je, ni nchi ngapi tulizosaidia ukombozi wake, zenyе uchumi mzuri na ambazo zimetusaidia kuboresha uchumi wetu uliodidimia kutokana na kujingiza katika harakati hizo za ukombozi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Frank Maghoba, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tanzania ilijitolea kwa kiasi kikubwa katika harakati za ukombozi wa Afrika. Hata hivyo, haikuwa nchi pekee iliyofanya hivyo Barani Afrika. Nchi nyingi Barani Afrika na kwingine duniani zilishiriki na kujitolea kwa hali na mali. Kwetu sisi ni jambo la kuleta faraja na heshima kuona kuwa jitihada zetu hizo zimezaa matunda yaliyotazamiwa na kwamba ukoloni mkongwe na ubaguzi wa rangi vimetokomezwa Barani Afrika. (*Makofi*)

Baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nijibu swalii la Mheshimiwa Frank Maghoba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakati wa Rais wa Kwanza wa nchi yetu Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alipoongoza Watanzania katika harakati za ukombozi na Watanzania kuridhika na uongozi wake huo hakufanya hivyo kwa nia ya kutafuta manufaa binafsi au kwa nchi yetu bali aliongozwa na kutambua wajibu wa kihistoria wa mwanadamu aliye huru kuwasaidia wanadamu wenzake wanaotawaliwa, wanaokandamizwa na kunyanyaswa na wakoloni na wabaguzi wa rangi. Manufaa ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kwa nchi yetu yangekuwa ni matokeo na siyo msingi wala lengo. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, katika harakati za vita vya ukombozi, wanajeshi wetu kadhaa wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania walishiriki bega kwa bega na wananchi wenzetu wa Afrika waliokuwa wanapigania uhuru na ukombozi. Katika

ushiriki huo wapo waliopoteza maisha yao ama kwa kuuawa ama kwa kuumwa na wapo walioumia. Wanajeshi wa Kitanzania wote waliopoteza maisha yao kwa kupidia kwa ndugu zao wote walisafirishwa na kuzikwa nyumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, endapo kuna baadhi ambao hawakusafirishwa ni kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wetu kama vile mwili kuharibika vibaya sana, kutotambuliwa au kutokupatikana kabisa. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa jamaa ya wale waliokufa na wale walioumia wamelipwa stahili zao kwa mujibu wa sheria za ulinzi na taratibu husika.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tanzania ilitoa mchango wa hali na mali katika harakati za ukombozi hasa wa nchi za Kusini mwa Afrika. Lakini, si kweli kwamba tumetumia kiasi kikubwa cha uchumi wa nchi yetu na kuwafanya Watanzania waishi maisha ya kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa gharama zote za uendeshaji wa harakati za ukombozi wa Afrika zilitoka katika mfuko maalum wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (*OAU*) wakati ule uliokuwa unachangiwa na nchi zote wanachama na marafiki wa Bara letu Tanzania ikiwa mionganoni mwake. Gharama hizo hazikuwa zinabebwa na Serikali ya Tanzania na wala Serikali haikuwa na bajeti maalum kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, tulipochangia harakati za ukombozi tulikuwa tunatimiza wajibu wetu mtakatifu kama wanadamu kwa wanadamu wenzetu waliohitaji msaada huo na kustahili msaada wetu. Hatukutoa mkopo na wala hatukusaidia na hivyo kutaraji kwamba hatimaye watulipe. (*Makofii*)

MHE. FRANK G. MAGHOBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa kama alivyosema Waziri tumejitolea kwa kiasi kikubwa na hatuwezi kudai...

SPIKA: Ngoja, hatuwezi kusikia vizuri, hebu soga pale, soga *microphone* karibu.

MHE. FRANK G. MAGHOBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa Waziri amesema kwamba tulijitolea na hatuwezi kudai fidia kwa sababu nia yetu ilikuwa ni kuwakomboa wenzetu ambao walikuwa katika ukoloni, je, sasa Serikali yenye nchi yetu ina mpango gani kuwasaidia wanajeshi ambao ni walemvu na ambao sasa hawawezi kutumika tena Jeshini wakiwa wanaishi katika hali mbaya? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyooleza katika jibu langu la msingi kwamba jamaa ya waliokufa na wale ambao waliumia katika harakati hizo wote

wamelipwa stahili zao kwa mujibu wa utaratibu na kanuni zilizowekwa za Jeshi.
(Makofî)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, wanajeshi wetu kweli walifanya kazi kubwa na wameweka historia kubwa sana na wametuletea sifa katika Bara letu la Afrika. Wanajeshi waliozikwa nje ya nchi, mpango umeandaliwa kurudisha mabaki yao na watazikwa kama mashujaa, makaburi yameandaliwa katika Mkoa wa Mtwara nayo itakuwa ni sehemu ya sherehe ya miaka 40 tangu kuundwa kwa Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanajeshi wale mavu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaandaa sera ambayo ikikamilika itashughulikia wanajeshi walioumia na amba ni wale mavu. *(Makofî)*

Na. 266

Kampeni za Kupambana na UKIMWI Nchini

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA aliuliza:-

Kwa kuwa Kampeni dhidi ya Ugonjwa wa UKIMWI zimetiliwa mkazo na Serikali kupitia *TACAIDS*; na kwa kuwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali yameelekeza nguvu zake kwa jamii ya Mijini zaidi kuliko Vijijini; na kwa kuwa hivi sasa wapo watu wengi wanaotokea sehemu mbalimbali kuingia kwenye maeneo ya migodini, uvuvi au kwenye masoko kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibashara; na kwa kuwa wote hao hawapati elimu hiyo ya kupima UKIMWI na kupata ushauri nasaha:-

- (a) Je, ni lini shughuli za kupima UKIMWI na kutoa ushauri nasaha kwa waliothirika zitafikishwa Vijijini?
- (b) Je, isinge kuwa vyema Serikali ikaelekeza nguvu na uwezo wake zaidi Vijijini kwa sababu misaada minge inayotolewa na wahisani huishia Mijini tu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inapanua utoaji wa huduma za ushauri nasaha kwa awamu kwa kuanzia na Hospitali za Mikoa na Wilaya. Hadi sasa hivi huduma hizi zinapatikana katika vituo 360 vilivyopo kwenye Wilaya zote hapa nchini. Upanuzi wa huduma hii unaendelea kwa utoaji wa mafunzo kwa wataalam wa afya ili hadi kufikia mwaka 2006 kila Wilaya iwe na angalau vituo 6 vya umma vyenye uwezo wa kutoa huduma za ushauri nasaha. Baada ya hapo, itafanyika mipango ili vituo vya afya navyo viweze kutoa huduma hii. Kutokana na idadi kubwa ya Wilaya na watumishi amba

watahusika katika huduma hii, upanuzi hadi ngazi ya zahanati utachukua muda mrefu. Hata hivyo, Wizara ya Afya inafanya kazi kwa kushiriki na wahisani mbalimbali ili kuweza kufupisha muda wa kufikia lengo hili.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali hupanga utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia msingi wa usawa (*equity*). Kwa msingi huo, mipango yetu ya huduma italenga kuwafikia wote wale wenye mahitaji muhimu na wale walioathirika zaidi bila kujali kuwa wanaishi mijini au Vijijini. Wahisani wanapojitokeza kutusaidia katika shughuli zetu tutawaelekeza kwa kuzingatia msingi huu.

SPIKA: Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga ameridhika, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibowi.

Matangazo ya vikao ni kwamba, Kamati mbili zimepangiwa kufanya vikao vyake leo. Kamati hizo ni Kamati ya Maliasili na Mazingira, inaendelea na kikao chake leo saa saba mchana ghorofa ya pili ukumbi namba 231.

Kamati nyingine ni Kamati ya Uwekezaji na Biashara, nao watakuwa na kikao leo saa 5.00 asubuhi hii kwenye chumba namba 227 ghorofa ya pili. Hivyo ni vikao vya leo.

Semina za kesho na kesho kutwa ni kwamba, kesho Jumamosi kutakuwa na semina ya Wabunge wote juu ya Maendeleo ya Simu Tanzania ambayo imeandaliwa na Kampuni ya Simu, inaanza saa 3.00 asubuhi kama kawaida.

Keshokutwa Jumapili, kutakuwa na semina kuhusu shughuli za *CAMARTEC* ile ya Arusha kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge juu ya shughuli zao. Kwa kuwa ni Jumapili, semina itaanza saa 5.00 asubuhi katika ukumbi huu wa Bunge.

Mwisho wa matangazo. Katibu, tunaendelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, kutohana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2004/05.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze hotuba yangu kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mwenza wa Tume ya Utandawazi Duniani, kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), kuteuliwa kuwa Kamishna katika Kamisheni ya Afrika iliyoanzishwa na Waziri Mkuu

wa Uingereza, Mheshimiwa Tony Blair, kuwezesha kukamilishwa kwa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya Ushuru wa Forodha na kwa mchango wake mkubwa katika kusuluhiha migogoro ya nchi zilizoko kwenye eneo la Maziwa Makuu. Sifa hizi zinatufanya Watanzania tutambulike na kuheshimika na Mataifa mengine duniani kote. Tumejivunia pia uteuzi wa Profesa Anna Tibajuka, ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Makazi, kuwa mmoja wa Wajumbe wa Kamisheni hiyo ya Afrika na tunampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa juhud zake kubwa za kuimarisha Muungano na kwa kuhamasisha utekelezaji wa Sera mbali mbali za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ambayo imekuwa dira ya mjadala wetu hapa Bungeni. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao zilizofafanua kwa kina mwelekeo wa uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Vile vile napenda kwa namna ya pekee kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, kwa ushauri na hekima za Kamati yake ambazo zimesaidia sana uchambuzi wa Bajeti ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka uliopita wa fedha yapo matukio muhimu yaliyojitezea katika Taifa letu. Ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Hii ni mara ya pili kwa Mheshimiwa huyo kuleta msisimko na sifa ya aina yake Tanzania kwani itakumbukwa kuwa aliteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuwa Katibu Mkuu wa Mkutano wa Wanawake Duniani uliofanyika huko Beijing, China mwaka 1995. (*Makofi*)

Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambye, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Mazingira, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Mbunge wa Maswa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Tume ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia na Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge wa SADC. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wapo Wabunge wengine waliochaguliwa kuwa Wabunge wa Afrika, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini na Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mbunge wa Dimani, Zanzibar.

Napenda pia kuungana na Mawaziri wenzangu waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa

Mbunge, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki kuptitia CCM, kwa kuchaguliwa tena kwa kishindo katika uchaguzi mdogo uliofanyika mwezi Mei, 2004. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kukushukuru wewe, Mheshimiwa Naibu Spika na kuwapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, utulivu na hekima kubwa. Nawashukuru vile vile Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri ya kukusaidia wewe, Mheshimiwa Spika na kutuongoza vizuri ukiwa haupo kwenye kit. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni wapo Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopatwa na matatizo mbalimbali kama vile ajali barabarani, kuvamiwa na majambazi, kufiwa na wapendwa wao na kadhalika. Napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole na kuwatachia nafuu ya haraka. Waheshimiwa hao ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao.

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Anna Nyinamtemi Kilango Malecela, kwa kuvamiwa na majambazi, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa kupata ajali. Mwenyezi Mungu awapoze na awape faraja.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge letu Tukufu, lilipata msiba. Mheshimiwa Yeti Sintemule Mwalyego, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, alitutoka ghafla. Napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kutoa pole kwa familia ya marehemu, kwako wewe Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya. Tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, napenda kuchukua fursa hii sasa kufanya mapitio ya utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2003/2004 na makusudio ya utekelezaji katika kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu uliongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kuondoa Umaskini, Sera ya Maendeleo ya Jamii, Sera ya Maendeleo ya Mtoto na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia.

Aidha, Wizara yangu inaendelea kuongozwa na dira yake ya kuwepo kwa jamii yenye uwezo thabiti wa kutambua matatizo yanayoikabili, kuyachambua na kuyawekea mikakati ya kuyatatuwa kwa kutumia raslimali zilizopo ili kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Dira hii inatekelezwa kwa kupitia sera na miongozo mbalimbali zikiwemo Sera za Wizara katika maeneo ya Maendeleo ya Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Jinsia na Maendeleo ya Watoto na Familia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Jamii iliyozinduliwa mwaka 1996 inaendelea kutekelezwa kwa mafanikio. Mafanikio yaliyopatikana ni kuzingatiwa na kuingizwa kwa maudhui ya Sera hiyo ambayo ni ushirikishwaji jamii katika sera nyingine za kisekta na kijumla. Matokeo yake ni kuwa programu na mipango mbalimbali ya maendeleo imetekelizwa kwa mafanikio makubwa kutokana na ushiriki wa jamii katika ngazi ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi na programu zilizofanikiwa kutokana na ushiriki mkubwa wa wananchi ni pamoja na Mpango wa Uhuru, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto (*CSPD*), Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (*MMEM*) na Programu ya Kuimarisha Sekta ya Kilimo (*ASDP*).

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba nitawasiliana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu suala la Vikosi vya Ujenzi kuhamishwa kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii kwenda Idara ya Ujenzi katika Halmashauri. Mawasiliano hayo yamefanyika na Wizara imehakikisha kuwa hakuna mwongozo uliotolewa wa kuhamishia vikosi hivyo kwenye Idara ya Ujenzi. Wizara inasisitiza kwamba majukumu ya vikosi hivi hayafanani na yale ya Idara ya Ujenzi kwa kuwa mafundi wa vikosi hivi wana mbinu na stadi za ufundi pamoja na taaluma ya maendeleo ya jamii. Kwa mantiki hiyo, vikosi hivyo havipaswi kuunganishwa na Idara ya Ujenzi. Wizara inawaomba Waheshimiwa Wabunge wasaidie kuhakikisha vikosi hivyo vinabakia katika Idara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa vikosi vya Ujenzi na mafunzo ya ufundi katika utekelezaji wa miradi ya kujitegemea kama vile ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, zahanati, miradi ya maji na ujenzi wa nyumba bora vijijini. Ili kuziwezesha Halmashauri kutekeleza jukumu hili, Wizara yangu katika mwaka 2003/2004 ilitoa mafunzo ya rejea kwa mafundi 30 wa Vikosi vya Ujenzi na Mafunzo ya Ufundu kutoka Wilaya za Bagamoyo, Handeni, Iringa, Kibaha, Kinondoni, Kisarawe, Korogwe, Lushoto, Mafia, Mafinga, Makete, Muheza, Pangani na Tanga. Mafunzo hayo yamewawezesha mafundi kuwa na upeo mkubwa zaidi katika kuwasaidia Wananchi kutekeleza miradi yao ya kujitegemea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwa matumizi ya sayansi na teknolojia ni kigezo muhimu cha kupima mabadiliko ya kimaendeleo yanayotokea katika jamii. Katika nchi yetu mabadiliko hayo hayana budi kupimwa kuanzia vijijini ambako Wananchi wengi huishi na kujishughulisha na kazi mbali mbali za uzalishaji mali. Ili kuwawezesha Wananchi kuzifahamu teknolojia mbali mbali, Wizara yangu imeandaa na inaendelea kusambaza Kitita cha Teknolojia Sahihi kwa wadau mbalimbali. Matumizi ya kitita hicho yatawawezesha wadau hao kuongeza kasi ya matumizi ya sayansi na teknolojia sahihi katika utekelezaji wa shughuli zao za maendeleo.

Aidha, watafafamu baadhi ya teknolojia zinazoweza kupatikana hapa nchini ambazo ni sahihi katika mazingira yao. Miiongoni mwa teknolojia hizo ni zile

zinazohusiana na maji na usafi wa mazingira, nishati ya nyumbani, kilimo, usafiri na usafirishaji na ujenzi wa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wanalo jukumu la kuwawezesha wananchi kupata utaalama, ujuzi na stadi mbali mbali za kujiletea maendeleo yao. Kwa kutambua umuhimu huo, Wizara yangu katika mwaka 2003/2004 iliongeza michepuo miwili ya mafunzo ya Stashahada ya Juu katika Jinsia na Maendeleo na Upangaji na Uendeshaji Shirikishi wa Miradi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Baada ya kuongezeka kwa kozi hizo mbili, Chuo kimekuwa na uwezo wa kuchukua jumla ya wanachuo 230 kwa mwaka badala ya 70. Hivyo ifikapo mwaka wa masomo 2005/2006 Chuo kitakuwa na jumla ya wanachuo 700. Aidha, kozi hizo mbili zitaongeza upatikanaji wa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ambao wanahitajika sana katika hatua mbali mbali za kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma mbalimbali na kukidhi mahitaji ya malazi yaliyotokana na ongezeko la wanachuo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Wizara yangu ilipanga kutekeleza miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni ukamilishaji wa ujenzi wa bweni, uchimbaji wa kisima kirefu cha maji, ununuzi na uwekaji wa pampu na matanki ya maji, ujenzi wa vyoo pamoja na ununuzi na ukarabati wa samani. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imetumia Shillingi milioni 117.2 kwa kutekeleza kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kukidhi mahitaji ya Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata na Vijiji, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Misungwi na Rungemba vimeendelea kutoa mafunzo ngazi ya cheti. Katika mwaka 2003 jumla ya wanachuo 182 wakiwemo wanawake 135 na wanaume 47 walihitim u mafunzo hayo ikilinganishwa na mwaka 2002 ambapo walihitim u wanachuo 116 wakiwemo wanawake 89 na wanaume 27. Wataalam hao huajiriwa katika ngazi za Kata na Kijiji hivyo wana umuhimu wa pekee katika kuleta chachu ya maendeleo katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kutoa ujuzi na stadi mbali mbali kwa Wananchi kama nyenzo muhimu kwao katika kuongeza uelewa, tija, ufanisi na uwezo wa kujiajiri. Kwa kutambua hili, katika mwaka 2003/2004 Wizara iliwapatia Wananchi 23,086 mafunzo na stadi mbalimbali kuitia Vyuo 58 vya Maendeleo ya Wananchi. Kati ya hawa, wanawake walikuwa 10,554 na wanaume walikuwa 12,532. Katika kipindi hiki Wananchi 3,728 wakiwemo wanawake 1,949 na wanaume 1,779 walipatiwa mafunzo nje ya vyuo (*outreach training*). Mafunzo hayo yalijumuisha kilimo cha mazao ya biashara, ufugaji, miradi ya maji vijijini, kuzuia kuenea kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI, kuzuia uharibifu wa mazingira na mengineyo kulingana na mahitaji ya Wananchi mahali chuo kilipo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana, Wizara yangu iliahidi kufanya ukarabati mdogo na mkubwa kwenye baadhi ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Ukarabati mdogo ulipangwa kwa vyuo 24 ambapo ukarabati mkubwa ulipangiwa vyuo 12.

Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu, kwamba Wizara imetekeleza jukumu hilo kwa kutoa kiasi cha shilingi milioni 270 zilizowezesha kufanya ukarabati mdogo wa majengo na miundombinu kwa vyuo 28. Aidha, vyuo 12 vilipelekewa jumla ya shilingi milioni 145 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa majengo na miundombinu. Vyuo hivyo ambavyo ukarabati wake unaendelea ni Chisalu (Dodoma), Gera (Kagera), Karumo (Mwanza), Kihinga (Kigoma), Kilosa (Morogoro), Kisangwa (Mara), Mabughai (Tanga), Mlale (Ruvuma), Monduli (Arusha), Mtawanya (Mtwara), Ruaha ((Iringa) na Sofi (Morogoro).

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba kuenea kwa virusi vya UKIMWI kwa sehemu kubwa kunachangiwa na tabia. Wizara kuptitia Vyuo vyake vya Maendeleo ya Wananchi imeendelea kutoa elimu ya kudhibiti kuenea kwa virusi vya UKIMWI kwa jamii. Vile vile, Wizara iliwaelimisha Watendaji wa Maendeleo ya Jamii, katika ngazi mbalimbali juu ya kutumia Mkakati wa Kijamii wa Kuwakinga Wanawake na Watoto dhidi ya UKIMWI. Mkakati huo unasisitiza kwamba jitihada za uhakika za kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI hazina budi kuchukuliwa na watu wenyewe, familia na jamii zinazowazunguka. Katika kutekeleza mkakati huo Vyuo vyote 58 vya Maendeleo ya Wananchi vimekuwa Vituo vya Elimu ya UKIMWI mahali pa kazi na kwa maeneo yanayovizunguka. Hali kadhalika, Wizara imeshiriki katika maandalizi ya uendeshaji wa mafunzo kwa Kamati za Kudhibiti UKIMWI katika Halmashauri. Mpango huo ulibuniwa na kugharamiwa na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*).

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jinsia ni muhimu katika maendeleo ya jamii. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia inahimiza uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sera za Sekta mbalimbali, mipango na miradi. Katika kipindi cha 2003/2004, Wizara yangu iliendelea na juhudzi za kusimamia na kufuutilia uingizwaji wa masuala ya jinsia katika mikakati, mipango, programu na mitaala ya Sekta mbalimbali zikiwemo afya, elimu ya juu na kilimo. Aidha, kama nilivyoahidi mwaka jana, sera hiyo imeshachapishwa katika lugha ya Kiingereza na kusambazwa ili kuwezesha wadau wasiojua Kiswahili kuitumia.

Vile vile, Sera hiyo imetafsiriwa katika lugha nyepesi ya Kiswahili ili iweze kueleweka na watu wengi zaidi na hivyo kutekelezwa katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 katika Bunge lako Tukufu niliahidi kuwa, Wizara yangu itakamilisha utayarishaji wa mwongozo wa kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia. Wizara yangu imeandaa mwongozo huo na inaendelea na zoezi la kukamilisha Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia (*National Strategy for Gender Development*). Mkakati huo utawezesha wadau mbalimbali kuwa na mtazamo wa pamoja katika kutekeleza masuala ya jinsia na hivyo kuharakisha upatikanaji wa usawa wa jinsia. Aidha, mkakati utabainisha majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wa Sera.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia pamoja na mambo mengine inahimiza kuundwa kwa Dawati la Jinsia katika Sekta mbalimbali.

Katika kutekeleza azma hiyo, Asasi mbalimbali zinaendelea kuteua watumishi watakaoshughulikia Dawati hilo, ambao ndio watakaoratibu uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, mipango, mikakati na miradi ya Sekta zao. Lengo la Wizara yangu ni kuwa na Dawati la Jinsia katika kila Wizara, Mkoa, Halmashauri, Idara na Taasisi zote za Serikali. Mpaka sasa jumla ya Madawati ya Jinsia 84 kati ya 171 yanayotarajiwu yameundwa katika Wizara, Mikoa, Halmashauri na Idara zinazojitegemea. Madawati hayo ni viungo kati ya Sekta husika na Wizara yangu kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa maendeleo ya jinsia nchini. Kupitia Madawati yaliyoundwa Wizara yangu imeanza kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maendeleo ya Jinsia katika Sekta mbalimbali. Taarifa hizo zimesaidia katika uandaaji wa taarifa za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, masuala ya jinsia yanashughulikiwa na wahusika wengi kama vile Jamii, Ofisi za Serikali, Wizara, Mikoa, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na Wahisani. Kwa vile dhana ya jinsia hajaelewka vizuri na wengi, Wizara yangu kama ilivyoahidi mwaka jana imetoa mafunzo kwa watendaji 37 kati ya 85 walioteuliwa. Mafunzo hayo yamewapatia uelewa mpana katika masuala ya jinsia na maendeleo. Kupitia madawati hayo, baadhi ya Wizara na Taasisi zimeanza kuhamasisha na kutoa elimu ya jinsia katika sehemu zao za kazi. Wizara na Taasisi hizo ni pamoja na Wizara za Afya, Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi na iliyokuwa Tume ya Utumishi ya Walimu. Napenda kuzipongeza Wizara na Taasisi hizo kwa jitihada zao ambazo zinfaa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, kutohana na ukweli kuwa Sekta binafsi ni muhimu katika maendeleo ya jamii, masuala ya jinsia hayana budi kuzingatiwa katika Sekta hiyo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zisizo za Kiserikali imeendelea kueneza dhana ya uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango kwa watendaji wa ngazi mbalimbali katika Sekta binafsi.

Katika mwaka 2003/2004 Wizara yangu ilishirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Taasisi ya Sekta Binafsi (*Private Sector Foundation*) na Shirikisho la Viwanda Tanzania, kuendesha mafunzo ya jinsia kwa watendaji wa Sekta binafsi na Sekta za Umma kwa ufadhili wa *UNIDO*. Mafunzo hayo yametoa uelewa mpana wa maendeleo ya jinsia katika Sekta ya Viwanda na Biashara. Washiriki hao wanatarajiwu kuchangia katika kuleta mabadiliko katika mifumo ya ajira kwenye Sekta rasmi na isiyo rasmi na kutoa haki sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira, aina za kazi, uongozi na utawala, usalama kazini na katika kukidhi mahitaji ya kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Chama cha Wanasheria Wanawake (*TAWLA*) iliendesha mafunzo kuhusu demokrasia, ushirikishwaji na usawa wa jinsia. Walioshiriki mafunzo hayo walikuwa ni Wanawake Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wabunge wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Makatibu wa Vyama vya Siasa na Wawakilishi wa Wyama visivyo vya Kiserikali. Mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha washiriki kutambua umuhimu wa demokrasia inayozingatia usawa wa jinsia na viti maalum kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nyingi za Serikali katika kuhimiza usawa wa jinsia, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia imeelekeza kuanzishwa kwa Chombo cha Wanawake ambacho hakitafungamana na itikadi ya kidini wala kisiasa. Chombo hicho kitasimamia na kufuutilia maendeleo ya wanawake.

Wizara yangu imeendelea na jitihada zake za kuwezesha uundaji wa Chombo hicho ambacho kimependekezwa kuwa katika mfumo wa Tume. Wizara yangu imekwishapokea mapendekezo ya mwongozo wa jinsi ya kuunda Tume hiyo kutoka Kamati ya Mpito ilioundwa kusimamia uundwaji wa Chombo hicho. Mapendekezo hayo hivi sasa yamefikia ngazi ya juu ya kufanyiwa kazi Serikalini. Chombo hicho kikiundwa kitasaidia sana kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji wa masuala ya usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeridhia Mikataba na Maazimio mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa ambayo inapaswa kutekelezwa. Mojawapo ya mikataba hiyo ni Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (*CEDAW*). Wizara yangu kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Wanawake ya Umoja wa Mataifa (*UN-DAW*), iliendesha mafunzo ya namna ya kuingiza masuala ya Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake katika sheria za nchi kwa Majaji wa Mahakama kutoka nchi 14 za Afrika.

Mafunzo hayo yamewawezesha Majaji hao kuelewa jinsi ya kuoanisha masuala ya Mkataba huo na utekelezaji wa sheria mbalimbali za nchi. Majaji hao watakuwa chachu katika kuleta usawa wa jinsia katika jamii kupitia maamuzi yao.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya namna ya kuandaa taarifa za nchi kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake, yalitolewa kwa Viongozi na Maafisa wanaoshughulikia masuala ya jinsia kutoka nchi 14 za Afrika. Ujuzi uliopatikana katika mafunzo hayo utawawezesha wataalam hao kuutumia kikamilifu katika kuandaa taarifa za nchi za utekelezaji wa Mkataba huo kwa kufuuta mfumo mmoja ulioelekezwa na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa hutakiwa kutia saini na kuridhia Mikataba ya Kimataifa inayopitishwa. Katika kutekeleza hilo, mwaka 2004 Wizara yangu imeridhia Itifaki ya Nyongeza kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake. Itifaki hii ni sehemu ya mkataba huo na inaweka utaratibu ambao wanawake wanaovunjiwa haki katika nchi zao, wataweza kuwasilisha malalamiko katika Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake.

Mikutano ya Kimataifa na kikanda hutumika kuboresha utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyoridhiwa na kuptisha mikakati ya kuboresha utekelezaji wa mikataba hiyo. Aidha, maazimio hutolewa kwenye mikutano hiyo kuhusu utekelezaji wake. Wizara yangu imeshiriki mikutano mbalimbali ya Kimataifa ukiwemo wa Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki ya Wanawake (*CSW*) mwezi Machi, 2004 huko New York Marekani. Mikutano huu ulisisitiza wajibu wa wanaume na wavulana katika kuleta

usawa wa jinsia na ushiriki wa wanawake katika kusuluhiha migogoro ya kivita na kudumisha amani duniani baada ya vita.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imetia saini Azimio la Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Jinsia na Maendeleo na nyongeza ya Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake. Azimio hili linahitaji kutekelezwa na kutolewa taarifa kila mwaka kuhusu utekelezaji wake na kutoa taarifa kwenye Mikutano ya Kikanda. Wizara yangu imeendelea kushiriki na kuitoa taarifa hiyo kwenye mikutano mbalimbali ya Kikanda ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) iliyohusu masuala ya jinsia. Taarifa hizi zimewezesha nchi kujipima kwa kuzingatia hatua iliyofikiwa katika kuleta usawa wa jinsia na maendeleo ya wanawake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia imeshiriki katika mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuandaa rasimu ya kiunzi cha Afrika Mashariki cha Jinsia na Maendeleo ya Jamii. Kiunzi hicho kitakapokamilika kitatumiwa na nchi wanachama katika kuleta usawa wa jinsia katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, taarifa ni nyenzo muhimu katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Wizara yangu inacho Kituo cha Habari cha Wanawake (*Women's Information Centre*) ambacho kimeanzisha sehemu maalum (*Women's Information Window*) ambayo inatoa ushauri kwa wanawake wanaotafuta kazi, nafasi za masomo na uhisani. Kituo kinawapa wanawake mbinu za kushiriki katika usaili wa kazi na jinsi ya kuandika maombi ya kazi. Kituo hicho kimesaidia wanawake waliokuja kukitembelea na kuomba huduma. Hata hivyo, Wizara itaendelea na jitihada za kukitangaza kituo hicho kwa nia ya kuwavutia wanawake wengi waje kupata ushauri.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imefanya utafiti wa kuainisha uwezekano wa kuwa na utaratibu utakaowezesha uanzishaji na uendeshaji bora wa biashara zinazofanywa na wanawake. Utaratibu huo unawalusisha wafanyabiashara katika maandalizi, uanzishaji hadi utekelezaji wa mradi. Utafiti uliofanyika katika Mikoa ya Iringa na Dar es Salaam umeonyesha kuwa utaratibu huo unafaa katika biashara za usindikaji wa vyakula, kazi za mikono na ushonaji na utawasaidia wanawake wengi zaidi hasa kwa wale ambaa baada ya kupatiwa elimu inawawia vigumu kuanzisha biashara.

Mheshimiwa Spika, wanawake wengi wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na kukosa mikopo na uwezo mdogo wa kuingia kwenye ushindani katika utandawazi na soko huria. Serikali imekuwa ikiratibu uwezekano wa kuanzisha Benki za Wanawake ili kuwakomboa kiuchumi. Mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hatua tuliyofikia katika mchakato wa kuwezesha uanzishaji wa Benki hizo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu uanzishaji wa Benki hizo ambazo zinakusudiwa kuendeshwa kwa mfumo wa Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa mchango wake katika kuwaimarisha wanawake kiuchumi kwa kutoa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (*WDF*). Fedha za Mfuko huo awali zilikuwa zinatumwa moja kwa moja kwenye Halmashauri ambako zilikuwa zinachanganywa na fedha za Mfuko wa Vijana na za Halmashauri.

Baada ya kutambua upungufu huu, Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI ilibadilisha utaratibu huo wa kutuma fedha na kuanzisha utaratibu wa kufungua akaunti maalum ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na kuingia mikataba na Halmashauri. Utaratibu huo umewezesha Halmashauri zote kufungua akaunti maalum. Aidha, utaratibu huo umeongeza ufanisi katika udhibiti, ufuatiliaji na urejeshwaji wa fedha za Mfuko.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Wizara yangu pia imetayarisha Mwongozo unaoelekeza namna ya kuendesha Mfuko huu katika ngazi mbalimbali. Utekelezaji wa Mwongozo huo umezifanya Halmashauri zote kuwa na utaratibu wa aina moja wa kugawa fedha na kufuatilia, ambao umewezesha Halmashauri nyingi kufanya marejesho.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa masoko ni tatizo linalowakabili wanawake wengi wafanyabiashara. Wizara yangu iliendelea kuratibu na kuwezesha wanawake kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (*DITF*) yaliyofanyika Dar es Salaam mwezi Julai, 2003. Kazi hii iliwezekana kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), Wizara ya Viwanda na Biashara, Halmashauri za Wilaya na Miji na Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (*FAWETA*). Tunawashukuru sana washirika wetu hawa.

Ili kuwawezesha wanawake kufanya biashara zao kwa ufanisi zaidi, Wizara yangu mnamo mwezi Septemba, 2003 iliendesa mafunzo ya utumiaji wa vyombo vya mawasiliano katika biashara na jinsi ya kujitangaza kutafuta masoko. Mafunzo hayo yaliwashirikisha wanawake wafanyabiashara 65 waliokuwa wameshiriki katika maonesho ya biashara ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, Mwenyekiti wa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote kwa jitihada zake na kwa kupitia Mfuko huu, wanawake wengi wamepata mafunzo, bidhaa zao zimetangazwa nje na za nje zimeletwa hapa nchini ili waweze kuziona na kujipima. Juhudi hizi za *EOTF* zimewawezesha wanawake kadhaa kupata masoko ya ndani na nje ya nchi. Hivi karibuni vikundi kadhaa vilijigharamia wao wenye kushiriki Maonyesho ya *SADC* ya WanawakeWafanyabiashara yaliyofanyika tarehe 21-27 Juni, 2004 huko Gaborone, Botswana. Katika maonyesho hayo, mojawapo ya vikundi vilivyopata mafunzo ya *EOTF* kiitwacho *QualiCloth Limited* cha Dar es Salaam kilishinda tuzo ya kwanza kwa bidhaa zinazotokana na vitambaa (mavazi, vikoi na batiki). Wizara yangu inawapongeza sana wanawake walioshiriki maonyesho haya na tunatumaini jitihada na ari walionayo itawawezesha kupenya kwenye soko la *AGOA*, *EBA* na mengineyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kufuatilia na kutathmini maendeleo ya wanawake nchini tumekuwa tukiadhimisha siku ya Wanawake Duniani kama njia mojawapo ya kutafakari shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na wanawake. Wizara yangu imekuwa na kawaida ya kushirikiana na Wizara ya Vijana, Ajira, Wanawake na Maendeleo ya Watoto, Zanzibar. Ushirikiano huo ni wa kuimarisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya wanawake na jinsia nchini.

Mwezi Machi, 2004 Wizara yangu ilishirikiana na Wizara hiyo, katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Kitaifa maadhimisho hayo yalifanyika Mkoa wa Kusini Unguja na kauli mbiu ilikuwa Zingatia jinsia kwa Maendeleo. Ujumbe huu ulilenga kuchochea ari ya Wananchi kuzingatia usawa wa jinsia katika kupanga mipango na kutekeleza shughuli zao za maendeleo katika ngazi zote.

Maadhimisho hayo pia yalitoa fursa kwa shughuli mbalimbali zinazofanywa na wanawake wa Tanzania kuonekana na hivyo kuwawezesha kutathmini kibiashara na ubora wa bidhaa zao. Mikoa yote ya Tanzania Bara ilielekezwa kuandaa na kuadhimisha siku hiyo na vyombo vya habari vilitumika kutangaza ujumbe wa siku hiyo nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha watoto wote wanapatiwa haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kutobaguliwa na kushirikishwa katika maendeleo ya Taifa. Hii itasaidia kupata watoto walioayarishwa kikamilifu kuwa raia bora na nguvu kazi ya kukuza uchumi wa familia zao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nilieleza kuhusu juhudhi mbalimbali za kuendeleza familia hapa nchini. Napenda sasa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu imetayarisha rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Familia na hivi sasa ipo katika hatua za kukamilishwa. Sera ya Maendeleo ya Familia inalenga kuiweshesha jamii kutambua umuhimu wa kuimarisha familia kama chimbuko na kitovu cha maendeleo.

Aidha, Wizara yangu imedurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996 kwa lengo la kuandika Sera mpya ya Maendeleo ya Mtoto. Matayarisho ya Sera hii yamefikia hatua za mwisho kabla ya kuitishwa na Serikali. Lengo kuu la Sera hii ni kuhakikisha kuwa masuala yanayohusu maendeleo na ustawi wa watoto yanapewa umuhimu katika Sera zote za Kiswahili na pia yanatekeleza kuitia mipango na programu mbalimbali za Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imekamilisha utayarishaji wa programu ya Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu kwenye hotuba yangu ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika programu hii inayolenga kujenga maadili mema hasa kwenye ngazi ya familia imeainisha mikakati ya kipaumbele katika kupambana na matatizo ya

umaskini katika familia, afya ya uzazi, UKIMWI, kukosekana kwa usawa wa jinsia katika familia na familia zinazoongozwa na mzazi mmoja na zile zinazoongozwa na watoto. Utekelezaji wa Programu hii ya Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia utakuwa ni mkakati muhimu na wenye tija kubwa kama sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaandaa mpango wa Taifa wa utekelezaji uliotokana na Waraka wa Umoja wa Mataifa uitwao Dunia Iwafaayo Watoto. Katika kutekeleza hilo Wizara imeandaa mwongozo wa kutayarisha mpango huo na kuusambaza kwa wadau ili wautumie katika kuandaa mipango yao itakayojumuishwa katika mpango mmoja wa Taifa. Mwongozo huo umeainisha maeneo ambayo yataingizwa katika Mkakati wa Kuondoa Umaskini. Maeneo hayo ni pamoja na kuboresha afya za watoto, kutoa elimu bora, kupambana na UKIMWI, kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji, unyonyaji na ukatili, ushiriki wa watoto na vijana wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kufuatilia na kuratibu uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa inayohusu haki za watoto. Wizara imekamilisha uandaaji wa Taarifa ya Pili ya Nchi ya Utekelezaji wa Mikataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto, kama inavyoelekezwa na Umoja wa Mataifa. Uandaaji wa taarifa hiyo ulishirikisha Asasi zisizo za Kiserikali ambazo ni pamoja na Mtandao wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayoshughulika na watoto, Kituo cha Haki za Mtoto cha Kuleana, Mtandao wa Maendeleo ya Makuzi ya Watoto, KIWOHEDE, Kituo cha Watoto cha Dogodogo, *Plan (T)* na *Save the Children*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Tanzania kwa kupitia Wizara yangu iliridhia Mikataba mitatu ya Kimataifa inayohusu Haki za Mtoto. Mikataba hiyo ni, Mikataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, Itifaki ya Nyongeza ya Mikataba wa Haki za Mtoto kuhusu Ushirikishwaji wa Watoto katika Migogoro ya Kivita na Itifaki ya Nyongeza kuhusu Biashara ya Watoto, Ukahaba wa Watoto na Upigaji Picha za Udhaililishaji Watoto. Kwa kuridhia Mikataba hiyo, Tanzania imetekeleza Azimio la Umoja wa Mataifa ambalo limezitaka nchi zote Wanachama wa Umoja huo ziridhie Mikataba hiyo. Kadhalika kwa kuridhia Mikataba hiyo, Tanzania itahakikisha kwamba inachukua hatua zote zitakazowezekana ili haki za msingi za watoto zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikiadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika kila ifikapo tarehe 16 Juni, kuanzia mwaka 1991. Madhumuni ya maadhimisho hayo ni kuelimisha, kuhamasisha na kukumbusha wazazi, walezi, Taasisi, Mashirika na Serikali kwa ujumla juu ya wajibu na jukumu letu kwa watoto. Mwaka huu Tanzania iliadhimisha miaka 14 ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa makongamano na shughuli mbalimbali zilizoshirikisha watoto na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa siku hiyo. Kaulimbiu ya mwaka huu inasema: "Fursa Sawa kwa Watoto wote." Lengo la kaulimbiu hii ni kuhakikisha kuwa watoto wote wanapatiwa huduma na haki za msingi ikiwa ni pamoja na kutobaguliwa, kujieleza, kusikilizwa na kupata nafasi ya kuonyesha vipaji vyao.

Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maadhisho haya yalifanikiwa sana kuhamasisha umma kuhusu umuhimu wa kuwapa watoto wote wa kike na wa kiume fursa sawa kwa ajili ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu vile vile iliratibu maadhisho ya miaka 10 ya Siku ya Familia Duniani ambayo yalifanyika Kitaifa huko Kigoma tarehe 15 Mei, 2004. Kaulimbiu ya maadhisho hayo ilikuwa Familia ni Kitovu cha Maendeleo. Kaulimbiu hii inasisitiza kuwa familia ni kitovu cha maendeleo ya jamii, kujenga mshikamano mionganoni mwa wanafamilia, kuhakikisha kunakuwepo usawa baina ya wanawake na wanaume katika familia na kuona umuhimu wa kushughulikia matatizo ya kijamii na kiutamaduni ndani ya familia. Maadhisho hayo pia yalitoa hamasa kwa watu kushiriki kikamilifu kujenga familia imara kwa faida yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu ilikamilisha maandalizi ya mpango wa miaka mitatu wa kuboresha utendaji kazi wa Wizara (*Master Plan*) na ungetekelezwa mwaka wa 2003/2004. Hata hivyo, mpango haukutekelezwa kama ilivyopangwa kwa sababu washirika wetu walihitaji muda wa kuupitia na kutoa maoni yao. Kwa kuanzia, Wizara yangu imeandaa mpango wa mwaka mmoja (*Interim Plan*) ili kutoa nafasi kwa mpango wa miaka mitatu kukamilishwa. Mpango huo utawezesha Wizara yangu kupata ufadhili wa pamoja (*Basket Funding*) na hivyo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu itaweka Tovuti (*Website*) kwa ajili ya kusambaza taarifa zinazohusu Wanawake, Watoto, Maendeleo ya Jamii na Jinsia. Uwekaji huo wa tovuti umekamilika na watakaohusika na kuweka taarifa kwenye tovuti wameshafundishwa. Anuani ya tovuti hiyo ni www.mcdgc.go.tz. Ili kurahisisha mawasiliano na Wizara yangu naomba Waheshimiwa Wabunge waanze kutumia Tovuti hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza maandalizi ya kuanzisha uwekaji wa kumbukumbu zinazohusu wanawake katika kompyuta (*Women's database*). Kazi ya uwekaji kumbukumbu itatekelezwa mwaka wa 2004/2005 na itagharamiwa na Serikali ya Italia. Kumbukumbu hizo zitasaidia Serikali kufahamu wasifu wa wanawake walioko katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Masuala ya Idadi ya Watu (*UNFPA*) ilitayarisha Kitini cha Uhamasishaji kuhusu Jinsia, virusi vya UKIMWI na UKIMWI katika Afrika Kusini mwa Sahara kwa lugha ya Kiingereza. Pia, nilitoa taarifa kuwa Wizara yangu itakitafsiri Kitini hicho katika lugha ya Kiswahili.

Madhumuni ya kutafsiri Kitini hicho ni kukiweka katika lugha inayofahamika na wengi nchini na hivyo kuongeza wigo wa uelewa mionganoni mwa jamii kuhusu masuala mbalimbali yalioainishwa ndani yake. Kitini hicho cha lugha ya Kiswahili kilizinduliwa tarehe 12 Julai, 2004 tulipoadhimisha Siku ya Idadi ya Watu Duniani. Nakala 5,000 za Kitini hicho zimechapishwa na zinaendelea kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kujenga uwezo wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Wizara, Mikoa, Wilaya na Kata. Wizara imeendelea kusimamia ajira za watumishi na maendeleo yao kazini, kuboresha mazingira mazuri ya kazi na kuona kwamba sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa zinafuatwa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana Wizara yangu iliahidi kutekeleza mpango wa Serikali wa kuboresha huduma kwa umma kwa kushirikisha Sekta binafsi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imetekeliza hilo kwa kubinafsisha huduma za usafi wa mazingira katika Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Wizara yangu kupitia Tume ya Utumishi wa Umma iliwapandisha vyeo Maafisa 26. Watumishi 30 wa kada mbalimbali kupitia Kamati Maalum ya Utumishi Serikalini (*KAMUS*) walipandishwa vyeo, watumishi 22 walithibitishwa kazini na watumishi 52 walajiriwa katika masharti ya kudumu baada ya kutimiza sifa na masharti ya kada zao. Aidha, Wizara yangu ilipata kibali cha ajira mpya na kuajiri watumishi watatu wa kada ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu iliwaendeleza watumishi katika nyanja na viwango vya taaluma kama ifuatavyo: -

Watumishi 11 katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili, watumishi 2 mafunzo ya Stashahada ya Juu, Makatibu Mahsus 13 mafunzo ya Uhazili, Wahasibu 5 wamepewa mafunzo ya kuijandaa kwa mitihani ya uhasibu, Msaidizi wa Masjala mmoja ngazi ya Stashahada katika utunzaji kumbukumbu, watumishi watatu mafunzo ya lugha ya Kiingereza na Madreva wawili mafunzo ya udreva mahiri.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliahidi kuimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Jamii kwa kukipatia vifaa na mafunzo kwa wataalam wake. Katika kukiwezesha Kitengo hicho kufanya kazi kwa ufanisi, Wizara yangu imeanza kununua vifaa mbalimbali na inakamilisha taratibu zitakazowezesha Mkuu wa Kitengo kuteuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kusisitiza umuhimu wa Utawala Bora na kupiga vita vitendo vya rushwa, Wizara yangu ilitoa Mafunzo ya Utawala Bora na namna ya Kupambana na Rushwa kwa watumishi 370. Watumishi hao ni wa Makao Makuu ya Wizara, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, watumishi wa Wizara wamepata mafunzo ya kanuni za fedha, ugavi na utumishi wa umma. Elimu hii itawasaidia wafanyakazi kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ni mionganoni mwa Wizara zilizo katika mpango maalum wa Serikali wa kuimarisha huduma zake (*Performance Management Systems*) na imo katika hatua za mwisho za kuandaa mpango/mkakati kama sehemu ya utekelezaji wa mpango maalum wa Serikali wa kuimarisha huduma zake.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2003, Wizara yangu ilifanya Mkutano Mkuu wa Mwaka Mkoani Dodoma. Mkutano huo ulihusisha Viongozi wa Wizara, Maafisa Waandamizi kutoka Makao Makuu ya Wizara, Washauri wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii katika Sekretarieti za Mikoa, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya, Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Wengine ni wawakilishi kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Mkutano huo ulilenga kujadili mikakati mbalimbali ya kuboresha utendaji wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Mikutano ya aina hiyo imesaidia kuimarisha mawasiliano kati ya Wizara na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii walioko Mikoani na Wilayani ambao ndiyo watekelezaji wa Sera za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inao utaratibu wa kufanya mikutano miwili kwa mwaka na Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Zanzibar kwa nia ya kuongeza mashirikiano. Katika mwaka 2003/2004, Wizara hizi mbili zilikutana na kujadili masuala ya maendeleo ya wanawake na jinsia na maendeleo ya mtoto.

Mheshimiwa Spika, aidha, mikutano hiyo ilianda mikakati ya utayarishaji wa taarifa ya pamoja ya nchi kuhusu Mkataba wa Haki za Mtoto na Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake. Vile vile, mikutano hiyo ilitoa mapendekezo ya namna ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani na Siku ya Familia Duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mawasiliano ya karibu na wafanyakazi, Wizara yangu imeendelea kutekeleza agizo la Rais Na. 1 la mwaka 1970 kwa kufanya vikao viwili kwa mwaka vya Baraza la Wafanyakazi. Hatua hii imeongeza uhusiano mzuri kati ya viongozi na wafanyakazi. Vikao hivi vimewevesha wafanyakazi kuzifahamu haki zao, kanuni na taratibu za kazi. Aidha, wafanyakazi wameweza kueleza matatizo yanayowakabili kiutendaji na mapendekezo ya namna ya kuyatatuu.

Mheshimiwa Spika, kutohana na utekelezaji wa majukumu yake, Wizara kwa ujumla imepata mafanikio yafuatayo: -

- Ushiriki wa Wananchi katika maendeleo umeimarika na matokeo yake yameanza kuonekana kupitia programu na mipango mbalimbali ya maendeleo.

- Programu mbili mpya za Jinsia na Maendeleo na Upangaji na Uendeshaji Shirikishi wa Miradi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru zimevutia waombaji kiasi cha kuongezeka kutoka 800 mwaka 2003 na kufikia 2200 mwaka 2004.

- Uelewa wa umuhimu wa masuala ya jinsia ili kuleta usawa kati ya wanaume na wanawake umeongezeka.

- Wanawake wengi wameona umuhimu wa kuongeza uwezo wao kiuchumi kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato.

- Sera za Wizara zimezingatiwa na kuanza kuingizwa kwenye programu na mipango ya Sekta mbalimbali Kitaifa.

- Uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia umeimarika kutokana na kuwepo maafisa wanaoshughulikia Madawati ya Jinsia.

- Baadhi ya wanawake wamepata nafasi katika ngazi za maamuzi.

- Wanawake wengi wameanza kuelewa haki zao na kuzidai na wanaume kwa upande wao wanakubali na kuheshimu haki hizo.

- Kuanzishwa kwa mtandao wa watoto Tanzania kumechangia utekelezaji wa masuala mbalimbali ya maendeleo ya watoto ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto na kuhakikisha kuwa watoto wanashiriki katika kutoa maoni yanayohusu maendeleo na ustawi wao.

- Ushirikiano kati ya Wizara na Mashirika yasiyo ya Kiserikali umeongezeka katika kuanzisha na kuratibu mitandao ya watoto.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyotajwa, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- Ukosefu wa nyenzo na bajeti za kuendeshea ofisi za Idara za Maendeleo ya Jamii katika hal mashauri.

- Uhaba wa wataalam na watumishi katika ngazi zote za Wizara.

- Unyanyasaji wa wanawake na watoto bado unaendelea katika baadhi ya jamii.

- Maendeleo ya wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii bado hayaridhishi.

- Pamoja na jitihada za kuleta maendeleo ya jamii kuna baadhi ya jamii zinabadilika polepole.

- Uwezo mdogo wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kukidhi mahitaji ya waombaji kutokana na uhaba wa majengo, uchache wa vitendea kazi na wakufunzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii sasa kutoa matarajio ya mipango na utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mabadiliko mengi ya kijamii na kiuchumi yanayotokana na utandawazi tangu Sera ya Maendeleo ya Jamii ilipozinduliwa na kuanza kutumika mwaka 1996. Upo umuhimu mkubwa kwa baadhi ya mabadiliko hayo kuzingatiwa na kuingizwa kwenye Sera hii ili iende na wakati. Katika kipindi cha 2004/2005, Wizara yangu pamoja na kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera hiyo, itafanya tathmini ili kubaini mafanikio na upungufu. Ni matumaini yangu kuwa tathmini

hiyo itaiwezesha Wizara kupata taarifa muhimu zitakazotoa mwelekeo wa hali ya baadaye ya Sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa matumizi ya sayansi na teknolojia, Wizara yangu itaendelea kusambaza Kitita cha Teknolojia sahihi na kutoa elimu kuhusu matumizi ya teknolojia mbalimbali. Kwa kuanzia Wizara itatoa mafunzo kwa wakufunzi watakaotoka kwenye Vikosi vya Ujenzi na Mafunzo ya Ufundis vilivyoko kwenye Halmashauri na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Wakufunzi hao wanatarajiwa kutoa mafunzo hayo kwa mwananchi mmoja mmoja na katika vikundi vya uzalishaji mali. Aidha, Kitita kitatumika kuwafundishia wanachuo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na watumiaji wengine wa teknolojia hizo.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa wataalam wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu katika kuharakisha maendeleo ya nchi yetu. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa wanachuo 530 katika kiwango cha Stashahada ya Juu katika fani za Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Maendeleo na Upangaji na Uendeshaji Shirikishi wa Miradi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya Maendeleo ya Jamii ngazi ya cheti kwenye vyuo vya Buhare, Missungwi na Rungemba. Katika mwaka 2004/2005, jumla ya wanachuo 420 watapatiwa mafunzo katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa mafunzo hayo kwa ufanisi, Wizara yangu itaimarisha uendeshaji katika vyuo vya Tengeru, Buhare, Missungwi na Rungemba. Wizara itaaniszha Bodi za Uendeshaji wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Buhare, Misungwi na Rungemba. Aidha, Wizara itaaniszha mchakato wa Chuo cha Tengeru kutungiwa Sheria yake ambayo itakiwezesha kuwa na Bodi na kukipa uwezo wa kujiendesha chenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa elimu ndio msingi wa maendeleo ya jamii yoyote ile, Wizara yangu inatarajia kutoa kozi za stadi mbalimbali kwa Wananchi wapatao 18,100 kwenye vyuo vyake 58 vya Maendeleo ya Wananchi. Kozi hizo zitakuwa za muda mrefu na za muda mfupi. Vile vile, vyuo hivyo vinatarajia kutoa mafunzo nje ya vyuo (*outreach training*) kwa Wananchi 3,500. Mafunzo hayo yatawapatia Wananchi maarifa na stadi mbalimbali zitakazowawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi, kujijiri na kujitegemea na hivyo kuongeza kasi ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, ubora wa miundombinu na mazingira ya vyuo yana mchango mkubwa katika utoaji wa mafunzo. Kwa kuzingatia hayo Wizara yangu inatarajia kuvifanyia ukarabati mkubwa Vyuo sita vya Maendeleo ya Wananchi kwa wastani wa chuo kimoja katika kila Kanda. Uchambuzi wa kuvipata vyuo hivyo unafanywa kwa kushirikiana na Mikoa. Aidha, Wizara itawezesha upimaji wa maeneo ya baadhi ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili vipatiwe hati miliki. Zoezi hilo litapunguza matatizo ya uvamizi wa maeneo katika vyuo na hivyo kuondoa migogoro ya ardhi inayovikumba.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mazingira katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Wizara yangu itaendelea kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu. Aidha, Wizara itanunua kwa awamu, mitambo ya maabara kwa ajili ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi ili kukiwezesha kutoa mafunzo ya Cheti cha Ufundı Sanifu (*Full Technician Certificate*). Hali kadhalika, Wizara itawezesha upimaji wa maeneo ya vyuo hivyo ili viweze kupatiwa hati miliki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kujitegemea katika jitihada zetu za maendeleo, Wizara yangu inathamini sana mchango wa Vikosi vya Ujenzi na Mafunzo ya Ufundı viliwyoko kwenye Halmashauri. Vikosi hivi kwa kushirikiana na Wananchi vimekuwa vikifanya kazi nzuri katika ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, zahanati na miradi mingine ya kijamii. Kwa kuwa katika siku za usoni miradi mingi ya kijamii itatekelezwa na Wananchi wenyewe, kama inavyojidhihirisha katika miradi inayogharimiwa na *TASAF*, vikosi hivi vitakuwa na umuhimu zaidi. Kwa kuzingatia hayo, Wizara itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa mafundi 60 kutoka Wilaya 20 ili kupanua uelewa wao katika masuala ya ufundı na hasa matumizi ya mbini shirikishi katika kutekeleza miradi ya kujitegemea. Ni matarajio yangu kuwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri watavitumia vikosi hivyo katika miradi ya kujitegemea inayotekeliza kwa nguvu za Wananchi na kuwapa Wananchi hao ujuzi wa kiufundi watakaotumia katika kuifanya miradi yao kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mazoea kuwa punde mhisani anapoondoka ndiyo unakuwa mwisho wa mradi au programu aliyokuwa akiifadhili. Mazoea hayo ni potofu na yanawakatisha tamaa wafadhili. Kuna suala la uendelevu (*sustainability*) ambalo linapaswa kuzingatiwa ili rasilimali zilizowekezwa kwenye miradi na programu za namna hii ziweze kuwa na maana kwa Taifa.

Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005 itaendelea kufuatilia utekelezaji na uendeshaji wa miradi ya *HESAWA* katika Kanda ya Ziwa. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo itaeneza dhana ya *HESAWA* (Afya, Maji na Usafi wa Mazingira) kwa Wananchi na Watendaji wa Wilaya zote nne za Mkoa wa Singida. Katika kueneza dhana hii msisitizo utawekwa kwenye ushirikishwaji wa Wananchi katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kutathmini miradi yao ya maji na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisheseleza hapo awali, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itachapisha Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Jinsia na kuusambaza kwa wadau ili kuwa na mtizamo wa pamoja katika utekelezaji wa masuala ya jinsia. Vile vile, itachapisha na kusambaza Mwongozo wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuimarisha uelewa wa masuala ya jinsia kwa Watendaji wa Dawati la Jinsia mmoja kutoka kila Halmashauri na katika Asasi mbalimbali kwa kuwapatia mafunzo. Mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yatawawezesha kuingiza masuala ya jinsia katika mipango, sera, mikakati na programu za maendeleo ya Sekta husika. Pia, yatawawezesha kufanya uchambuzi wa takwimu na

taarifa za kijinsia katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa na hivyo kuondoa tofauti za maendeleo zilizopo kati ya wanawake na wanaume. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa pia tunatekeleza utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika taarifa ya mapitio ya utekelezaji, Wizara yangu itaendelea kufuatilia upatikanaji wa maamuzi kuhusu uanzishwaji wa Chombo kitakachowaunganisha wanawake bila kujali itikadi za kisiasa na tofauti nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaandaa taarifa ya nne na tano ya utekelezaji wa Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake na kuwasilisha taarifa hiyo Umoja wa Mataifa.

Aidha, Wizara yangu itaendelea kushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa inayohusu maendeleo ya wanawake na jinsia.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ya Ulingo wa Beijing ambayo ni kuwapa uwezo wanawake katika sheria, kuwaimarisha wanawake katika siasa na ngazi za maamuzi, kuwaimarisha wanawake kiuchumi na kuondoa umaskini na kupata elimu, mafunzo na ajira. Wizara yangu itaandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Ulingo wa Beijing baada ya miaka kumi. Taarifa hii itabainisha mafanikio, matatizo ya utekelezaji na mapendekezo ya jinsi ya kuboresha utekelezaji wake. Taarifa hiyo itachapishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara yangu itaendelea kuratibu mchakato wa uanzishaji wa Benki za Wanawake. Benki hizo zitatoa huduma mbalimbali kwa wanawake ili kujimarisha kiuchumi na kukuza vipato vyao na hivyo kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu ilifanya ufuatiliaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Ufuatiliaji huo ulionyesha kuna matatizo ya kiutendaji ambayo Wizara yangu itayatafutia ufumbuzi. Matatizo hayo ni pamoja na fedha za Mfuko kutotumika kwa matumizi yaliyokusudiwa, fedha kukopeshwa kwa watu wasio walengwa, kutorejeshwa mikopo kwa wakati uliopangwa na usimamizi na ufuatiliaji hafifu wa Halmashauri. Wizara itaendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, kubuni njia za kuuimarisha ili uweze kuwanufaisha wanawake wengi zaidi. Vile vile, Wizara itaendelea kuhimiza marejesho kupitia Halmashauri, Manispaa na Miji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani tarehe 8 Machi kila mwaka ili kufuatilia maendeleo ya wanawake katika shughuli mbalimbali. Siku hii pia itatumika kuadhimisha miaka 10 ya Utekelezaji wa Ulingo wa Beijing Kitaifa kwa lengo la kutathmini mafanikio, matatizo na kupendekeza namna ya kukabiliana nayo. Changamoto zilizojitokeza Kitaifa katika kipindi hicho zitabainishwa na kuandaliwa mikakati ya kuboresha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/05, Wizara yangu itafuatilia maamuzi ya Serikali kuhusu Sera ya Maendeleo ya Familia. Aidha, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa mipango inayolenga kuendeleza dhana ya familia kama kitovu cha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara pia itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto iliyodurusiwa. Kuwepo kwa Sera hiyo kutawezesha kujenga mazingira mazuri yanayowafanya watoto kukua na kupata ustawi kulingana na malezi bora ya jamii yetu. Baada ya kudurusu na kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa Sera hiyo, Wizara yangu itaelimisha jamii na wadau wengine juu ya Sera.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2003/2004 nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Tanzania inazo mila na desturi ambazo baadhi ni nzuri na baadhi zina madhara kwa wanawake na watoto.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, pamoja na juhudi za Serikali kuendelea kuenzi mila zinazofaa na kupiga vita zile zenye madhara, bado ziko mila na desturi zinazoleta madhara kwa jamii na bado zinaendelezwa. Hizi ni pamoja na ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike, ndoa katika umri mdogo na upendeleo wa watoto wa jinsi moja. Mila na desturi zenye kuleta madhara hazina budi kuondolewa. Hivyo, Wizara yangu kwa kutumia Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo katika ngazi mbalimbali na wadau wengine itaendelea kuwaelimisha Wananchi juu ya mila na desturi hizo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa Mwenyekiti wa Mtando wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Kutokomeza Ukeketaji wa Wanawake na Watoto wa Kike kuanzia mwaka 2002 hadi 2003. Nchi wanachama wa Mtando huo ni Djibouti, Eritrea, Kenya, Uganda na Tanzania. Kama Mwenyekiti, tuliratibu juhudi za nchi wanachama za kutokomeza ukeketaji.

Aidha, baadhi ya wakeketaji wanaendelea kusalimisha zana zao na kutangaza kuachana na mila hiyo yenye madhara. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kuratibu jitihada zinazofanywa na Asasi mbalimbali katika kulikabili tatizo hilo. Nachukua nafasi hii kuzipongeza Asasi zisizo za Kiserikali kwa jitihada wanazozifanya za kutokomeza ukeketaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kuelimisha jamii ili kuongeza uelewa wao kuhusu Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia. Mkazo utawekwa katika kuelimisha jamii kuhusu mila na desturi zenye kuleta madhara, elimu ya afya ya uzazi, matatizo ya familia na jinsi ya kuyatatua, umaskini wa familia na namna ya kuuondoa. Kwa kufanya hivyo tutaweza kubadilisha fikra zao na kuwaendeleza. Ili tuweze kufikia lengo letu katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara itaandaa makala ya programu ya Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia na kuisambaza kwa wadau husika. Vile vile, Wizara itatayarisha Kitini cha elimu hiyo ili kiweze kutumika katika mafunzo yatakayoandalisha.

Mheshimiwa Spika, makuzi na maendeleo ya utotoni ni mwanzo muhimu wa maendeleo ya mwanadamu. Ili kuhakikisha kuwa watoto wanapatiwa mwanzo mzuri wa uhai, ulinzi, makuzi na ustawi wao, Wizara yangu katika mwaka 2004/2005 itaendelea kusaidia na kuimarisha Mtandao wa Tanzania wa Maendeleo ya Awali ya Utotoni (*Tanzania Early Childhood Development Network*). Mtandao huo unadhamiria kujenga mazingira bora yatakayoimarisha uwezo wa jamii ili waweze kushiriki katika kuwathamini, kuwatimizia mahitaji muhimu na kuleta maendeleo ya watoto wachanga na wenyе umri mdogo. Wizara yangu ikiwa ni Mwenyekiti wa Mtandao huo, itasimamia na kuratibu shughuli zake.

Katika mwaka 2004/2005, Mtandao huo utasaidia baadhi ya watoto wadogo walioko kwenye mazingira magumu kulipia karo na chakula wakiwa katika shule za awali. Mtandao utaelimisha na kuwasaidia walezi wa familia zisizojiweza na pia kwa kutumia Vyombo vya Habari, utaelimisha jamii kuhusu malezi bora ya watoto na UKIMWI. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, wapo watoto wengi wenyе vipaji maalum kama vile kuchora, kucheza michezo mbalimbali, masomo ya sayansi na hesabu, kuigiza na sanaa. Hata hivyo, vipaji hivi bado havijaweza kutambuliwa katika hatua za mwanzo na kuweza kuthaminiwa na kuendelezwa. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Wizara yangu itaandaa programu na mikakati itakayowezesha kuwatambua na kuendeleza vipaji vya watoto.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa makubaliano yaliyomo katika Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Mtoto. Kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, nchi zinazoridhia mkataba zinawajibika kutoa taarifa ya awali ya utekelezaji wa mkataba huo kwenye Umoja wa Afrika katika kipindi cha miaka miwili baada ya kuuridhia. Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2004/2005 itaandaa ripoti hiyo na kuiwasilisha Umoja wa Afrika.

Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), itaratibu programu maalum ya kukomesha utumikishwaji wa watoto katika ajira mbaya. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara yangu itatekeleza programu hiyo kwa kuingiza masuala ya haki za watoto, hususan kukomesha utumikishwaji wa watoto, katika mitaala ya mafunzo yanayotolewa na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Hatua hii itasaidia kuwalinda watoto dhidi ya kazi hatari ambazo zinaathiri maendeleo na ustawi wao.

Aidha, hatua hii itawawezesha watumishi wa fani ya Maendeleo ya Jamii kuelimishwa mikataba mbalimbali ya haki na ustawi wa mtoto na hatimaye kuwaelimisha Wananchi, kwa lengo la kuitekeleza mikataba hiyo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI itaendelea kuhamasisha familia kuzalisha na kuhifadhi chakula cha kutosha ili kujihakikishia usalama wa chakula katika ngazi ya familia. Suala hili pia lilisisitizwa na Mheshimiwa

Rais Benjamin William Mkapa, alipokuwa anafungua Mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) tarehe 15 Mei, 2004 kuhusu upatikanaji na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu utekelezaji bora wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo ya jamii unategemea kwa kiasi kikubwa matumizi sahihi ya rasilimali katika kuleta makusudio yaliyotakiwa. Ili hili lifanikiwe, ni lazima kuwepo mfumo wa utaratibu wa ukusanyaji takwimu sahihi na za kuaminika ili kusaidia ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali hizo. Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005 itafuatilia na kufanya tathmini ya miradi na programu mbalimbali za Wizara ili kupima manufaa yake kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kitengo cha Kompyuta cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitakamilisha maandalizi ya uwekaji kwenye Kompyuta mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaozingatia jinsia (*Computerized Gender Sensitive Monitoring and Evaluation System*). Maandalizi yameshakamilika na mwaka wa 2004/2005 Wizara itakusanya takwimu kutoka kwenye Wizara, Idara za Serikali, Halmashauri, Miji, Manispaa na Jiji. Wakusanyaji wa takwimu hizi watakuwa Watendaji wa Dawati la Jinsia amba watapewa mafunzo kabla ya utekelezaji. Takwimu hizi zitaiwezesha Wizara kufuatilia na kutathmini vipaumbele vya Serikali vya Ulingo wa Utekelezaji wa Maazimio ya Beijing na utekelezaji wa Mkakati wa Kuondoa Umaskini. Ni matumaini yangu kuwa, wote wanaohusika wataiwezesha Wizara kupata takwimu hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nawasilisha mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2003/2004, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu ilianda mpango wa miaka mitatu wa Wizara (*Master Plan*) amba hauktekelezwa ili kutoa nafasi kwa wadau, wakiwemo wahisani kuupitia. Kwa mwaka 2004/2005, Wizara itaukamilisha mpango huo na kutekeleza mpango wa mwaka mmoja (*Interim Plan*). Hii ni pamoja na kukamilisha utayarishaji wa mfumo wa wahisani wa kuchangia Mfuko wa pamoja (*Basket Funding*). Wahisani watakaoisaidia Wizara ni Uhlanzi, Ireland, Denmark, Canada, *UNICEF*, *UNFPA* na *UNDP*.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI unafahamika kuwa ni tatizo ambalo linaathiri maendeleo ya nchi kwa kuwa linagusa nguvu kazi. Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005, itaendelea kuelimisha wafanyakazi wa Wizara na Vyuo vyake namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Pia, Wizara itaendesha mafunzo ya uelewa kwa watumishi wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii ili waweze kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa huu. Aidha, Wizara itatumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika kuelimisha jamii inayovizunguka.

Mheshimiwa Spika, upandishwaji wa vyeo kwa watumishi wa kada mbalimbali kwa wakati unaostahili ni njia mojawapo ya kuongeza motisha na uwajibikaji kwa watumishi na hivyo kuleta ufanisi. Wizara yangu itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi wa kada mbalimbali kulingana na utendaji wao wa kazi, sambamba na vigezo

vya mpango maalum wa Serikali wa kuimarisha huduma zake (*Performance Management System*).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mpango wa Serikali wa kuziba mianya ya rushwa kwa kuwaelimisha watumishi maadili ya utumishi wa umma ili kuwaongezea wadau na walengwa wetu imani juu yetu. Elimu hii itatolewa kwa Watumishi wa Makao Makuu ya Wizara pamoja na wa Vyuo.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Wizara ni njia mojawapo ambayo Viongozi na Maafisa waandamizi kutoka Makao Makuu ya Wizara wanaweza kukutana na watendaji na wadau mbalimbali. Mkutano huo hutumika kutathmini kazi za Wizara kwa pamoja kwa nia ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake na ya Kisekta. Hivyo katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itafanya Mkutano wake Mkuu wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kufanya mikutano ya mashirikiano baina yake na Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Zanzibar. Kuendelea kufanyika kwa mikutano hii kutazijengea Wizara zetu moyo wa kushirikiana katika utayarishaji wa programu mbalimbali za maendeleo kama vile *Gender Advancement* na pia kuimarika kwa mawasiliano kati yetu. Mashirikiano pia yataweza kunyambulishwa katika maeneo ya maadhisho mbalimbali, Uandishi wa Ripoti za Kimataifa na kuhudhuria Mikutano ya Kimataifa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, itaendelea kufanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi kila mwaka kwa mujibu wa Agizo la Rais Na. 1, 1970. Vikao hivyo ni muhimu kwani vinasaidia kuimarisha ushirikiano na uhusiano kati ya Viongozi wa Wizara na chombo cha wafanyakazi (TUGHE) kwa nia ya kuimarisha ushirikiano na pia utendaji kazi ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Jamii kwa: -

- Kununua vifaa mbalimbali kama vile *LCD Projector, TV Screen* na *Photographic sets*.

- Kuongeza wataalam wanne zaidi na kuwapatia mafunzo. Wizara yangu kwa kupitia Kitengo hicho itaelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji wa kazi, Wizara yangu itaajiri watumishi wapya 82 kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kama ifuatavyo:-

Afisa Habari Mkuu mmoja, Maafisa Maendeleo ya Jamii wanne, Maafisa Elimu watano, Maafisa Elimu Wasaidizi 10, Matabibu wawili, Wauguzi wawili, Makatibu Mahsus 10, Wakutubi watatu, Mafundi Sanifu 10, Madreva watano, Wasaidizi wa Ofisi watano, Wapishi 10 na Walinzi watano.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Malengo ya Wizara kwa mwaka 2004/2005 yanaonyesha ni kiasi gani Wizara yangu ilivyo mtambuka na hivyo kuhitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali katika kuimarisha na kuleta ufanisi katika utendaji wa Wizara hii. Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika maendeleo yao binafsi na Taifa letu kwa ujumla. Lengo letu sote, ikiwa ni pamoja na Wizara yangu, ni kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kijitabu cha majedwali kimegawiwa pamoja na hotuba hii. Majedwali hayo yanatoa ufanuzi zaidi wa masuala mbali mbali yaliyoelezwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Parkar Khan, kwa ushirikiano, ushauri na usaidizi mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Vile vile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Bibi Hilda Ausi Gondwe, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote na waliopo kwenye Taasisi zetu zote, kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Bila ya mchango wao muhimu ingekuwa vigumu kupiga hatua katika majukumu tuliyonayo ya kuendeleza Sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu, sina budi kuwashukuru wale wote tunaofanya nao kazi au wengine ambao kwa namna moja au nyingine tunashirikiana. Peke yetu kama Wizara tusingeweza kufikia mafanikio niliyoyataja.

Napenda kutumia nafasi hii na kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa shukrani zangu za dhati, kwa wafuatao: Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), Shirika la Mtandao wa Jinsia Tanzania (*TGNP*), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*TAWLA*), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (*TAMWA*), Shirikisho la Vyama vyta Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (*FAWETA*), *Plan International* na Mashirika mbalimbali pamoja na wale ambao wanafanya kazi kwa maslahi yetu kwa namna moja au nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzishukuru Serikali za nchi rafiki ambazo kwa kupitia Mashirika yake ziliendelea kutusaidia. Nchi hizo ni Ireland, Italia, Netherlands na Sweden. Mashirika ya Kimataifa ambayo ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (*UNICEF*), *UNDP*, *UNFPA*, Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake (*UNIFEM*) pamoja na Mashirika mengine ya ndani na nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2004/2005, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Matumizi ya shilingi 4,989,293,400/=. Kati ya hizo, shilingi 4,121,300,200/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Sh.1,825,310,500/= ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi

2,295,989,700/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*Other Charges*). Aidha, shilingi 867,993,200/= ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi 600,000,000/= ni fedha za hapa nchini na shilingi 267,993,200/= ni fedha za nje.

Mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. JINA KHATIB HAJI (k.n.y. MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2003/2004 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2004/2005 ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutekeleza Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati yetu kwa niaba yake.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa salaam zangu za rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge wafuatao kwa kufiwa na wapendwa wao Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi, Mheshimiwa Parmukh Sigh Hoogan na Mheshimiwa Dr. Laurence Gama, kwa kufiwa na watoto wao.

Aidha, naomba kutoa pole za dhati kabisa kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yetet Sintemule Mwalyego, aliyeferiki ghafla akiwa anahudhuria Mkutano wa Bunge hapa Dodoma akiwakilisha Jimbo la Mbeya Vijijini tarehe 24 Juni, 2004. Kifo chake ni msiba mkubwa kwa Bunge letu Tukufu na kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Mungu aziweke roho za Marehemu hawa mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki kwa tiketi ya CCM. (*Makofi*)

Napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa maelezo yake ya kina

aliyotoa mbele ya Kamati wakati akiwasilisha mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2004/2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wajumbe wa Kamati, kwa mujibu wa Kanuni Na.102 (1) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004, Kamati ya Maendeleo ya Jamii ina Wajumbe 18 wafuatao:-

Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Omar Mohamed Mwenda, Mheshimiwa Janeth Mashele, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Ramadhan Nyoje Pandu, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Bakari Mbonde na Mheshimiwa Kisyeri Chambiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupitia na kupata maelezo ya Waziri kuhusu utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Kamati kwa kiasi kikubwa imeridhika na utekelezaji uliofanywa na Wizara. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya Halmashauri ambazo bado hazijachangia kikamilifu asilimia 10 ya mapato yake kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uanzishwaji wa chombo cha wanawake na Benki ya Wanawake, Kamati imeona kuwa mchakato wa uanzishwaji wa vyombo hivi unaenda taratibu sana na hivyo kuchukua muda mrefu wa maandalizi. Kamati pia imeona kuwa bado kuna upungufu mkubwa wa bajeti kwa Wizara hii. Aidha, Kamati imebaini kuwa kuna uhaba wa Wataalam na Watumishi hasa Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2004/2005, katika Bajeti ya mwaka 2004/2005, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imetengewa kutumia kiasi cha shilingi 4,989,203,400/= kwa mwaka. Kiasi hiki cha fedha ni kidogo sana ukilinganisha na majukumu iliyopangiwa Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati baada ya kupata maelezo ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo kwa Wanawake na Vijana:-

(1) Kamati haijaridhika na urejeshaji wa mikopo inayotolewa kwa wanawake na Halmashauri. Hivyo inashauri Wizara ibuni njia bora itakayowawezesha wakopaji kurejesha mikopo kwa wakati ili kuwawezesha wanawake wengine kukopa.

(2) Kamati inashauri Serikali kuwatumia Maafisa Maendeleo ya Jamii Wilaya, kufanya kazi ya kufuatalia kwa karibu urejeshaji wa mikopo hiyo.

(3) Kamati inapongeza Wizara kwa uamuzi wake wa kutuma mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake wenye kuzitaka Halmashauri zitumie riba ya asilimia 10 ya mikopo inayotolewa na Halmashauri kubaki kwenye Halmashauri hizo ili itumike kwa ajili ya mafunzo na ufuataliaji. Hata hivyo, Kamati inashauri Wizara kuchukua hatua za makusudi dhidi ya Halmashauri ambazo bado hazitaki kutoa 10% kwa ajili ya mikopo ya wanawake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Chombo cha Wanawake na Benki ya Wanawake, Kamati inapongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya juu ya uanzishwaji wa chombo cha wanawake pamoja na Benki ya Wanawake. Hata hivyo Kamati inashauri kuwa ni vyema Wizara ikajiwekea muda maalum wa kuhakikisha kuwa vyombo hivi vinaanzishwa kwani ni muda mrefu sasa tangu mchakato wa uanzishwe kwa Benki ya Wanawake na Chombo cha Wanawake ulipoanza.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza fani mbili katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kukiboresha Chuo hiki na vingine kama hivi, ili viweze kwenda na wakati, hasa katika kuvipatia vifaa muhimu kama *Computer*, huduma za *Internet* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Kamati inapongeza Uongozi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ifakara, kwa juhudi zao katika kujitegemea na kukiweka Chuo katika hali nzuri. Hata hivyo Kamati inashauri Wizara kuvihamasisha Vyuo vingine ambavyo havifanyi vizuri kuiga kutoka Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ifakara. (*Makof*)

Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa na Wizara kwenda katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, zitumike kama zilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara, hii ni mengi sana ukilinganisha na bajeti inayopangiwa. Kamati inaomba Serikali kuona uwezekano na umuhimu wa kuongeza bajeti kwa Wizara hii, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2004/2005. Baada ya maelezo hayo, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, inayakubali mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida, shilingi 4,121,300,200/=, Miradi ya Maendeleo shilingi 867,993,200/= .

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Pia napenda nimshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, vile vile naomba kumshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu, Ndugu Hilda Gondwe na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao katika kuandaa taarifa ya Bajeti na hasa kutoa maelezo ya kina mbele ya Kamati yangu wakati wa kuwasilisha bajeti ya Wizara yao. (*Makofii*)

Kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa michango yao katika kujadili na kuchambua maoni ya Bajeti ya Wizara.

Mwisho, naomba nimshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa, pamoja na Katibu wetu wa Kamati, Bibi Angelina Sanga, kwa huduma na ushauri mbalimbali katika kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi zake kwa ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Nawashukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Baada ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, wachangiaji wanne wa mwanzo ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Margareth Mkanga na Mheshimiwa Rhoda Kahatano. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu. (*Makofii*)

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c) Toleo la mwaka 2004.

Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa pole kwa familia ya Marehemu Yetet Mwalyego, wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, bila kuwasahau ndugu zetu wa Chama cha Mapinduzi kwa msiba mkubwa wa kuondokewa na ndugu yetu Yetet Mwalyego. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze pema roho yake. *Amin.* Aidha, tunawapa pole wale wote waliopatwa na masahibu ya aina yoyote kwa ujumla wao. Poleni sana!

Mheshimiwa Spika, kwa kipimo chochote kile, bado Tanzania ni Taifa maskini sana. Huduma za kijamii bado ziko nyuma sana na huenda itachukua muda mrefu sana maendeleo ya kijamii kuimarika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufutiwa madeni ya nje yanayofikia dola za kimarekani 749.7 milioni chini ya utaratibu wa *HIPC*, kufikia mwezi Desemba, 2003,

bado umaskini uliokithiri unaendelea kujichimbia. Idadi ya watu wanaopata maji safi na salama vijijini na mijini inakadiriwa kufikia asilimia 53.5 mwaka 2003. Ukusanyaji wa mapato ya ndani unaofikia shilingi bilioni 108 kwa mwezi bado haujafanikiwa kuboresha maisha ya Mtanzania hohehae. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2003 watu wasio na kazi nchi nzima wanakadiriwa kuwa asilimia 12.9. Watu wasio na kazi Jijini Dar es Salaam ni asilimia 46.5, miji mingine asilimia 25.5 na vijijini asilimia 8.4. Idadi ya wanafunzi waliojiunga na sekondari mwaka 2003, ni asilimia 38.7 tu, na hiki ni kiwango cha chini mno ikilinganishwa na mataifa mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa wataalam. Wataalam wa Maendeleo ya Jamii vijijini bado idadi yao ni pungufu sana. Mabwana Maendeleo na Mabibi Maendeleo ya Jamii wanayo nafasi nyeti katika kuchochea na kuhimiza maendeleo, hasa vijijini. Wataalam hawa wanalo jukumu la kuitabiri na kuichanganua vema Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jamii, Sera ya Maendeleo ya Wanawake, Sera ya Maji, Mazingira, Ukimwi na Umasikini na kadhalika. Maafisa wa Maendeleo ya Jamii hawafanyi kazi zao ipasavyo kutokana na vijimishahara vidogo na mazingira ya kazi yasiyovutia, kwani ni wachache, hawana usafiri ili kuifikia jamii. Ingekuwa jambo la busara kwa Serikali kuongeza idadi ya Mabwana na Mabibi Maendeleo angalau mmoja au wawili kwa kila kata ili waweze kufikia jamii.

Katika vijiji vingi vya Tanzania, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii hawafahamiki kabisa. Jambo hili ni tatizo na linawanyima wananchi nafasi ya kujiletea maendeleo kwa kukosa uungwaji mkono wa kiutaalamu kutoka kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii. Vivutio zaidi viwekwe na Serikali kwa lengo la kuifanya kazi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii ipendwe na iheshimike zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) Vyuo vingi vya Maendeleo ya Wananchi havina hati za kisheria za kumiliki maeneo ambayo viro na vimekaa kienyeji au kisiasa tu. Jambo hili ni la hatari na linazuia uendelezaji wa vyuo hivyo kwa matazamio ya muda mrefu. Wakopeshaji wote, kama Mabenki na kadhalika., daima huulizia na kufuatilia kuwepo umiliki wa kisheria wa mali zote zilizopo katika Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hulazimika, kufanya mitihani ya *VETA*, jambo ambalo limekuwa likiongeza usumbufu na hata gharama kwa wanafunzi hao. Mtando mkubwa wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ungeliweza kutumika kupanua Elimu ya Sekondari nchini mwetu. Kwa sababu lengo la Elimu ya Sekondari kwa wote wanaomaliza Elimu ya Msingi lipo, ila tatizo ni rasilimali, ikiwa ni pamoja na majengo, si vibaya kuwazia kuvibadilisha angalau baadhi ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuwa Shule za Sekondari na hasa katika maeneo ya vijijini, au kuviongezea hadhi na kutambulika kama *VETA* yaani vyeti vyake vitambulike, kusiwe na sababu ya kufanya mitihani ya *VETA*.

Hata hivyo, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilikuwepo kabla ya Vyuo vya *VETA* na viko vijijini. Nashauri vyuo hivi viwe na hadhi sawa na *VETA* au hadhi yake inayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa wanawake. Bado zipo Halmashauri ambazo hazitaki kutoa ile asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya Maendeleo ya Wanawake kupitia mikopo, visingizio vinavyotolewa ni vingi, lakini kuna kila sababu za kuchukuliwa kwa hatua za kinidhamu dhidi ya Watendaji Wakuu wa Halmashauri hizo. Uzembe huo na labda kiburi cha Halmashauri hizo ni hujuma tosha dhidi ya Maendeleo ya Wanawake. Waziri mhusika pia anao wajibu wa kuwaeleza wananchi kikamilifu ni kwa nini ameendelea kuwadekeza Watendaji Wakuu wa Halmashauri hizo zinazokwamisha Ukombozi wa Wanawake na pia Maendeleo ya Jamii kwa ujumla. (*Makofî*)

Pia wanawake wanaopewa mikopo hiyo waelimishwe kwamba sio misaada na hivyo walipe mikopo hiyo kwa wakati, ili wanawake wengine na wenzao wapate yaani ni katika utaratibu wa *revolving fund*. Wanawake ni wote waliozaliwa wanawake, bila kujali itikadi zao, rangi, dini au umaarufu wa aina yoyote ile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ufinyu wa Bajeti ya Wizara, kama sote tunavyoolewa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, inashughulikia maswala ya Jamii na Jinsia, kwani imetamkwa wazi wazi, hivyo, Wizara si ya wanawake tu, ni yetu sisi sote, kwani jamii ni wanawake, wanaume, wakiwemo watoto, wazee, vijana, walemavu, wakulima, wafanyakazi, wagonjwa na kadhalika.

Kwa msingi huo, natoa ushauri na ili kuonyesha mfano thabiti kwa vitendo, Wizara hii iongozwe na jinsia zote, hasa katika ngazi za juu kama Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, ngazi hizi ziwe na wanawake na wanaume, angalau mwanaume mmoja (1/3). (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imekumbatia sehemu muhimu ya Jamii ya Watanzania, kwa msisitizo zaidi wa Wanawake na Watoto. Wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wote na wengi ni wakulima wa jembe la mkono huko vijijini. Wizara hii ndiyo inayoongoza na kuratibu harakati za kuwakomboa wanawake. Ni jambo la kushangaza kuona Wizara hii imetengewa kutumia kiasi cha shilingi 4,989,203,400/= tu kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kupitia utaratibu wake wa Malengo ya Maendeleo ya Mileniamu (*Millennium Development Goals*), Umoja wa Mataifa umepania kuboresha maendeleo ya kijamii katika ulimwengu wa tatu hasa kwa kuhamasisha Ufutwaji wa madeni kupitia utaratibu wa *HIPC*, kuhakikisha Elimu ya Msingi na hata ya Sekondari inapatikana kwa watoto wote, kutoa kipaumbele kwa maendeleo ya kielimu na kijamii ya Mtoto wa Kike, kulinda Afya ya Mama na Mtoto, na kadhalika. Kwa sababu mwelekeo wa dunia ni wa kuvalia njuga maendeleo ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Serikali ya Tanzania ilielewe hilo badala ya kurundika fedha kwenye Vyombo vyta Ulinzi na Usalama kwa kisingizio cha Uchaguzi Mkuu. Uchaguzi Mkuu ni tukio la furaha ambapo inapatikana nafasi ya wananchi kutoa ridhaa yao kuhusu ni nani wanataka awatawale kwa kipindi fulani. Uchaguzi Mkuu ni

rehema na siyo mkamiano wa kivita na hasa kama misingi yote ya uchaguzi huru na wa haki inazingatiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, uwekezaji mdogo katika maendeleo ya kijamii yanayogusa watu wengi wa kawaida, ni chanzo kikubwa cha mkusanyiko wa hasira ambayo ni lazima ipate pakutokea. Tusijitafutie mitafaruku ya kijamii na hata ya kisiasa, kwa kupuza utengaji fedha za kutosha kwa ajili ya maendeleo ya kijamii. Ni lazima keki ya taifa igawiwe kwa uwiano ulio makini. Maslahi ya watu wa kawaida kabisa, ambao ndiyo wengi katika jamii yetu ni muhimu yalindwe. Si busara kuwatoa muhanga watu wanyonge kwa kuiminya bajeti yao. Ni nani asiyejua kwamba, akina mama kupitia majembe yao ya mikono ndiyo wanaozalisha chakula cha taifa hili na ndiyo wanaoleta fedha za kigeni kupitia pamba, chai na tumbaku, pia alizeti na pareto wanayoilima? Ni nani asiyejua kwamba akina mama ndio walezi wa familia na Taifa kwa ujumla na ndio wapiga kura wetu wanaotufikisha hapa tulipo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Wanawake, wazo zima la kuwepo kwa benki maalum kwa ajili ya maendeleo ya wanawake ni jambo la kuungwa mkono na yeote yule anayependa Maendeleo ya Jamii. Benki hiyo itaimarisha sana nguvu za kiuchumi za wanawake na kwa hali hiyo kuchochea sana maendeleo ya kijamii na ukombozi mzima wa mwanamke.

Mheshimiwa Spika, changamoto kwa wanawake wote nchini ni kijiandaa kuiunga mkono Benki hiyo kwa kuisimamia vizuri, kutumia huduma zake kwa kukopa na kurejesha mikopo kwa wakati. Wanawake wataweza kuitumia benki hiyo kwa faida kama watawezesewa kuelewa mapema misingi ya ufanyaji biashara ndogo ndogo, nguzo muhimu za ujasirimali *Entrepreneurship*, ufundi wa kubuni na kutayarisha pia kuchanganua miradi midogo midogo na suala zima la misingi ya uhasibu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imedhihirika unapomwendeleza mwanamke, utakuwa umeendeleza sehemu kubwa ya jamii, ukianzia na familia, Kambi ya Upinzani inashauri, Serikali ishawishi mabenki yawe na idara maalum kwa ajili ya kukopesta wanawake kwa masharti nafuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, pamoja na kwamba hata Chuo hiki hakina hati ya kumiliki ardhi ya eneo kilipojengwa, kama vivilyo vyuo vingine chini ya Wizara hii, bado Wizara haijaweza kufaidi vizuri kutokana na huduma ya Chuo hiki. Chuo hiki ndiyo kisima cha utaalamu na mawazo mapya kwa Wizara hii muhimu.

Chuo hiki kinayo nafasi ya *think tank* na kupitia tafiti mbalimbali za kitaalamu kinayo nafasi kubwa ya kuwa injini na chachu ya mabadiliko kwa Wizara nzima na sekta ya Maendeleo ya Jamii. Wakufunzi wa Chuo hiki waendeshe tafiti za kitaalamu zaidi na zaidi, watoe machapisho zaidi ya kitaalamu na waboreshe ushauri wa kitaalamu (*Consultancy services*). Wizara itoe kazi zake nydingi kwa wataalamu wa Chuo hiki na itumie ushauri wao ipasavyo. Wizara igharamie mafunzo ya juu ya wakufunzi ndani na nje ya Tanzania. Chuo hiki pia kifanye mafunzo ya muda mfupi na ya jioni kwa

wananchi walio jirani ili kujipatia kipato cha ziada na kusambaza elimu hii kwa jamii nzima. Nimeelewa kwamba wameshaanza kwa hiyo, nawapongeza na ninaomba waendeleee. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu vita dhidi ya rushwa, utawala bora na kushamiri kwa rushwa za daraja la juu ni adui mkubwa wa maendeleo ya jamii. Rushwa ni chanzo cha ujenzi wa miundombinu isiyodumu na isiyo na ubora unaolingana na fedha zilizotumika. Barabara za lami zinazochimbika muda mfupi baada ya kufunguliwa, majengo duni ya hospitali na zahanati, madaraja yaliyojengwa ovyo ovyo na huduma nyingine duni (*sub-standard or below standard*) ni dalili kubwa ya kuwepo kwa rushwa Serikalini na kwa kiasi kikubwa kabisa, hukwamisha maendeleo ya jamii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa ni lazima iimarishe ili kuchochea zaidi maendeleo ya kijamii kwa kuokoa fedha za wananchi ambazo zinaelekezwa katika mifuko ya watu wachache sana badala ya maendeleo ya jamii nzima. Utawala bora si wimbo fulani tu, bali ni vitendo vya makusudi vyenye lengo la kuifanya jamii ifaidi kutokana na kodi zinazokusanywa na Serikali, usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za Serikali, utungaji na utekelezaji mzuri wa Sera za Kiserikali, uwazi na uwajibikaji zaidi wa Serikali kwa wananchi wake na utoaji wa huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa wananchi wote. Kazi zote hizi lazima zifanyike kwa kushirikiana na jamii kwa maendeleo yao.

Nashauri Wizara iendelee na mapambano ya vita dhidi ya rushwa kwa faida na maendeleo ya jamii kwani Wizara hii ni daraja (*link*) inayounganisha Serikali na jamii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya wanawake kuitia uongozi wa Kitaifa, imekuwa kawaida kwa Serikali za nchi mbalimbali duniani na hasa katika Bara la Afrika, kukwepa kuwapatia Wanawake nafasi nyeti na nzito za Uongozi wa kitaifa au Kiserikali.

Kama ni Uwaziri basi wanawake huwekwa mbali na Wizara nzito na nyeti, kwa mfano, si rahisi kusikia Wizara kama Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi, Mambo ya Ndani, Fedha, Elimu na Utamaduni, pia Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, zinaongozwa na Mawaziri wanawake katika nchi nyingi za Afrika, ikiwa ni pamoja na Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na utaratibu uliopo hivi sasa, naomba kuwafagilia wanawake wenzangu toka Chama kinachotuongozza yaani CCM kwani ikikubalika, watanufaika wa kwanza. Lakini, wanawake ni wanawake, hata sisi wa upande wa pili wa shilingi yaani Kambi ya Upinzani, tupate bila kujali itikadi zetu, kwa sababu sisi pia ni wanawake. Nawaomba wanawake wote tuwe na mshikamano thabiti kwa kunyanyuana bila kujali itikadi zetu ndiyo tutajikomboa sisi wenywewe, familia zetu, jamii na Taifa nzima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba wanawake wenye uwezo wa kuongoza Wizara nyeti na taasisi nyingine nyeti hawapo. Wapo wengi tu, tatizo ni kujichimbia kwa mfumo dume ambao kwa hakika ni mfumo kandamizi na wa kibabe.

Kwa mfano, ni kwa nini zaidi ya miaka 40 baada ya Uhuru, Tanzania haijawahi kuwa na mwanamke wa kuweza kuwa Jaji Mkuu, Gavana wa Benki Kuu, Katibu Kiongozi (*Chief Secretary*), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkuu wa Chuo Kikuu (*Chancellor*), Spika wa Bunge, Mkuu wa Usalama wa Taifa au Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kasoro kubwa katika uendeshaji wa nchi. Ni kwa nini nafasi nzito nzito na kubwa zinashikwa na wanaume tu, hasa ukizingatia wakati huu wa sasa ambapo wapo wanawake wengi wenye uwezo toshelevu wa kiuongozi, kielimu, kiutaalamu, kiujuzi na kadhalika? Ni kwa nini Serikali nyingi za Kiafrika zipo tayari kutoa nafasi nyeti za uongozi wa juu kwa wanaume wenye sifa za kawaida sana, za wastani, au hata za kiubangaizaji kama si kiubabaishaji, kuliko kutoa nafasi hizo kwa wanawake waliobobea na kutopea kitaaluma na kiuwezo? (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, haki kubwa ya maendeleo ya mtoto ni kupata elimu bora na katika mazingira yaliyo bora. Ili kuhakikisha Watoto wa Tanzania wanaifaidi haki hii muhimu, Kambi ya Upinzani inashauri Elimu ya Sekondari tangu kidato cha kwanza hadi kidato cha sita itolewe bure kabisa kwa wote. (*Makofî*)

Mipango bora ya kiuchumi na kielimu inaweza kabisa kulifanya jambo hilo liwezekane kwa muda mfupi kabisa. Huu utaratibu wa kimafungu mafungu na kiawamu awamu unachelewesha sana Maendeleo ya Taifa. Kama askari wetu wanawenza wakanywa bia kwa bei nafuu kutokana na ruzuku ya Serikali kupitia migongo ya walipa kodi, watoto wetu vile vile wanawenza kuhakikishiwa elimu bora na ya bure ya sekondari kupitia aina ya ruzuku ya Serikali na migongo yetu walipa kodi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kufaidi matunda ya Uhuru ni pamoja na kutengeneza kimakusudi mazingira wezeshi ya kuelimisha watoto wetu katika ngazi ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo unaosema kwamba, mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe. Mimi naamini mtaji wa maskini ni maarifa na taarifa alizonazo kichwani kwake mtu mwenyewe kupitia elimu aliyoipata na anayoendelea kuipata. Hivyo basi, elimu ni silaha madhubuti ya kufutilia mbali umaskini. Elimu bora na kuwa na watu wengi walioelimika na kutaalamika ni dalili kubwa kabisa ya maendeleo ya jamii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, si busara kuwajengea au kuwarithisha watoto nyumba, magari na kadhalika. Ni busara kubwa kuwekeza katika Elimu. Mtoto akipata elimu bora, elimu hiyo anaweza kuitumia kujipatia uwezo wa kujenga majumba, kununua magari, mashine mbali mbali, mashamba makubwa, hisa katika Makampuni na hata kujiajiri mwenyewe na kadhalika. Ni kweli kabisa kwamba elimu ni mwanga na ni mtaji nambari moja wa kupalilia au kuleta maendeleo endelevu ya jamii nzima.

Mheshimiwa Spika, kuna mkanganyiko ambao huwezi kuamini, lakini ndio hali halisi, kwamba Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Monduli, kuna *rest house* ambayo imo

kwenye eneo la Chuo na hivyo ni mali yao ila haimilikiwi na Chuo kwa sababu ambazo ni za utata sana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inashauri jambo hili lishughulikiwe haraka iwezekanavyo ili mali za Chuo zitumike na Chuo na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna eneo pia hapo hapo Monduli, ambalo lilichukuliwa na KKKT kwa shughuli ya Ujenzi wa Chuo Kikuu, lakini cha kusikitisha eneo hili halina hata mchoro wala hati.

Kambi ya Upinzani inashauri, kwa kuwa eneo hili ni la Chuo na kwa kuwa, kama eneo hili lilitolewa kwa KKKT kujenga Chuo Kikuu na Chuo hakijajengwa wala michoro haipo, basi Chuo kiendelee kuliweka katika mipango yake kwani ni lao na litawasaidia katika kupanua Chuo kielimu na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi hakuna matatizo sana ya kutisha katika Vyuo tulivyotembelea kama Kamati, mimi nikiwakilisha upande wa Upinzani wa Wizara hiyo. Nawapongeza Wakuu wa Vyuo vya Kilosa na hasa Ifakara jinsi wanavyoendesha Vyuo vyao. Tunaomba Vyuo vingine viige mfano huo hasa wa Chuo cha Ifakara. Pia Kambi ya Upinzani, inashauri Kurugenzi ya Maendeleo ya Jamii, itembelee Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kama kazi zake sio kungojea safari za Kamati. Ndio maana nawaombea fedha zaidi Wizara hii ili kila mtu aweze kutimiza wajibu wake ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iboreshe zaidi maisha ya watu maskini na katika hali ya kudumu. Suala lisiwe kutambia ongezeko la makusanyo ya kodi tu ya kila mwezi, ila liwe kuimarisha vipato vya Wananchi. Umaskini wa kipato ambao ndio unaoifanya mifuko ya Watanzania iwe tupu kwa maana ya *low purchasing power* ni lazima ufutiliwe mbali kwa kuwawezesha wananchi kuwa na namna nyingi za kuimarisha uzalishaji wa bidhaa na huduma. Suala lisiwe kuchomekeza neema chache chache hapa na pale kama chambo katika ndoano ya kuzinasa kura za Wananchi katika Uchaguzi Mkuu ujao. Hoja isiwe kuwaziba macho wananchi kwa kuanza kurusha fedha katika maeneo fulani fulani ya huduma za kijamii kwa kuyachagua kiufundi ili kujitafutia kura. Maendeleo ya jumla na endelevu kwa Watanzania wote ndiyo liwe lengo na siyo mikogo ya muda mfupi mfupi kwa malengo maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kuweza kunipa nafasi ya mwanzo asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake kwa hotuba nzuri yenyе kutoa dira na mwelekeo wa kumkomboa mwanamke na jamii kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumza chochote, ningependa kutoa pole kwa waliofiwa na watoto wao na wazee wao na vile vile ningependa kutoa mkono wa pole na rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yetete Mbalyego, Mbunge wa Mbeya Vijiji. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu pema peponi. *Amin.*

Vile vile ningependa kutoa pole kwa Mama Anne Kilango, ambaye alijeruhiwa kidogo na majambazi. Vile vile namwomba Mwenyezi Mungu ampe moyo wa subira. Hii ni mitihani ya Mwenyezi Mungu inamfika kila mtu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu mikopo kwa wanawake kupitia Halmashauri. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutoa dhana hii nzuri ya kuwawezesha wanawake waweze kupata mikopo katika Wilaya zao. Lakini ningependa kuzungumzia kuhusu mikopo hii kidogo katika sehemu ya Halmashauri kwamba kuna utata kidogo na utata wenyewe ni kwamba Halmashauri bado zinazorotesha, haziwezi kufuatilia mikopo hii ili iweze kuzunguka na wanawake wengine nao wapate.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba katika mkopo huu, Halmashauri 74 tu ndizo ambazo zilikubali kuchukua mikopo hii. Halmashauri hizo, baadhi ya Halmashauri ambazo zilirejesha ni Halmashauri 26 ndizo zilizokuwa na moyo wa kurejesha mikopo hii na idadi ya fedha ambazo Halmashauri hizo zimerudisha ni karibu shilingi 50,611,846/= wakati Halmashauri 74 kwa hesabu ya haraka haraka kwa kila Wilaya ni karibu shilingi milioni 296. Kwa hiyo, hapa utaona kwamba bado kuna upungufu wa Halmashauri kusimamia kikamilifu kurudisha fedha hizo. Kwa hiyo, naomba sana Halmashauri bado zisimamie ili fedha hizi ziweze kurudi kwa wanawake wengine ili nao waweze kukopa.

Mheshimiwa Spika, kuna Halmashauri ambazo hazijafanya marejesho katika kipindi cha mwaka 2001/2004. Kuna Halmashauri 25 bado wao ndio hawajarudisha kabisa hata senti moja. Hii inatia aibu kwa kweli! Kwa sababu nia ya mikopo hii ni kuwasaidia wanawake na vijana na vile vile Halmashauri ilichangia asilimia tano, lakini bado Halmashauri zimeona kwamba mikopo hii ni sadaka na Wizara ilikuwa ina dhamira nzuri tu ya kuwasaidia wanawake wetu hawa katika Wilaya zetu ili waweze kupata maendeleo na kujikomboa katika umaskini. Lakini bado fedha hizi baadhi ya Halmashauri hazijazirudisha. Naomba sana Wizara ishirikiane na Halmashauri ziweze kurejesha mikopo hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningeweza kulizungumzia ni kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake. Dhana na nia ya Wizara ni nzuri sana kwamba sasa umefikia wakati kwamba wanawake nao wawe na chombo chao cha kukopa na kuweka ambayo ni Benki ya Wanawake. Shirika la Utafiti la Masuala ya Uchumi na Jamii (*ESRF*) ilifanya utafiti na kuona kwamba iko haja ya kuanzishwa Benki ya Wanawake. Lakini wametoa ushauri kwamba kwanza kuanzishwe vikundi vya *SACCOS*. Sio dhamira mbaya, ni nzuri lakini lengo letu sisi wanawake ilikuwa ni kufika wakati wa kupata Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba hivi vikundi viro, wanawake wanajishirikisha, wanakopa, wanarudisha na sisi wanawake hatuna historia kwamba tukikopa hatulipi, tuna historia ya kukopa na kulipa, kwa hiyo, nafikiri Wizara bado ishikilie kwamba Benki ya Wanawake iwepo kwa sababu imezungumzwa siku nyingi sana naaisikia tu Benki ya Wanawake itafunguliwa, lakini bado Wizara haijatilia mkazo kwamba Benki ya Wanawake iwepo. Ninaamini Wizara hii itakuwa na lengo hilo la kuwasaidia wanawake ili waweze kukopa.

Lakini ningependa kutoa ushauri kwamba pamoja na kwamba Benki hii haijafunguliwa, itakapofunguliwa basi, kuwe na masharti nafuu ya kumwezesha mwanamke aweze kulipa kwa sababu sasa hivi katika baadhi ya mabenki, kwanza kuna masharti magumu, lazima upeleke hati ya nyumba, hati ya shamba, kwa hiyo, inamfanya mwanamke asite kwenda kukopa kwa sababu wengine hawana nyumba wala mashamba, kwa hiyo, wanashindwa kwenda kukopa. Lakini naamini Benki hii ikifunguliwa, itaweka masharti nafuu ili wanawake waweze kwenda kukopa na kujikwamua katika wimbi hili la umaskini.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kuzungumzia suala la Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Vyuo vya Maendeleo hivi ni vya historia. Mimi toka najiunga na UWT nilikuwa nasikia kuna Mama Maendeleo, kuna Mabwana Maendeleo, kwa hiyo, hivi Vyuo ni vya historia, ni vya siku nyingi na vinawasaidia wanawake katika kujikwamua na mambo mengi sana, vinatoa wataalam wa Maendeleo ya Jamii, vinatoa taaluma na mwamko wa jitihada mbalimbali za maendeleo hususan katika mambo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na hata kimila vile vile. Kwa hiyo, Vyuo hivi inaonekana ni Vyuo ambavyo vinamfanya mwanamke apate mwamko wa kimaendeleo kama nilivyosema, mwamko wa kisiasa na pia katika mwamko wa kimila na kijamii. (*Makofii*)

Kwa hiyo, naamini kwamba Vyuo hivi vitasaidia zaidi ili kumwezesha mwanamke aweze kujua wapi alipo na wapi anakwenda.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia kwa upande mwingine pamoja na kwamba Waziri alisema kwamba baadhi ya Vyuo vimefanyiwa ukarabati, nampongeza sana kwamba baadhi ya Vyuo vilikuwa na hali ngumu sana, vilikuwa katika hali mbaya sana katika miundombinu, katika majengo yenyewe utaona kwamba mandhari ya Vyuo hivi vilikuwa viko katika hali ngumu sana. Lakini nampongeza kwa hilo na vile vile yanataka ukarabati kwa awamu, sio nia mbaya ni nia nzuri. Lakini hata hivyo, juu ya kwamba vinafanyiwa ukarabati kwa awamu, lakini hata hivyo kuna Vyuo ambavyo vyenyewe vinajitahidi kujirekebishia mambo yake katika na kukarabati.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Chuo cha Kilosa, Chuo cha Ifakara, ni Vyuo hivyo ambavyo vinaweza kutolewa mfano kwamba ni vinavyojitegemea wenyewe. Tusingoje fedha kutoka Wizarani tu na wao wenyewe waendelee kwa sababu kama jina lilivyo ni Vyuo vya Maendeleo, klwa hiyo basi wafanye njia tofauti watafute mbinu za kujisaidia wao wenyewe ili waweze kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningeweza kuzungumzia kuhusu chombo cha wanawake. Waziri alizungumza hapa kwamba kuna chombo cha wanawake ambacho kitawaunganisha wanawake wote wa itikadi zote. Nampongeza sana kwa sababu sisi hapa lengo letu ni kumsaidia mwanamke wa Tanzania. Ikiwa mwanamke wa CCM, *CUF*, *UDP* au *TLP*, sisi kama zilivyo sera zetu za Chama cha Mapinduzi ni kumsaidia mwanamke. Kwa hiyo, naamini chombo hicho kitasaidia wanawake wote katika Tanzania hii.

Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri, akiunde hiki chombo ili kisaidie wanawake. Mbinu na mikakati atapata kutokana na miongozo pengine ya maoni kutoka kwa wanawake katika Taasisi mbalimbali. Vile vile atapata fikra mbalimbali ya kwamba jinsi gani chombo hiki kiwe lakini yeye awe ndiye msimamizi mkuu wa chombo hiki. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aongeze kasi ya kuweza kukiunda chombo hiki cha kumsaidia mwanamke. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la tano, ningeomba kuzungumza kuhusu suala la ukatili kwa kuwaua wanawake wazee. Hili suala tunalisikia sana katika redio, tunaona kwenye *television* jinsi gani wanawake wazee wanavyonyonyaswa hususan wa Mkoa wa Shinyanga utaona kwamba kuna wanawake wanadhalilika na wanajihisi kwamba wao ni watumwa katika nchi hii. Kuwa mtumwa ni kwamba unajihisi huko huru, unaogopa hata kutembea. Sasa hapa sisi katika nchi yetu tumeshajikomboa, tumeshapata uhuru. Kwa hiyo, nafikiri haya mambo ya kuifanya nchi yetu baadhi ya Mikoa wanawake wawe kama watumwa, nafikiri hili halipo katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wizara hii ikashirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuona kwamba jambo hili halifanyiki kwa sababu inamnyima haki ya kuishi mwanamke huyu katika nchi yake iliyokuwa huru. Vile vile inamfanya awe mwoga na nchi yetu hii wanawake sio waoga, ni wanawake ambao wanachangamka wanataka maendeleo ya nchi yao. Sasa leo mwanamke kuwa mtu mzima imekuwa kosa jamani?

Kwa mwanamke kuwa mtu mzima ni fahari, kwa nchi hii kufikia miaka 60 au 70 bado uko hai na wenzetu wengine wa nchi nyingine wanawaenzi wanawake kama hawa, leo sisi tunawaua kwa sababu macho yao ni mekundu tunasema hawa ni wachawi! Mimi nafikiri dhana hii tuiondoe katika nchi yetu. Hii ni kurudisha nyuma maendeleo ya wanawake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, suala hili litungiwe sheria kwamba huu ni ukatili wa hali ya juu. Naomba Serikali isaidie hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nisigongewe kengele ya pili, ningeomba kuzungumzia kuhusu utupaji wa watoto wachanga. Kwa kweli sisi suala hili linatumiza sana kama wazazi. Mimi nalizungumza kwa uchungu sana kwamba kweli sisi wanawake tunatupa watoto! Kuna sababu nyingi tu mtu pengine anajihisi amtupe mtoto. Lakini hata hivyo nafikiri Wizara vile vile ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani kuliona hili kwamba ni suala ambalo ni gumu sana. Mbali na kwamba utavunja sheria na sheria itachukua

mkondo wake ukigundulika kama wewe ndiye uliyemtupa mtoto, lakini vile vile na Mwenyezi Mungu naye atapitisha mkono wake kuona jinsi gani wewe kakupa riziki hii, mtoto yule kakaa tumboni miezi tisa, umemzaa kwa uchungu, halafu unamtupa.

Mimi naamini kwamba bado wanawake tunahitaji kupatiwa elimu ili ituwezeshe kuona kwamba hawa watoto tukiwalea na kuwatunza ni Taifa la leo na ni amana kubwa kwa sisi wanawake. Ndio maana leo unaona hapa tuko wengi Wabunge, Mawaziri kwa sababu tumelelewa na wazee wetu vizuri, kwa matunzo mazuri.

Kwa hiyo, natoa tena rai kwa wanawake ikiwa ni wasichana au wanawake wajane kwamba hili sio jambo zuri kwa kweli. Turudi kwa Mwenyezi Mungu wetu. Kwa sababu huyu Mungu tunamwamini sote ikiwa ni Muislam unamwamini Mungu yupo, ikiwa Mkristo na hata ukiwa huna dini unaamini kwamba Mungu yupo. Kwa hiyo, naamini kwamba hili jambo bado tulifikirie kwamba sio jambo zuri na tutoe elimu kwa wanawake wenzetu, tutoe rai na tutafute ufumbuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nisingependa kugongewa tena kengele ya pili, naunga mkono tena hoja hii mia kwa mia. Nashukuru na ahsante. (*Makofi*)

MHE. MONICA N. MBEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kabla sijasahau, naomba niseme kwamba naunga mkono kwa dhati kabisa hotuba ya Wizara hii ambayo kwa hakika kama tulivyoiona ni nzuri sana na kwa kweli Wizara imejitahidi kuweza kuangalia makundi yake yote kwa maana ya jamii nzima ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba na mimi niungane na Wabunge wenzangu katika kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yeti Mwalyego, aliyefariki akiwa hapa Bungeni na pia natoa pole nyingi sana kwa wananchi wake wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pia naomba nichukue nafasi hii kutoa pole nyingi kwa Wabunge hapa Bungeni ambao wamefiwa na watoto, wengine wamefiwa na wazazi na pia naomba nitoe pole kwa Wabunge ambao wamepata majanga mbalimbali ya ajali barabarani, kupigwa na majambazi barabarani na pia kuibiwa kama ambavyo Mheshimiwa Venance Mwamoto, ameibiwa kila kitu huko Iringa.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nichukue nafasi hii kutoa salaam za pongezi kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi mkubwa alioupara na hivyo kuwa Mbunge tena kwa mara nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo mwanzo naiunga mkono kwa dhati hotuba hii na kwa kweli hotuba yangu au mchangano wangu ni mdogo kwa ajili ya kushauri au kutoa maombi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Wizara hii imeweka mipango mizuri sana kwa upande wa kutoa Elimu ya UKIMWI kama tunavyoona katika ukurasa wa 12, inaonyesha Vyuo vyake vyote vinavyohusiana na maendeleo vitakuwa ni vituo vya kutoa Elimu ya UKIMWI na amejitahidi sana kushirikiana na Halmashauri zetu katika kuweza kutoa elimu mbalimbali kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana nishauri kuhusu madhara haya ya UKIMWI na madhara haya yanahu watoto yatima. Nashauri kwamba Wizara hii pamoja na kwamba itakuwa na *Desk* ambalo litakuwa linashughulikia jinsia, nashauri kuwe na *Desk* ambalo kwa makusudi kabisa litashughulikia watoto yatima. Nasema hivi kwa sababu watoto yatima sasa hivi ni wengi sana na wanazidi kuongezeka siku hadi siku. Sasa tusipoweza kuwa na mpango ulio thabiti, ina maana hata hili *Desk* ambalo litakaa katika Wizara nyingine zote kwa ajili ya kufuutilia masuala ya jinsia, ina maana tutakuwa tumechelewa kwa sababu tutakuwa tunaangalia mtu aliyekwishakua lakini huyu mtoto ambaye kutoka mwanzoni hakulelewa na mama mzazi, ameletelewa pengine na jamii tu au watoto wengine kama ambavyo katika hotuba hii tumeona kwamba inatambua kwamba watoto wengine wanalea watoto wadogo kwa sababu wazazi au hata jamii ambayo ni ya karibu nao wanakuwa wameshafariki. Mama anakuwa amefariki na baba amefariki, mlezi aliyekuwa anamlea naye amefariki. Kwa maana hiyo unashtukia wale watoto wanabakia wenyewe sasa wanajilea. Sasa tuwe na mpango ulio thabiti wa kushughulikia hawa watoto yatima na kwa kweli nashauri kwamba kuwe na mtu ambaye atakuwa ni kiungo kati ya Vituo ambavyo vimekuwa vikisaidia kulea watoto yatima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vituo hivi viko vingi, kwa mfano katika Manispaa yangu ya Iringa unakuta kuna Vituo vya Huruma, Faraja, Tosamaganga upande wa Iringa Vijijini, Bulongwao na Makete. Lakini najua katika Mikoa yote tuna vituo hivi vya kulelea watoto. Lakini ukiangalia vituo hivi vimekuwa vikichukua watoto wachache kwa sababu uwezo ni mdogo. Kama mahali kwa mfano katika Manispaa yangu ya Iringa watoto ambaa wako shule za msingi ni zaidi ya 4,000 ambaa ni yatima, lakini waliochukuliwa katika vituo hawafiki hata 1,000 kwa sababu hawana uwezo wa kuweza kuwashughulikia. Sasa kama Serikali itakuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba kuna mtu ambaye anapita kuona ni nini mahitaji ya Vituo hivi kwa maana ya chakula, mavazi kwa ajili ya wale watoto na pia kutoa ushauri nasaha kwa sababu hivi Vituo vinahitaji kuwe na mtu ambaye atatoa ushauri nasaha kwa hawa watoto ili wakue na elimu bora na pia wakapate malezi bora kama ambavyo wangeweza kukaa na wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, tusipoweza kuwasaidia kwa namna hiyo ina maana ndio tutakuwa tunalea baadaye kama watakuja kujilingiza au wakishatoka pale katika Vituo kwa sababu itafikiwa mahali watashindwa kuendelea kukaa nao. Wameshakuwa wakubwa, lazima watajilingiza katika masuala ambayo sio mazuri. Kwa maana hiyo tutakuwa tunarudi tena katika mpango ule ule wa kupata UKIMWI kwa sababu atakuwa hakupata elimu nzuri, hakupata ushauri nasaha mzuri na atajisikia kwamba yeze katika ulimwengu huu labda hatakiwi au ana mkosi wa aina fulani, kumbe hapana ni hali ya dunia kwamba mzazi au mlezi wake amefariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nichangie kwa upande wa akina mama na vijana ambao walikopa mikopo katika miaka ya nyuma. Nakumbuka wakati tunaanza Bunge hili la mwaka 2004 mwezi Juni, kulikuwa na swali likiomba kwamba kwa sababu kuna mikopo mingi iliyotolewa kati ya mwaka 1994 na 2000 ambayo ilitolewa wakati ule chini ya Wizara ya Vijana na pia chini ya Wizara ya Wanawake na Watoto, lakini bila kutoa elimu ya kutosha ya ujasiriamali kwa maana ya biashara ya namna ya kuendesha biashara hizo au utunzaji wa vitabu, kwa maana hiyo tunakuta kwamba vijana wale walipewa ile mikopo lakini mpaka sasa hivi wameshindwa kurejesha.

Mheshimiwa Spika, wanawake walipewa mikopo lakini mpaka sasa hivi wameshindwa kurejesha. Hata mimi katika Manispaa yangu ya Iringa wapo wengi. Sasa madhara ya kutorejesha mikopo hiyo ni kwamba sasa hivi katika kipindi hiki ambacho Wizara imejitahidi kuweka masharti mapya ya kutoa mikopo kwamba Ofisi ya Maendeleo ya jamii imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali ya namna ya kuendesha biashara, na wanawake kwa kweli wameitikia wito na sasa hivi hakuna mtu anayeshindwa kurejesha. Lakini yule mwanamke aliyekopa au yule kijana aliyekopa kati ya mwaka 1994 mpaka 2000 ambaye ameshindwa kurejesha anashindwa kupata mkopo tena kwa sababu anadaiwa. Kwa kweli inasikitisha kwa sababu ukimtafuta na akijua kwamba unamtafuta kufuata mkopo anakimbia anajificha. Kwa hiyo, anaishi maisha ya shida katika nchi yake. Anajificha huku na huko akijua leo Maafisa wanakuja kumfuatilia, basi anakimbia na kwa kweli hana uwezo wa kurejesha.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Serikali ingeweza kufumbia macho kwamba iweke hata mkato kati ya mwaka 1994 labda mpaka 1998, basi wale ambao kwa kweli kabisa walikuwa katika kipindi ambacho kulikuwa hakuna elimu kabisa, mikopo ile iweze kufutwa ili waanze upya. Kwa hakika tunahitaji wananchi wetu wote waweze kujikombua katika umaskini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukiangalia Benki zimekuwa zikitoa mikopo, Wizara, Halmashauri, lakini kwa sababu huyu mama anadaiwa deni la huko nyuma, basi anajikuta kwamba yeche mahali popote atakapokwenda hataweza kufanikiwa. Lakini kama tutaweza kumsaidia na kufuta huu mkopo, basi inakuwa tumemsaidia kwa hiyo, ataanza ukurasa mpya ambao utaweza kupata mikopo na hivyo kuweza kupambana na huu umaskini ambao kwa kweli kila mmoja tunaona anahitajika kupambana nao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba nirudie tena kusema kwamba naunga mkono sana hotuba hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Zaidi nitoe pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Naibu wake, Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu, Bibi Hilda Gondwe, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara kwa kutuandalia hotuba nzuri, iliyofafanuliwa vizuri, kwa Kiswahili mwanana kwa kweli. Niseme wenzenetu hawa kwa Kiswahili aah! Wamefuzu kwa kiasi kikubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo naomba nitoe shukrani za jumla kwa Waziri, Naibu Waziri na Wizara kwa jumla wake kwamba mimi nawashukuru, wananihirikisha sana katika siku kuu za Kitaifa zilizoko chini ya Wizara yao. Kwa mfano, Siku ya Mwanamke Duniani, Siku ya Familia na Siku ya Mtoto wa Afrika. Kwa kweli huwa wananalika rasmi kama Mbunge mlemau pekee niliopo humu ndani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu katika vipengele hivi kuna walemau, kuna mwanamke mlemau kwenye hii siku kuu, kuna mtoto mlemau kwenye hii siku kuu, kuna mtoto mlemau, kwa hiyo, kwa kweli hawajisanahau na ndani yake humo ndimo ninapata uzoefu na mafunzo na kukutana na wenzangu hawa na wao wakajisikia kwamba bado wanathaminwa katika jamii hii. Kwa kweli hilo nimeona nilitoe wazi, ni Wizara ambayo inanishirikisha kinyume na Wizara zingine mtambuka ambazo na sisi tumo. Ahsante sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nianze kuingia kwenye hoja yenye. Kuhusu suala la mikopo, Wizara naipongeza kwa kujitahidi kutoa fedha ndani ya Halmashauri zetu kuitia taratibu ambazo wameziweka ili akinamama waweze kukopa kwenye mfuko huo wa wanawake. Kijana mwanamke na mama mtu mzima mwanamke. Lakini kama walivyotangulia wenzangu inasikitisha kwamba Halmashauri zilizo nyingi wanapaswa kutoa kifungu chao kuchangia mfuko huu asilimia 5 hazitoi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi wakati mwininge huwa nashangaa hasa baada ya kuwa Diwani. Habari hii ya kuchangia asilimia 5 mfuko wa Vijana na Wanawake ni agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kwa Halmashauri nyingi agizo hili wala hawalitekelezi na sijui wanafanya nini. Sina maana ya kuchongea Wakurugenzi, lakini hivi inakuwaje sasa? Kwa sababu katika kuchangiana namna hiyo mfuko huu ungeweza kutuna kwa hiyo wanawake katika vikundi vingi wakaweza kukopeshwa. Lakini hali sivyo ilivyo. Kwa msingi huo hata fedha ambazo zinakopeshwa vikundi vyta akinamama ni kidogo sana kwa sababu fungu bado ni dogo sana. Labda sasa hapa nijaribu kurudi nyuma kwa Wizara yenye hiyo hiyo, je, Wizara ina mkakati gani labda kwa upande wake yenye kuweza kuwasaidia hawa akinamama kuwapatia fedha nyingi zaidi kama Halmashauri bado zinaendelea kugoma. Lakini kweli tuzidekeze Halmashauri kugoma na hali halisi ni mwanamke huyu ndiye anayezalisha fedha hizo za nchi hii kwa njia mbalimbali kwa kuitia kilimo na mengineyo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo hilo la mikopo, pamoja na kuipongeza Wizara, lakini nitoe masikitiko kwamba ndani ya Halmashauri zetu wanawake wenye ulemavu hawapati nafasi ya kukopeshwa. Sina uhakika ni kutokana na uhamasishaji labda mdogo au wanawake wenye ulemavu hawajungu kwenye vikundi.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ningeshauri kwa sababu sisi ni wazito na uzito wetu unatokana na matatizo ya ukosefu wa elimu na wakati mwininge kujiona kwamba hatufai basi niombe Maafisa Maendeleo wa Wilaya, wa Kata katika ngazi mbalimbali wachukue jukumu la kazi yao hiyo muhimu kitaaluma ya kuwashamasisha wanawake

wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi kusudi waweze kufaidika na mfuko huu na ndiyo mfuko pekee unaokopesha kwa riba ndogo tu wakishindwa huu mabenki watayagusa, hawawezi kuyagusa na akinamama wenye ulemavu ndiyo wenye matatizo na maisha duni kabisa, tunafahamu kabisa, tunawaona mitaani, ni duni kuliko hao wenzetu ambao wana viungo vyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba kabisa Halmashauri ziweze kujitahidi angalau kutekeleza hilo na kuwahamasisha wanawake wenye ulemavu na wao wakawenza kukopa. Hata hivyo, nafarijika kutamka kwamba kuna Halmashauri chache nchini ambazo zimeonyesha mfano kabisa Maafisa Maendeleo wame wahamasisha akina mama wenye ulemavu wamejiunga na wanatoa mikopo. Kwa mfano, Halmashauri ya Kigoma Vijijini, niliweza kuwepo huko mwezi wa tano vikundi sita kati ya nane nilivyota fedha za mifuko ya mikopo ilikuwa ya akina mama wenye ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wamehamasishwa wamejiunda, wameelimishwa jinsi ya kuendeleza mradi, wamepewa laki tano tano. Inawezekana kama kweli tukinuia kufanya hivyo. Wilaya nyingine ambayo napenda kuipongeza ni Kahama, Morogoro Mjini na zinginezoo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa ninalolisema ni kwamba inawezekana, nichukue nafasi hii kuweza kuomba Halmashauri zingine ziweze kuiga mfano wa hiso chache nilizozisema huenda na nyingine zipo. Sijui kama Wizara itaweza kunisaidia kunipa *data*, huenda na wengine wapo. Lakini nahimiza Wizara ikishirikiana na Halmashauri iweze kufanya hiyo kazi ya kuhamasisha kusudi akina mama wenye ulemavu waweze kufaidika. Kwa kweli wanalamika na mimi huwa ninawahimiza kwamba jiundeni kwenye vikundi. Wanapojiunda hakuna wanachokipata. Kwa hiyo, nafanya kazi bure na wanania kidogo kama vile wala sifanyi yale ambayo napaswa kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na hotuba iliyozungumzia juu ya benki ya wanawake na nipongeze tu mchakato mzima jinsi unavyoendelea kwa sababu kama wenzangu walivyotangulia hiki chombo kinaweza kikawa ni ukombozi wa mwanamke hasa yule wa kijijini katika nchi yetu. Lakini hapa ningependa kushauri ili kuharakisha mchakato huo basi Wizara ishirikiane kwa karibu sana na Wizara ya Ushirika na Masoko kuweza kuhamasisha uanzishwaji wa *SACCOS* hizi za akinamama, ili kama Wizara inavyodhamiria ndiyo tuanzie hapo na hiyo benki haraka iwezekanavyo. Pawe na ushirikiano wa karibu sana kwa sababu Ushirika na Masoko nayo ina kazi hiyo hiyo ya kuhamasisha *SACCOS* na kuimarisha. Kwa hiyo, hizi Wizara mbili zifanye kazi kwa karibu sana kama ukurasa wa 21 unavyosema tuweze kuona nini kinatokea.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo kwa taaluma yao ni watu muhimu sana mimi ndivyo ninavyowaona. Ninawahesabia kana kwamba ni watu ambao wanaenda msituni, msitu mkubwa tu, wao ndiyo wanaanza kufyeka magogo, wao ndiyo wanaanza kukwangua kwangua halafu baadaye trekta inaingia inalima, inapanda, kwa nini nasema hivyo. Wao ndiyo wahamasishaji namba moja kabla ya mganga hajaenda kwenye suala la kuhamasisha uchemshaji wa maji ili wananchi wasiwe na kipindu pindu ni Afisa

Maendeleo ndiye anayekwenda kule kwa kutumia taaluma yake kuhamasisha hawa wananchi ndipo anaripoti Afisa Afya kule mambo sawasawa. Ndiyo anakwenda sasa kueleza kutoa taaluma yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni watu muhimu sana hawa mimi ninavyowaona katika hali zao. Sasa inasikitisha kuona kwamba bado idadi yao ni ndogo na uwezo wao wale wa ngazi za chini unahitaji kuongezwa. Kuongezwa kwa vipi, kwa taaluma, kwa sababu sasa hivi kwa mfano dunia yetu hii iko kwenye mabadiliko ya kiuchumi, sembuse chini ya karne ya utandawazi ambayo inahitaji mambo mengi kidogo kujiwaka sawa.

Kwa hiyo, ningeomba taaluma pamoja na kwamba napongeza Wizara imeshasema hapa kwamba Tengeru kumeongozwa kozi mbili. Mimi nashauri kozi na mambo ya kisasa yaongezwe katika vyuo ambavyo vinachukua wahitimu wa cheti. Kwa mfano hiyo Buhare, Rungembra na Misungwi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hawa wa cheti, ndiyo wanaokwenda kule chini na kule chini ndiyo kuna wananchi wengi kabisa huko vijijini na ngazi ya Kata. Kwa hiyo, hawa wafundishwe haya ya kileo ili angalau hata wanapotoa taaluma hiyo ya kuwahamasisha wananchi kule waendane na wakati na mambo yanayopaswa katika dunia ya leo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeelezwa kwamba kuna utafiti umefanyika wa jinsi ya kuanzisha na kuendeleza biashara bora kwa upande wa wanawake. Nashauri kutokana na taarifa hii endapo utaratibu huu utaanza kusambaa, ninaomba kabisa kabisa wanawake wenyewe ulemavu wasisahauliwe. Washiriki kikamilifu kwa sababu hawa ndiyo hata wakijiunda, elimu yenye kwanza wengi wameikosa hata ile ya msingi. Sasa wasiposaidiwa hata jinsi ya kuendesha hizo biashara, hii mikopo ninayoizungumzia nayo itakuwa hata haina maana. Kwa hiyo, kwa sababu kuna mkakati umeanza hapa naomba kabisa, kabisa, kabisa wasisahauliwe ili na wao waweze kufaidika na utaratibu huu ambao utafiti umethibitisha kwamba unafaa na ndiyo utakaotuendeleza.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hotuba katika ukurasa wa 37 unaozungumzia unyanyasaji wa wanawake na watoto nchini na moja ya sababu nadhani ni mila potofu ambazo bado tunazo. Sasa hapa imewekwa tu wanawake na watoto jumla jumla, mimi ninajikita kwa wanawake wenyewe ulemavu na watoto wenyewe ulemavu. Hawa wananyanyasika haswa. Watoto wenyewe ulemavu kama nilivyochangia kwenye Wizara ya Elimu na Utamaduni, shule wanafanya kuisikia. Elimu kwa wengi wanafanya kuisikia. Pamoja na MMEM ya sasa kutokana na matatizo mengi tu wanazagaa wanazagaa hawana elimu na elimu ni haki ya msingi. Akinamama wenyewe ulemavu waliofikia umri wa kupevuka, wanabakwa ovyo tu hawawezi kujitetea.

Mheshimiwa Spika, waliowahi kuolewa basi unaolewa lakini mwanamume akiishachoka, choka unaachika haraka tu. Wewe tatizo na mtoto tatizo tena bahati mbaya umzae aliyelemaa, ni balaa, matatizo ndani ya shida. Silaumu kwa sababu katika hali

hiyo wewe mwanamke ambaye kimila unahesabika kwamba ndiyo trekta ya nyumba, hujiwezi, utafanya nini, unaonekana haufai kitu.

Mheshimiwa Spika, unanyanyasika sana. Akinamama wengine wanafikia kiwango yeze ni mzima, lakini anabahatika kuzaa mtoto mwenye ulemavu, mwanamume anamwacha. Kwa ushahidi wangu Morogoro, mama amelia na mtoto ambaye aliishia kutokuwa sawasawa kwa sababu ya utindio wa ubongo mpaka mtoto yule alipofariki, mme amemwacha. Watoto watano ni wazima, yule wa sita alikuwa mlemavu, ameacha familia nzima na wale watano pia wananyanyasika.

Mheshimiwa Spika, hili mimi nakubaliana nalo, ninaloshauri hapa ni tuziangalie upya Sheria zetu, ziingize na masuala haya kiundani zaidi kuliko kujumlisha jumlisha, labda itasaidia sana. Lakini kwa sasa hivi nasema kwa uchungu ni manyanyaso ambayo yapo ya kwamba hata mwenye ulemavu wa kawaida ukiona wenzako wanavyoteseka, unasema eeh! Kuolewa ya nini, kuzaa ya nini na ukata tamaa. Lakini kuolewa na kuzaa ni haki ya binadamu, lakini unaogopa sasa, unaona Mungu wangu, haya mambo yamezidi, mateso juu ya mateso.

Kwa hiyo, naomba katika suala hili Wizara ishirikiane na *NGOs* tuone kwamba mila potofu na Sheria zetu tunaweza kuzirekebisha vipi kusudi pawe angalau na hali inayoelewaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi leo sikuwa na mengi sana ya kuzungumzia. Niseme tu niwatakie kheri Wizara na niipongeze kidogo Serikali. Nimeona katika fedha walizotoa za maendeleo angalau milioni 6 pamoja na uchache wake zimetoka humu humu nchini.

Kwa hiyo, angalau Serikali inaanza kuona labda umuhimu wa masuala haya na zile milioni 2 na kitu ndiyo tunazipata kutoka nje. Lakini bado niombe kabisa kama wenzangu walivyozungumza, Wizara hii ni nyeti. Ndiyo wazalishaji wa binadamu sehemu kubwa ipo hapo. Ndipo watunzaji wa binadamu sehemu kubwa iko hapo. Sasa hii sehemu tusipoiweka sawasawa hata hao wajao watakuwa si sawasawa kama inavyosemwa ukimwelimisha mwanamke ndiyo umeshamaliza dunia kuielimisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono tena. Nawatakia kheri watekeleze haya walivoyaweka kwa fedha chache walizo nazo. Naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kabla ya yote naomba niseme naunga mkono hoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi yao nzuri walioifanya ya kuandaa hotuba hii katika shida ambazo ninaziona za ufinyu wa bajeti yao. Lakini wamejitahidi, wamefanya kazi nzuri na hata sisi tunawashukuru kwa kujitahidi hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuipongeza Wizara kwa jinsi inavyoshirikiana na Wizara nyingine na Mashirika mbalimbali ambayo yanashughulikia shughuli za wanawake kama vile *TAMWA*, *TAWLA* na *NGOs* nyingine ambazo zinajishughulisha na maendeleo ya wanawake. Mmeonyesha uhusiano mzuri na sisi tunamshukuru sana Waziri na wenzake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jinsi wanavyosimamia maendeleo ya wanawake huko vijijini katika hali ngumu. Wizara hii ndiyo ilikuwa ya kwanza katika kuwahimiza wanawake kutengeneza vifaa ili waweze kujikomboa kwanza, waweze kuuza na kupata fedha za kuweza kujikimu. Lakini vile vile katika Bunge lako hili la mwaka 1995 Wizara hii ilianzisha maonyesho yale ya Saba Saba ikishirikiana na Mheshimiwa Mama Anna Mkapa na mpaka sasa huko vijijini tunaona jinsi watu wa maendeleo wanavyojitahidi kuwasukuma wanawake ili waweze kutengeneza vifaa na waweze kushiriki katika shughuli hii ya maendeleo ambayo ni muhimu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba waendee na moyo huo wa kuweza kuangalia kazi za wanawake pale walipo ili ziweze kulitangaza Taifa letu na liweze kuwasaidia wanawake kujikomboa kupata matumizi yao wenyewe kwa kupigana na umaskini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Wizara hii kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake nadhani hakuna mtu anayeweza kudharau. Ni Wizara muhimu. Ni Wizara ambayo watu wake kama alivyosema aliyenitangulia kuzungumza, wanakwenda vijijini kuishi na watu na mtu anayeishi na watu ndiyo wanayemwamini na unaweza kuchukua ushauri anaowapa. Kwa hiyo, Wizara hii ni muhimu kwa mabadiliko yoyote ambayo tunayahitaji katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba sana Serikali kwa umuhimu wa Wizara hii ilivyo, Serikali ijitahidi sana kuongeza fedha za bajeti ili waweze kurahisishiwa kazi zao waweze kuwafikia wananchi na hasa hasa wawafikie wanawake amba mara nyingine huwa hawapendi kutoka mpaka mtu amemwamini. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imefanya kazi kubwa ya kuwatoa wanawake uani na kuwapeleka nje kuonana na watu wengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, basi mtu aliyetufanyia kazi hii kwa nini tusiweze kuona kwamba huyu atatusaidia, maana ni uwekezaji, uwekezaji wa kumkomboa mtu ambaye haelewi ndiyo utakaotusaidia kumfanya huyu akawaeleweshe wasioelewa. Kwa hiyo, tunawekeza kwa watu wa maendeleo ili wakatuvulie wale watu tunaowahitaji katika q shughuli za nchi yetu. Kwa maana tukiwaelimisha sana hawa watu wa maendeleo basi tutakuwa na watu wanaoelewa. Watu wanaowafikia wananchi sawasawa na watumishi wa Wizara hii wanaweza kugawa fedha zao walizozipata katika sehemu zile ambazo bado ziko nyuma katika kuchangia michango yao katika nchi hii ili tuongeze tija. Tuongoze uwezo, tuongeze ufahamu wananchi waweze kujifunza kutoka kule nyumbani.

Mheshimiwa Spika, hizi shilingi bilioni 4 tuseme karibu shilingi bilioni 5 kwa Wizara hii mimi kwa kweli nashangaa. Zimeongezeka kidogo kuliko zamani, kuliko mwaka uliopita na mwaka ule mwingine. Lakini ni kwa nini kuongeza kwa bajeti ya Wizara hii kuwe kidogo sana kuwe kwa chini. Wizara hii ni ya watu wote. Ni ya wanaume na wanawake maana kama ingekuwa maendeleo ya jamii, wanawake na watoto ningesema labda Wizara inadharauliwa labda kwa sababu ni ya wanawake maana wanawake wako chini. Lakini sasa tukabadilisha na jina iwe ya wote.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini tusibadilishe mawazo ya kuweka bajeti ikawa kubwa kwa kuwahudumia wote? Ni kwa nini bado tunaiangalia kwa jicho la namna gani sijui sielewi Kiswahili labda. Jicho gani ambayo Wizara hii inaangaliwa kupewa fedha hizi ndogo kwa maendeleo shilingi milioni 600. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fedha hii ni kidogo sana. Mimi sielewi niseme nini. Nilipokuwa nimesoma haraka haraka nikasema kwamba hivi Serikali ni kweli ina nia ya kuwakomboa Watanzania. Ni kweli inataka Watanzania ambao ni wengi ambao hawakupata bhahati ya kwenda shule wako vijijini inataka wafikie kwa urahisi wakubali masuala ya kilimo? Wakubali masuala ya maji, kuchemsha maji? Hata kuacha kuoga katika dimbwi lile lile, kufua dimbwi lile lile na kuchukua maji ya kunywa na kupikia katika dimbwi lile lile. Watu wa Maendeleo ndiyo kazi wanazozifanya. Wanafanyakazi za kukomboa mtu kweli kweli. Sasa kwa nini tuwape fedha kidogo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali kwa heshima na taadhima nilizonazo kwa Serikali yetu naomba bajeti ijayo waweze kubadilisha mawazo. Ibadilike iweze kuongeza Bajeti ya Wizara hii ili waweze kufanya kazi yao sawa sawa na waweze kuwakomboa wananchi kwa kuwafundisha. Kwa sababu ndiyo majukumu tuliyowakabidhi. Tumewakabidhi majukumu mengi, lakini tunawapa fedha kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lako Tukufu wakati fulani nikichangia Wizara hii, nilisema Serikali inataka kuwa sawa na yule mwanamme aliyekwenda kuoa mwanamke kijijini akamleta mjini, asubuhi anaondoka, nikute umepika maini na maini hajampa hela. Atanunua na nini hayo maini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, atapata wapi fedha za kununua hayo maini? Sasa Wizara inapewa majukumu mengi lakini hatuwawezeshi. Naomba Wizara, Serikali iieleze Wizara hii waweze kufanya kazi njema ambayo sisi tunatazamia waweze kuifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo, nimefurahi nimeona kuna maendeleo katika mafunzo ya *Diploma* na mafunzo ya Vyeti. Lakini maendeleo haya ni madogo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba utakapokuwa unabajeti katika bajeti ijayo weka fedha nyingi wakakukate huko na wewe uwe na kitu cha kusema mimi nilibajeti lakini nilikatwa. Walizikata kwa ajili ya ile mnaita *ceiling* sasa tujue kwamba hapa Serikali ina mpango gani. Wewe andaa usomeshe watu wengi ili waweze kufanya kazi ambayo tunawatazamia. (*Makofi*)

Kwa mafunzo ya Cheti Mheshimiwa Waziri vile vile naomba uongeze wanafunzi wa kujifunza katika vyuo vya vyeti kwa sababu hawa ndiyo tunawahitaji kwenda vijiji ni kwenda kuishi na watu kwa sababu Bibi Maendeleo au Bwana Maendeleo ni lazima aende kijiji akaishi na watu. Akawaambie watu kwamba tunapata njaa kwa sababu hatulimi kilimo bora. Tunapata njaa kwa sababu sisi tunashindwa kuweka akiba ya chakula. Tunapata njaa kwa sababu katika vijiji vingi watu hawajitokezi kulima sawa ingawa wana afya njema.

Mheshimiwa Spika, haya yote yataweza kuzungumzwa na kufundishwa kwa wananchi kwa mtu anayemwelewa anayezungumza lugha yake yaani ya chini ya kumwinua na kutaka kumnyanya aweze kwenda juu.

Mheshimiwa Spika, hatutaweza kuwakomboa wananchi kwa kusema tu hapa Bungeni wekeni vihenge, wekeni akiba ya chakula. Kwanza wewe unayesema hakujui. Hata sauti yako pengine inamtisha. Sasa nasema huyu anasema niweke kihenge yeye anacho? Aliweka lini? Sasa akiwa naye Bwana Maendeleo na Bibi Maendeleo ni mtu anayemfahamu na anampenda na atamsikiliza vizuri. Kwa hiyo, tutashangaa vihenge vinavyoota katika vijiji kwa sababu watajifunza hata namna ya kuweka akiba ya chakula kisioze. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi naendelea kuiomba Serikali iongeze pesa. Narudia kabisa pesa zilizopo ni jambo la kutisha. Napenda kuzungumzia Vikosi vya Ujenzi. Mheshimiwa Waziri naomba Vikosi vya Ujenzi viimarishwe. Tunaangaika na majengo ya MMEM, mengine tunasikia kwamba yamejengwa kwa uhafifu kabisa. Lakini tungekuwa na vikosi vyetu vya Ujenzi na kama zingekuwa vimeimarishwa tungekuwa na watu wa kusimamia majengo ya Serikali, wakishirikiana na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naomba Vikosi vya Ujenzi viimarishwe ili waweze kusaidia Halmashauri zao kwenda pamoja na watu wanaojenga majengo yetu ya Serikali hasa ya Shule ambazo tumekiriwa pesa nyingi ili tuweze kuinua hali ya majengo ya Shule.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba ameweza kuendelea kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa sababu ya uhafifu wa fedha, bado *speed* ni ndogo. Tungeomba kama tutapata wafadhili mahali popote, uchacharike huko Mheshimiwa Waziri ili tuweze kuimarishe Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa sababu ndiyo pia viko karibu na wananchi ili waweze kujikakamua na kubadilisha.

Mheshimiwa Spika tunaomba Chuo chetu cha Gera, mimi ningeomba kama mngetujengea kibwawa kwa sababu tuna maji ya kujisukuma yenyewe, maji ya *gravity* ili tuweze kumwagilia katika sehemu hii, Chuo kina eneo kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akafikirie jambo hili kuimarishe maji pale kwa sababu tuna vijito lakini mtu hakutokea wa kuweza kutuwekea bwawa ili tuweze kumwagilia maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya vijana na wanawake ni kweli ina shida kwa sababu wale wa mwanzo wamekuwa hawalipi. Lakini kwa *speed* ambayo tunakwenda nayo sasa tukipata watumishi wengi wa maendeleo najua hakika watu wote watakuwa wanarudisha mikopo hii kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba mnatuletea zile fedha na muendelee hivyo ili nasi tutakuwa tunawahimiza wananchi wanaokopa kuweza kulipa. Kwa sababu ndiyo ukombozi peke yake ambao wanao wananchi wa vijijini kwetu tunakotoka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ambalo ningeomba Mheshimiwa Waziri alitilie maanani ni kutusaidia kuendelea kuwafundisha Bibi Maendeleo na Bwana Maendeleo namna ya kuandika miradi. Kwa sababu zamani walikuwa wanafundisha na ndiyo wamesaidia wanawake wengi na waliotaka kukopa mikopo midogo midogo wanawaandikia. Basi tunaomba kwamba mafunzo hayo yaendelee kama ikiwezekana Bibi Maendeleo wote wanaokwenda Vijijini na Mabwana Maendeleo wajue kuandika miradi ili waweze kuwasaidia akina mama wanaotaka kukopa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu unyanyasaji. Elimu hii ya kuwafundisha wanawake pia wajitetee itaendeshwa kama tutakuwa na Mabibi Maendeleo ambao wana ujasiri wa kuwafundisha akina mama kule vijijini. Mmeona jambo alilokuwa analizungumzia Mheshimiwa Joel Bendera, kwamba wanawake wanapigwa na ile fimbo kwenye *television* wanatangaza tangazo moja.

Mheshimiwa Spika, uhakika ni kwamba yule hataki kumpiga mke wake, anachagua fimbo ya mchezo. Lakini kwa sababu mwanamke amezoea kupigwa anaogopa hata lile gongo la kwenye mchezo wa yule mume wake, anafikiri atapigwa.

Kwa hiyo, hali hiyo ni lazima itoke katika mioyo ya wanawake na haiwezi kutoka mpaka na hawa wenzetu waache kutupiga. Muwafundishe wanaume wenzenu kwamba, kupiga sio suluhisho la maisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia kwako, Waheshimiwa Wabunge kama jinsi wanavyosimamia mambo ya maendeleo, wakasimamia mambo ya kuvunja unyanyasaji, wengine mnawona kabisa labda mdogo wako, baba yako, shemeji yako, anampiga mkewe wala huzungumzi kitu unaondoka kwa kuwa unaogopa kwamba atakuambia aah kumbe wewe humpigi mke wako umetawaliwa.

Mheshimiwa Spika, Bwana Maendeleo na Bibi Maendeleo ndio watajua ni mwanaume gani anampiga mke wake. Tukiwa nao wengi vijijini ndio watakaojua na watajaribu kumshauri kwa sababu wanajifunza namna ya *ku-approach* watu. Hawatamkemea, watamfundisha wewe unaonaje?

Mheshimiwa Spika, wakati ule watu wanahamia vijijini nilikutana na mama mmoja Iringa, nilimwuliza wewe umefaidi nini kwenda katika vijiji? Akasema moja

ninalomshukuru Mungu, ni kwamba, tumekaa karibu na watu wengi, mume wangu anaona aibu kunipiga. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu wanaona aibu kama Mbunge atamwambia wewe nimesikia unampiga mke wako sana kwa nini, itamsaidia yule baba labda kuona aibu kwamba hata Mbunge wangu ameona ninafanya vibaya hata kama itakunyima kura siku moja lakini utapata kura nydingi za wanawake kwa sababu ndio wanatoka kwenda kupiga kura, kwanza, wanaume wengi hawatoki, wanawake ndio wanaopiga kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba unyanyasaji usipiganiwe tu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto upaganiwe na Watanzania wote kuanzia Spika, Rais na watu wa jinsia nyininge, waone kupiga ni vibaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la watoto yatima.

MBUNGE FULANI: Kengele imelia.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Imelia ya pili?

SPIKA: Eeh ni kengele ya pili.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Spika, makofi yalikuwa mengi sikusikia, naomba radhi, naunga mkono hoja.

SPIKA: Shauri ya kuogopa kupigwa, ukajisahau. (*Kicheko*)

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hotuba hii. Labda tu niseme kwamba, leo ni siku yangu ya kujikata kisu mwenyewe sababu naijua moyoni mwangu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba hii na naiunga mkono mia kwa mia. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyoifanya kipindi kilichopita na matayarisho yao kwa mwaka ujao. Natawakia kila la kheri na naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia nitumie fursa hii, kwa niaba ya wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Koani, niwashukuru hawa wafuatao, ambao walifanya ziara katika Jimbo la Koani na wakanisaidia kiasi kikubwa sana cha pesa kwa ajili ya miradi tofauti. Waheshimiwa wenyewe ni wafuatao: Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Profesa Mark Mwандоса na simsahau kabisa na kwa njia ya pekee namshukuru sana Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Shamim Khan, alitembelea Jimbo langu kutwa nzima na bahati nzuri akafika mpaka nyumbani kwangu, lakini bahati nzuri mwenye nyumba alimkuta. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku mbili, tatu, zilizopita niliona katika vyombo vyaya habari taarifa ya kusikitisha na kwa vile leo ni siku ya Ijumaa, kwa sisi Waislam, dua zetu

zinapaa mbinguni haraka, kitendo ambacho kilijitokeza ndani ya *TV*, redio na magazeti ni lazima Waheshimiwa Wabunge wote tukilaani, tukilaani kwa njia ya pekee kabisa ambapo mtoto mdogo kabisa, mfanyakazi ndani ya nyumba alibakwa na bosi wake, ambaye ni mtu mwenye kuheshimika na ni Afisa wa Ubalozi. Kwa kupitia kwako naomba suala hili kwa vile leo ni Ijumaa na siku ya kheri na bahati nzuri ni saa sita sasa hivi, tunalaani, tunalaani kabisa kitendo hicho kwa watu Watukufu kama hao kufanya kitendo kibaya kama kile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sisi wenyewe hapa tunajitahidi kutunga sheria ili tuwalinde watoto wetu, tuwalinde wasichana, tuwalinde vijana wetu wote wa kike na wa kiume, lakini wanatokea watu wenyewe vyeo vya Ubalozi wanafanya vitendo vya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia kwako, naomba Wizara hii pamoja na Wizara zote zinazohusika, zisimamie kikamilifu kuhakikisha kwamba, sheria inachukuliwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa nitazungumzia Siku ya Wanawake Duniani. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba, siku hii safari hii ilifanyika huko Zanzibar Mkoa wa Kusini Unguja. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, lakini vilevile sitaacha kumshukuru zaidi Waziri wa Zanzibar, Mheshimiwa Samia Suluhu, kwa sababu yeche ndiye Waziri wa Vijana, Ajira na Maendeleo ya Wanawake, kwa njia ya pekee alichagua sherehe hizo zifanyike Koani yaani kwenye Jimbo langu mimi. Nawapongeza wote wawili lakini zaidi namshukuru Mheshimiwa Suluhu, kwa sababu angekuwa hakutaka ifanyike pale, basi isingefanyika. Kwa hiyo, nawashukuru na *inshallah* miaka mingine wataendelea katika Majimbo mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia Siku ya Familia Duniani, mwaka huu ilifanyika huko Kigoma. Bahati nzuri vilevile kama desturi yake Wizara hii ilishirikiana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ikapeleka wajumbe watano. Lakini vilevile kwa niaba ya Mwenyekiti wangu, niishukuru Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo ya Tanzania Bara, kwa sababu ilitoa tiketi tano nyingine ili tuweze kushiriki. Kwa maana hiyo, Waheshimiwa Wabunge kumi wa Kamati tulishiriki katika sherehe hizo na tulitembelea Wilaya mbalimbali kujiona maendeleo na baadhi ya vikundi vya akina mama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nayasema hayo kwa sababu kwenye ule usiku wa familia, ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, nilitakiwa niseme neno la shukrani baada ya chakula. Lakini kwa vile maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri yalikuwa mazuri sana na walioalikwa kwenye sherehe ile walikuwa kila mmoja na familia yake, mwanaume aliambiwa aje na mkewe na wanawake wakaambiwa waje na waume zao na watoto wao lakini bahati mbaya na jambo la kusikitisha, mimi binafsi niliyeambiwa nitoe shukrani nilikuwa peke yangu. Lakini vile vile kubwa zaidi na mwenyewe Mheshimiwa Waziri, alikuwa peke yake, sikumwona Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migoro pale. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilipotoa neno la shukrani nilisema kwa desturi yetu lazima tutoe kafara. Kafara ni sadaka ya kutubu yale maasi tuliyoyafanya siku ile mimi na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri alitakiwa atoe ng'ombe 15 na mimi nitoe 10. Mimi wale ng'ombe wangu 10 nimewatoa, ninataka kujua kama Mheshimiwa Waziri ameshatoa ng'ombe 15 na kama hajatoa anasema nini katika Bunge hili? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka niliseme ni funzo ambalo lilitolewa katika siku ile ya familia. Siku ya Familia maana yake hasa ni kuona ni kwa vipi tunaishi ndani ya majumba yetu, waliooa vipi wanaishi na wake zao, walioolewa vipi wanaishi na waume zao.

Mheshimiwa Spika, leo nimesikia nyimbo ambayo Mheshimiwa Jenista Mhagama alimpa dereva wa Bunge *cassette* aiweke asubuhi. Nyimbo ile ina mafunzo makubwa sana, inawasimanga wanawake wanaokwenda njiani wakawasema waume zao kwamba hawafanyi hili na hili vile vile mna mafunzo mengine na wanaume nao wanaowasema wake zao njiani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano miwili ambayo labda itakuwa mafunzo kwetu sisi hasa wanaume. Kulikuwa na bwana mmoja alikuwa yeye nyumbani kwake siku zote anarejea saa nane za usiku. Siku hiyo ilipofika saa sita alikuwa *grocery* anakunywa pombe, akakumbuka kuwa siku ya pili alikuwa anataka kusafiri kwenda *New York* na alitakiwa aamke saa kumi na moja awahi *Airport*. Akampelekea *message* mkewe, mke wangu naomba leo uniamshe saa kumi na moja alfajiri. Ilipofika saa kumi na moja mke alivyokuwa mstaarabu, msomi na yeye akachukua simu yake akampelekea *message* mumewe. Mume kalala hoi bin taabani, alipoamka saa kumi na mbili za asubuhi akamwambia mke wangu mbona hukuniamsha? Akamwambia nimekuamsha angalia simu yako *message* nilikutumia mume wangu. Mume kahamaki kamwacha mkewe. Hayo ndio madhila ya mwanzo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ambao napenda niutoe, bwana mmoja asubuhi alipoamka akamwambia mkewe leo nimeota ndoto nzito na ndoto mbaya na wewe mke wangu umetoo? Akamwambia nimeota. Ndoto gani? Kama yako. Sasa hajui ndoto gani. Yule bwana akakoga akaenda zake ofisini. Kumbe ndoto aliyoota yule mume kaota anafanya mapenzi na *secretary* wake. Kwa hiyo, alipomwambia *secretary* kuwa nimeota ndoto hii akafurahi sana *secretary*. Akamwambia lakini na mke wangu kaota ndoto kama hii. Akamwambia basi na mkeo ana rafiki kama ilivyokuwa wewe ni rafiki yangu mimi. Mume aliporejea nyumbani akampa talaka mkewe. Hizo ndio tabia zetu mbaya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu fedha ambazo Wizara inapeleka katika Halmashauri ili ikopeshwe vikundi mbalimbali. Naipongeza sana Wizara kwa sababu fedha ambazo wanazipeleka wanazipeleka kwa maslahi mazuri kabisa na ni fedha nyingi sana. Lakini tatizo ni kwamba, Wizara hii haipati ushirikiano kutoka Halmashauri za Wilaya ambazo fedha zinapelekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu ni kwamba, Halmashauri za Wilaya ndizo zinazopaswa kuzisimamia kikamilifu fedha hizo, wanazipokea, wanazikopesha, zinatumwi ipasavyo na zinarejeshwa. Lakini kwa mujibu wa barua au agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu na Halmashauri zilitakiwa zichangie asilimia kumi ya mapato yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo tumelikuta Halmashauri nyingi zinapuuza kutoa hiyo asilimia inayotakiwa na nasema huo ni ujeuri, ubabe, ukiritimba, wanaoufanya kwa sababu Halmashauri kama kweli inasimamiwa na Waziri anayehusika wa TAMISEMI, hakuna sababu hata moja Halmashauri hizo ziachiwe zisitoe asilimia kwa barua ambayo Mheshimiwa Waziri ameitoa. Kwa kupitia kwako, namwomba Waziri wa TAMISEMI ahakikishe kwamba, Kamati yetu itakuwa kali sana na kama tutashindwa tutamwona Waziri Mkuu mwenyewe kuhakikisha kwamba, fedha hizi zinatolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2001/2002, Wizara hii ilitoa Sh.456 milioni kupeleka katika Halmashauri lakini bahati mbaya kwa sababu ya usimamizi mbaya, marejesho yalikuwa Sh.308,982 milioni, mpaka sasa hivi kiasi kilichokuwa hakijarejeshwa ni Sh.147 milioni. Mwaka 2002/2003, fedha zote zilizotolewa na Wizara zilikuwa Sh.452 milioni, marejesho bahati mbaya ni shilingi milioni moja, bado bazijarejeshwa Sh.451 milioni. Lakini naipongeza sana Halmashauri ya Makete, Halmashauri zote hazijarejesha isipokuwa wao tu ndio wametoa shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuchangia ni vituo vya watoto yatima. Waheshimiwa Wabunge, wamezungumza hapa lakini bado iko hoja kwamba, mbali na Serikali inasaidia, *NGOs* zinasaidia, lakini hali za watoto yatima katika vituo ni mbaya sana. Nashauri viongozi wa dini zote Waislam, Makadiani, Wakristo, wasiokuwa na dini, tujenge tabia, tuwatangazie waumini wetu kwa kujenga tabia kila siku za sikuukuu zetu, kabla hatujala chakula kizuri wala kuvaan nguo nzuri, tujaribu kuweka mfuko maalum kwa kila mtu ndani ya familia yetu ili fedha zile zipelekwe katika vituo. Nadhani tukijenga tabia hiyo hata Serikali itafaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utupaji wa watoto, tabia hii imezagaa sana na inaendelea lakini cha kusikitisha sijui hata sababu ni nini. Kitendo ambacho unakifanya wewe hata ukampata mtoto ni kitendo cha makubaliano, baada ya ridhaa yako wewe mwanamke na mwanaume, mnakifanya kwa mapenzi, siri, lakini matokeo yake kiumbe ambacho kinakuja duniani ambaye atakuwa kiongozi baadaye, anatupwa jalalani au chooni. Hii ni tabia chafu na lazima kila tunapohubiri, kila tunapozungumza katika mikutano yetu, tujaribu kuwaelimisha hawa wenye tabia hii waache kwa sababu sheria ipo.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia chombo cha wanawake. Mheshimiwa Waziri, amezungumzia vizuri kabisa na mimi nampongeza. Labda nitoe rai yangu zaidi. Wenzetu Afrika Kusini wao wanacho chombo hiki lakini tukitaka sisi Tanzania tufanikiwe lazima chombo hiki cha wanawake kitamkwe ndani ya Katiba yetu ya Tanzania. Kikitamkwa ndani ya Katiba kitakuwa na nguvu kuona kinasimamia vyema zaidi juu ya mambo na maslahi yote ya akina mama. Chombo hiki ndicho kitakachoweka

muongozo mzuri wa Wizara zote kuona mwanamke habaguliwi kwa sababu ya uanamke wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameotea kwa sababu kabla chombo hakijaundwa, wiki nne zilizopita, alituonyesha muundo wa ofisi yake. Inaridhisha na inafurahisha kuona asilimia kubwa ya wafanyakazi wake ni wanawake na kazi inayofanywa katika ofisi yake ni nzuri na kubwa. Hii inaonyesha uwezo wa wanawake namna ulivyo. (*Makofi*)

Vilevile Mheshimiwa Waziri, naye kwa Wizara yake kwa sababu sisi ni Wizara ambayo tunaisimamia, tumeitembelea, inafurahisha kuona naye vilevile amejitahidi lakini juu ya jitihada zake bado aangalie zile nafasi ambazo wanawake wanaziweza hata ikiwa za udereva, nashauri Mheshimiwa Waziri, usiogope kumweka dereva mwanamke. Nakuomba kwa mara hii unikubalie Mheshimiwa Waziri, nadhani heshima yako itakuwa kubwa sana, hutokuwa ngariba wa pobwe kama utamweka dereva mwanamke, nakwambia na atakuendesha vizuri. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulichangia la jumla ni kuhusu bajeti ya Wizara. Hatuilaumu Wizara kwa kupata bajeti ndogo, lakini tunaiomba Serikali ione kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara hii na ijaribu kadri iwezavyo, kipindi kijacho waongezewe asilimia ingawa safari hii wameongezewa kidogo lakini waongezewe tena ili kuona nao wanafaidika na utendaji wao mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na nawaombea kila la kheri na naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kabla ya yote, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu na Wizara kwa jumla, kwa kutuletea hoja fasaha na maelezo mazuri kuhusu Wizara hii.

Tatu, nawapa pole wote waliofikwa na mikasa katika kikao hiki cha bajeti ya kufiwa na ndugu na jamaa zao, pia nawapa pole wapiga kura wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kumpoteza Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Yeteh Mwalyego.

Mheshimiwa Spika, naomba niingie kwenye hoja iliyo mbele yetu. Mimi nataka kuzungumza jambo moja tu, nalo ni dhana ya maendeleo ya jamii. Wizara hii kuitwa Maendeleo ya Jamii haikuwa bahati nasibu. Nadhani Mheshimiwa Rais, alikuwa na maana kwamba, jamii yetu iko nyuma na kwa maana hiyo ni lazima iundiwe Wizara na Wizara hii iwe kichocheo ambacho kitasababisha jamii yetu iende mbele. Sasa katika

Ibara ya 68, ukurasa wa 38 na ya 69 na 70, inatoa maelezo hayo kuhusu dhana ya maendeleo hasa hasa katika karne hii ya 21 ya utandawazi na maendeleo makubwa ambayo yanapatikana duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana, Wizara yetu ipo lakini mategemeo yaliyokuwa katika vichwa vyetu inawezakana yakawa madogo. Kwa sababu tulitegemea kioo cha maendeleo yetu kingekuwa ni vijiji vyetu, ni watu wetu huko vijijini na vitongojini na hivyo ndivyo walivyokuwa wanazungumza wataalam wengi wa Sayansi za jamii, Augustine Compte Jeremy Bentham na wengine wamezungumza vizuri sana kuhusu dhana ya maendeleo ya jamii kwamba, kioo na kipimo cha maendeleo katika jamii ni lazima viwe vijiji na watu waliokuwa nje kabisa ya miji. Jamii itahesabika imeendelea ikiwa watu kutokana katika maeneo yaliyokuwa mbali na miji wamestaarabika, wana uwezo wa kujieleza, wana elimu ya kutosha, wana vitu vyote ambayo vinahitajika kurahisisha maisha yao, hapo ndipo itahesabika jamii hiyo imeendelea, kinyume cha jamii yetu Tanzania, vijiji vyetu bado viko nyuma sana. Kwa maana hiyo, tuna kazi kubwa sana. Wizara hii nafikiri ingekuwa imeangaliwa sio kwa jicho la kawaida na sio kwa mizania ndogo kama hivi ya shilingi bilioni nne, hapana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala hili limezungumzwa vizuri na Mheshimiwa Rhoda Kahatano na sina haja ya kulirudia na Mheshimiwa Haroub Said Masoud, pia amelizungumzia, ufinyu wa bajeti katika Wizara hii, sina ya kuzungumza tena. Kwa nini leo tunapozungumza kupunguza umaskini kufuatana na Dira yetu ya 2025 tukifika mwaka huo tumeondoa umaskini au tumeondoa umaskini uliokithiri katika nchi hii na wakati huo huo tunategemea umaskini huo kuondoshwa kwa miujiza tu kwa kutamka au kwa kuona kwamba, pengine unawenza kuondolewa na fulani wakati ambapo tumeunda Wizara sasa ambayo ndiyo itakayoshughulikia na kuendeleza jamii badala yake Wizara hii tunaivalisha kilemba cha ukoka? Ukitzungumza hela za maendeleo katika Wizara na masuala ya maendeleo ya jamii, shilingi milioni sita kutoka hela za ndani, tunazungumzia nini?

Sina haja ya kuingilia huko kabisa lakini ninachosema ni kuwa, dhana ya maendeleo ya jamii maana yake ni kuanza vijijini na sio kuanza mijini. Wizara yetu imepangaje maendeleo kutoka vijijini kuelekea mijini kiasi ambacho taratibu hizo ndizo ambazo zitamkwamua mtu wa kawaida kijijini aweze kuona kweli ameendelea kwa kumpelekea vifaa vyote ambavyo vitaweza kumsaidia katika maendeleo yake. Hilo la kwanza nilitaka kuzungumza katika dhana ya maendeleo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili, vyuo vya maendeleo vijijini, vyuo hivi nashukuru Wizara inajitahidi lakini vinapimaje maendeleo ya vijiji hivyo ambapo vyuo hivyo au kanda hizo hivi vyuo vipo, vinapima kwa kigezo gani na kwamba kazi inayofanyika kule kwa ajili ya vyuo hivi ili kuviendeleza vijiji katika kanda ile inafanyika kwa kasi gani? Mimi nasema vyuo vya maendeleo wazo lilikuwa zuri lakini upimaji wake mwaka hadi mwaka, ulikuwa unafuata utaratibu gani na vigezo gani vilivyotumika kwa kupima maendeleo au kwa kupima kazi ya vyuo hivyo inavyofanya kwa ajili ya kanda hizo au vijiji hivyo au maeneo hayo kuendelea?

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na Ibara aliyokuwa ameitoa Augustine Compte kuhusu suala la dhana ya maendeleo ya jamii. Ibara hiyo inasema: "Ukitaka kuona mtu ameendelea, usimwangalie yule mtu mwenyewe angalia yale anayofanya." Hiyo katika lugha ya Kiswahili. Anayofanya ni ya kimaendeleo au ni ya kumuweka hapo hapo alipo? Kusema kweli sisi inawezekana Watanzania mtu akituona mijini tuna viwanda, tuna madini mengi, tunashughulika na kadha wa kadha, lakini matendo yetu tunayoyafanya, je, matendo hayo yanaweza kupimika kimaendeleo kwamba kweli mtu huyu ameendelea? Hilo ndio la msingi usimwangalie mtu mwenyewe, angalia matendo yake na mambo yake. Nasema kwa hali hiyo basi sisi katika maeneo yetu sio tu kusema tumepeleka kitu kadhaa, mikopo kadhaa, hapana, tuangalie ni jinsi gani tumewafanyia wale ili watu wale wajikwamue hatimaye sio kwa kuonekana kwao bali kwa matendo yao wanayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wataalam wa Falsafa Walisema kama unataka kumwondoa mtu katika njaa usimpe chakula cha wakati ule, kama unataka kumpa mtu kitoweo usimpe samaki akatowelee wakati ule bali mpe kile kitu cha kumletea samaki kila siku, yaani mshipi wa kuvulia samaki. Je, tumeefanyaje sisi kiasi ambacho katika vijiji vyetu, katika maeneo yetu, kumkwamua mwanamke, mtoto, mzee, Mtanzania aliye kijijini ili aweze kufanya yale ambayo kila siku ataonekana ye ye ni mwenye kufaidika kwa hayo anayoyafanya, sio kumpelekea kitu kitachomdumaza, akae akitegemea kwamba atakuja kufanyiwa tena mara ya pili, tatu na mtu mwingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo nalisema katika dhana ya maendeleo, bado Wizara ina kazi kubwa na nimetaka kuzungumzia hilo tu pekee kwa makusudi kwamba, Wizara ina kazi kubwa katika kuendeleza jamii kwa sababu jinsia (yaani mwanamume na mwanamke na watoto) wote wako katika jamii. Kwa maana hiyo, tukiendeleza jamii, tukaangalia yale mambo ya msingi ya kuwafanya waweze kuendelea wanamume na wanawake na watoto ambao tunataka Taifa hili liwe zuri, watakuwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa kabisa, naiomba Wizara ikazanie maendeleo vijijini na sio mijini na sio mahali pengine popote bali vijiji ndio viwe *yardstick*, viwe ndio kipimo cha maendeleo ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie fursa hii kumpongeza Waziri, ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, pia na Naibu wake, Mheshimiwa Shamim Khan, ndugu yangu au dada yangu, mpenzi wangu, kwa sababu ameshafika kunitembelea mpaka nyumbani kwangu. Naamini kwamba, tuna upendo mkubwa mimi na ye ye lakini pia naomba nitumie nafasi hii, kuipongeza Wizara nzima kwa jinsi ilivyochambua bajeti

yake hii na kugusa nyanja zote na pia ikiwa na matumaini ndani ya kuwaendeleza Wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nataka nianze kuchangia kuhusu suala la vyuo vyetu vya *FTC*. Mimi nataka niipongeze Wizara kwa juhudhi yao kubwa sana walivyoviangalia vyuo vyetu hivi, wakaweza baadhi yake kuvifanyia ukarabati. Lakini nina masikitiko makubwa sana ukiangalia vyuo vyetu vingine kwa hali ilivyo havina hadhi hata ya kuitwa vyuo vya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi kwa kweli vinatuletea maendeleo makubwa kwa Wananchi wetu, lakini kutokana na hali ya vyuo hivi ilivyo, ukiangalia majengo yao yalivyo, ukiangalia ukosefu wa vitendea kazi, kwa kweli inasikitisha sana. Lakini hii yote nataka niungane na wenzangu, ni kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa kweli bajeti hii ya shilingi 4.9bn/= ni kidogo sana kwa Wizara yetu hii hasa tukizingatia majukumu makubwa waliyonayo. Mimi naomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma, kama walivyokwishazungumza wenzangu iwaongezee bajeti yao hii, vinginevyo tutawapa shida Mawaziri wetu. Tutasema tu Watendaji, Watendaji, lakini hali tu haiwaruhusu kufanya hivyo. Naomba tuitazame Wizara hii kwa jicho la huruma na ikiwezekana iongezewe bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nataka niongelee suala la ubakaji. Kwa kweli ubakaji unaongezeka katika nchi yetu kwa kiasi kikubwa sana. Tena inasikitisha kwamba, wale wanaofanya kitendo hiki si walevi wala si wendawazimu, ni watu ambao wana akili zao timamu na wana uwezo mkubwa tu waliojaliwa na Mwenyezi Mungu, lakini wao ndiyo mashetani wakubwa wanaolifanya suala hili.

Mimi nasema ingawa sheria zipo nyingi tu, lakini bado ningeiomba Wizara kusimama kidete kushirikiana na Taasisi mbalimbali hasa *TAMWA*, vinginevyo nchi yetu kwa kweli itakuwa imo ndani ya hatari.

Mheshimiwa Spika, nataka vilevile nzungumzie au niungane na wenzangu kuhusu suala la mikopo hii ya wanawake. Naipongeza Wizara kwa kulifikiria suala hili la mikopo ya wanawake. Kwa kweli Wizara inajitahidi kutoa mikopo ya wanawake, lakini inasikitisha kuhusu urejeshaji wa mikopo kwa wanawake. Naamini kama alivyozungumza mwenzangu hapa, si lengo la wanawake kuwa wasizirudishe fedha hizi lakini nasema labda ni ukosefu wa elimu. Kwa hiyo, naishauri Wizara kwamba, kabla ya kutoa mikopo hii kuwapa akinamama, nasema suala hili kwa sababu nimeshalitembelea vituo vingi tu na mimi mwenyewe ni Mbunge kwenye Kamati hii na nimeshaona kwa jicho langu kwani navitembelea vikundi vingi vya wanawake lakini bado havina uwezo wa kurudisha mikopo hii. Nashauri labda Wizara kabla ya kuitoa mikopo hii, basi itoe elimu ya kutosha pia iwape mbinu ya namna ya kutafuta mradi unaokidhi mahali walipo. Nashauri Wizara ifanye hivyo, ijitahidi kutoa elimu, kwa sababu wanawake hatuna tabia ya kupenda kudaiwa, lakini tena saa nyingine inabidi tu kuwa hivyo. Naiomba Wizara itoe elimu ya kutosha kwenye vikundi hivi vya wanawake.

Mheshimiwa Spika, nataka nifungue ukurasa wa kumi na mbili, pia ninukuu kidogo kwenye maendeleo ya jinsia. Mheshimiwa Waziri, kama alivyoelezea anasema: "Mheshimiwa Spika, maendeleo ya jinsia ni muhimu katika maendeleo ya jamii". Kwanza, hapo mimi nakubaliana naye. Kwa kuzingatia umuhimu huu sera ya maendeleo ya wanawake na jinsia, inahimiza uingizaji wa masuala na jinsia katika sera za sekta mbalimbali, mipango na miradi.

Mheshimiwa Spika, narudia pale pale, nakubaliana naye Mheshimiwa Waziri kwamba, maendeleo ya jinsia yana mipango mbalimbali ya miradi, lakini kweli miradi hii itafanywa vipi na tukitazama kwenye fedha za maendeleo kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi hapa ni Sh. 600m/= tu ambazo ni fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo. Hivi kweli Sh. 600m/= zitaiwezesha Wizara hii kufanya maendeleo gani? Mimi naona suala lipo pale pale, ningeiomba Wizara iongezewe bajeti yake, vinginevyo tutabaki kudumaa pale pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa sana kuhusu Halmashauri. Halmashauri kama alivyozungumza mwenyewe Waziri Mkuu hapa kwamba, kumetengwa asilimia kumi ya kuchangia kwenye Mfuko huu, lakini sijui kuna uzito gani, Halmashauri hizi mpaka hazitaki kutoa fedha hizo kuchangia Mfuko huu. Ningeiomba Serikali au Wizara itilie mkazo katika kuzifuatilia zile Halmashauri ambazo hazitaki kutoa asilimia hii ziweze kuchukuliwa hatua zinazofaa kwa sababu naamini kwamba, Halmashauri zina mapato mengi na si kwamba, hawawezi kweli kuchangia asilimia hii, kwani ni asilimia ndogo sana ukilinganisha na Halmashauri zetu zilivyo. Naomba Serikali iangalie Halmashauri zinazofanya ukorofu huu basi washikiliwe sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niende ukurasa wa 34. Hapa nataka niwapongeze Mawaziri wote wawili, kwa ushirikiano wao mkubwa walionao katika Wizara hizi mbili, Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto na Wizara hii. Nawashukuru sana Mawaziri wote wawili na nawaombea dua, Mwenyezi Mungu awape moyo huu huu wa kuendeleza ushirikiano wao ili tupate kufaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naona masuala yote wenzangu wameshanifilisi. Sasa baada ya hapo na hasa kwa vile mimi mwenyewe ni Mwanakamati wa Kamati hii na mapendekezo yetu tushayatoa kwenye Kamati yetu, basi naomba niishie hapa ili niwapishe na wenzangu waendelee na hoja hii. Lakini kabla ya hapo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri, ya kina na kwa kweli inaonyesha mwelekeo mzuri ingawa pengine kama walivyozungumza wenzangu, inawezekana utekelezaji ukawa mgumu kwa vile bajeti yenye ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Najua kwamba, mambo ya watoto yanashughulikiwa na Wizara nyingi hata Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo wanashughulikia suala hili, lakini kwa upande wa Wizara hii, ningependa nizungumze kwamba, jinsi mimi ninavyoliona na jinsi linavyoshughulikiwa, nilidhani kwamba, kitu muhimu sana katika kushughulikia hawa watoto wanaoishi katika mazingira magumu ni kufanya utafiti na kujua sababu zinazowafanya waishi katika mazingira magumu, kwa sababu mimi ninavyojaribu kulitazama naona kwamba, baadhi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu kweli zipo sababu za msingi zinazowafanya waishi hivyo.

Lakini wapo watoto wengine ambao wanapenda tu waishi hivyo na matatizo yao yanayowapeleka mitaani yanaweza kutatuliwa, lakini utakuta kwamba, sasa hivi zimezuka *NGOs* nyingi ambazo zinajitahidi kushughulikia hawa watoto. Nimewahi kuzungumza na baadhi yao kwamba, je, ninyi mnapogundua kwamba, pengine mtoto ana wazazi wake au ana jamaa zake, hata kama wazazi wake wamefariki, lakini ana jamaa zake kwa nini hamfanyi juhudhi ya kumwunganisha mtoto huyu na hao wazazi wake au walezi wake na kitu kikubwa pengine kingefanyika kwa kweli ni kujaribu kutatua matatizo yale yaliyomfanya mtoto aende kuishi katika mazingira magumu badala ya kuanzisha vituo vya kutunza watoto hao? Kwa sababu hao nilioongea nao wanasema, sasa wewe mama sisi unataka sisi tukale Polisi? Kwa sababu na wao wanaweza kuishi kwa kuhudumia hawa watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi sioni juhudhi yoyote ambayo inafanywa ili kurekebisha tabia za hawa watoto au pengine hata kurekebisha tabia za wazazi maana wengine wanasema wamekwenda mitaani kutokana na wazazi wao pengine kuwatesa au kutowahudumia. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana tuwe na mwelekeo mpya. Tujaribu kuhakikisha kwamba, hawa watoto tunawasaidia ili waweze kuungana na familia zao huko Vijijini walikotoka. Haya mambo ya *NGOs* na mimi nafikiria kuanzisha ya kwangu maana wanapata chochote siyo kusema kwamba wanahangaika na hawa watoto kwa huruma tu, lakini na wao wanapata kula yao hapo, ndiyo maana akaniambia kwamba, hawa watoto tukiwarejesha huko kwa wazazi wao, sisi tutakula Polisi? (*Kicheko*)

Kwa hiyo mimi nadhani kwamba, Wizara hii isipoangalia inaweza kukuta kwamba tunafanya tu mambo bila kuelewa na kumbe pengine matatizo tungewenza kuyatatua. Maana siku za nyuma kabla ya *NGOs*, mimi nilikuwa sioni watoto wanaozurura mitaani, lakini sasa wengi wanashawishika kwa sababu wanapokuja mitaani huku wanapata huduma. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba hilo suala liangaliwe kama itaonekana ni vyema kama mimi ninavyoliona, ili tulenge kutatua matatizo yaliyosababisha kuja mitaani badala ya kuwapa hifadhi kwa kuwatifikia vituo vya kuishi Mjini.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu utendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wizara hii kimuundo ilitakiwa iwe na mtandao wake mpaka chini kabisa kule kwa Wananchi, kwa sababu lengo na madhumuni ya idara hii au kazi za mtumishi wa idara hii ni kujaribu kuwatambulisha watu matatizo

yao, watambue matatizo yao na kuwapa mbinu za kuweza kuyatatu. Kwa hiyo, tulitarajia kwamba, wawepo watumishi wa kutosha huko Vijiji. Sasa ingewezekana angalau katika ngazi ya Kata akawepo mtumishi wa Idara hii ili kuweza kuwasaidia Wananchi kuelewa matatizo yao na kuweza kuandaa mipango ya kutatua matatizo hayo kwa sababu unaweza ukakuta Wananchi wanavyoishi huko Vijiji ukajiuliza kama kweli mtu anatambua tatizo lake. Maana mwingine unamkuta yupo kwenye kibanda ambacho kimebomoka, yaani unaweza ukaangalia, si dirisha lakini unaweza ukaangalia mpaka ndani.

Lakini kilichokosekana pale ni nini, kwa sababu udongo upo na yeye yupo, angeweza kukanyaga udongo akakandika kile kibanda chake kikawa kizuri? Kama hana uwezo wa kununua bati, basi akate nyasi aezeke kibanda chake, kiwe sawasawa. Sasa huyu mtu kwa kweli ni maskini wa kipato na ni maskini wa akili yaani wa kuelewa. Kwa hiyo, anahitaji mtu wa kumwelimisha.

Mheshimiwa Spika, sasa ukingalia mambo yote mazuri aliyotueleza Mheshimiwa Waziri, mimi nina wasiiasi kama yanafika kule Vijiji. Nina wasiiasi sana kama yanafika kule Vijiji kwa hali mimi ninavyoijua na ninavyoona kwa sababu wafanyakazi wa idara hii wapo chini ya Mkurugenzi katika Halmashauri za Wilaya na Miji. Kwa hiyo, uvezeshwaji wanaopata ili kuweza kutimiza majukumu yao ni mdogo mno au huduma wanayopewa ni ndogo mno. Kwa hiyo, unakuta kwamba, hawawezi kufanya kazi ambayo tulikuwa tunatarajia kwamba ingefanyika.

Mheshimiwa Spika, Sera hizi zinifikaje kule kama mtumishi huyu kwanza huko Kijiji hayupo, lakini hata pale alipo hana uwezo wa kufanya kazi kwa sababu hana nyenzo? Kwa hiyo, watumishi wengi wamepoteza *morale* ya kufanya kazi kwa sababu ya matatizo hayo ninayoyasema. Kwa mfano, utakuta sherehe za wanawake duniani zinafanyika Kitaifa. Lakini je, hawa wanawake wa Vijiji hawastahili nao wakaelewa ni kitu gani kinaendelea katika hizi sherehe au wao ni kina nani ili waweze kujielewa, wakajua ni nini au namna gani waweze kujikomboa? Kwa hiyo, utakuta kwamba, mambo ya Kitaifa yanaishia Kitaifa na huku chini kule Vijiji bado mambo yanaendelea kuzorota.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni kama walivyzungumza wenzangu, kwa kweli Halmashauri hazina muda na hivi vyuo kama ambavyo hazina muda wa kuchangia asilimia kumi kwenye Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana. Mimi niliongea na Mkurugenzi mmoja, akanionyesha karatasi, akasema katika mfumo wa uboreshaji wa Halmashauri, mambo ya vyuo sio kitu muhimu, yaani hayapo katika *priority*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, asifikiri kwamba, kuna chochote kinachofanyika kule. Nilikuwa nafikiri kwamba, Wizara na Serikali kwa ujumla, kama kweli hii Wizara inastahili kuwepo na kuweza kuonyesha ule uwepo wake, basi ijaribu kuliangalia na kutoa fedha za kutosha kwa kweli kuonyesha ile haki ya kuwepo, nadhani Serikali iangalie upya majukumu ya Wizara hii na namna ambavyo inapaswa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuandaa *master plan* ambayo imeshindikana, lakini huenda baadaye mbele ya safari

itafanikiwa, ingawa anasema miaka mitatu au kila baada ya miaka mitatu. Kwa hiyo na hii fedha ya *Basket Fund* ambayo anatarajia kupata basi igawiwe, zipewe Halmashauri ili watumishi wa idara hii na miradi mbalimbali na vyuo viweze kufanya kazi. Sisi tuliteuliwa kuwa Wajumbe wa Bodi za Vyuo lakini hakuna vikao. Mbunge unawenza kujitolea kwenda kwenye kikao bila posho na bila kugharamiwa usafiri, lakini wale Wajumbe wengine si rahisi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu kueleza kwamba, hali ya idara hii kwa kweli ni ngumu na ni mbaya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Waziri, ajaribu kwa sababu yeye ni *Doctor*, basi aweke mikakati zaidi na kuielimisha zaidi Serikali ielewe kwamba, kwa kweli idara sasa hivi *hai-justify its existence*.

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kukushukuru na kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofit*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Katika waliojiandikisha kuchangia hotuba ya Wizara hii, amebaki mmoja tu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, yeye atachangia kipindi cha mchana na baada yake watoa hoja watahimisha hoja yao. (*Makofit*)

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, lakini pia niwapongeze timu nzima ya wataalam ambao wamekuwa wakifanya kazi ndani ya Wizara hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme pia kwamba, kazi ya Wizara hii ni kubwa, lakini kwa upande mwingine mimi naweza kusema kwamba, Wizara hii inaonekana kama ni Wizara ya mtoto yatima. Kwa sababu mazingira yanayoizunguka Wizara hii ya mafungu kibajeti na kadhalika yanaonyesha kabisa kwamba, Wizara hii bado ina unyonge mkubwa sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niipongeze sana Idara yetu ya Maendeleo ya Jamii ndani ya Mkoa wa Ruvuma, kwa kweli pamoja na matatizo makubwa sana ya vitendea kazi na kadhalika, lakini tumekuwa tukishirikiana nao kwa kiasi kikubwa. Naomba kwa nafasi ya pekee, nimshukuru sana Afisa Maendeleo ya Jamii

wa Mkoa wetu, Ndugu Nyoni, kwa jinsi anavyojitolea akishirikiana na wenzake katika Wilaya kusaidia maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nampongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa mara ya kwanza leo Msemaji huyo amethibitisha ni namna gani Chama cha Mapinduzi, kupitia Jumuia ya Wanawake wa CCM, imekuwa makini katika suala zima la kuwakomboa wanawake katika nchi ya Tanzania. Kwa hiyo, ninampongeza sana dada yetu, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, kwa kulitambua hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuunga mkono Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na kuvihamasisha Vyama vyote vya Upinzani, vielewe umuhimu wa wanawake katika Vyama vyao, visiwanyanyase na visiwabague. Tunampongeza Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa UWT, kwa kuwa amekuwa kiongozi shupavu, akisaidia sana harakati za wanawake katika UWT. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaweza kusema kwamba, bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa mwaka huu ni bajeti yetu ya kupima mwelekeo na hasa miaka kumi baada ya Azimio la Beijing, ama baada ya maazimio yaliyofanyika huko Beijing.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni wakati wetu muafaka sasa kuangalia ni mambo gani ambayo tumefanikiwa na mambo gani ambayo hatujafanikiwa na nini hasa iwe ni jukumu la Wizara hii katika kuhakikisha kwamba, jamii ya Watanzania kweli inapata maendeleo yakinifu na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa za Shirika ambalo linajulikana kama *AMNET International*, mpaka leo hii wakati ninafanya shughuli zangu katika *Internet*, bado asilimia 60 ya wanawake katika dunia nzima wako katika ajira zisizo rasmi, asilimia 70 ndiyo wakulima na wazalishaji wakuu katika maeneo ya vijijini na ni asilimia kumi tu ya malipo ambayo yanaeleweka eleweka ndiyo wamekuwa wakilipwa wanawake, hizo ndiyo *data* ambazo mpaka sasa hivi ziko kiulmwengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ndiyo maana ninasema kwamba, bajeti ya mwaka huu iwe ni bajeti ya kupima. Tupime mwelekeo wa Wizara, tupime mwelekeo wa jamii yenyewe kimaendeleo na tupime mwelekeo wa Taifa nzima la Watanzania katika mwelekeo wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu kwa makusudi mazima, iliamua kubadilisha jina la Wizara hii na kuingiza dhana ya Jinsia ili kuleta ule usawa wa kijinsia katika kuleta maendeleo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninasema kwamba, katika miaka hiyo kumi ya mtafakari wetu wa Beijing, hali ya maendeleo ya wanawake ni kubwa sana na hasa Mijini lakini siyo Vijijini. Taarifa za ukombozi wa mwanamke zimefika kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya Mijini lakini Vijijini bado. Wanawake kuingia katika vyombo vya maamuzi tumepiga hatua kubwa lakini katika ngazi za juu na siyo zile za

chini ambazo ndizo wanawake wanapotakiwa waanze. Elimu kwa wanawake ni nzuri lakini bado elimu ya juu inaleta utata wa kumsaidia mwanamke ili kuendelea zaidi na kushika nafasi mbalimbali za uongozi. Sasa Mheshimiwa Waziri, alitambue hilo na aelewe kwamba, Wizara yake ina kazi na sidhani kama ni suala la kuachia Wizara ya Elimu na Utamaduni tu ama Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Wizara yake ina kazi ya kuoanisha usawa wa jinsia katika suala zima la elimu toka shule za msingi mpaka sekondari. Nilitegemea kukuta hiyo mikakati imeelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Mimi hayo ninayasema kama ni mafanikio lakini bado tuna matatizo mengi na makubwa ya kijinsia tukiachia mbali kwamba ni *concept* ya kumkomboa mwanamke kama mwanamke. Nimesema kwamba, wanawake wanajua wanatakiwa kukombolewa, lakini vijijini bado hawajui. Sasa Wizara inatuambia nini katika mkakati huo wa kuoanisha jinsia hizo zote mbili zikaelewa maana ya mahusiano bora ya jinsia na hivyo kuleta maendeleo ya jamii katika maeneo yetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonyesha wazi kabisa kwamba, ukombozi mwininge wa mwanamke ungekuwa kupitia katika mitaji, lakini mpaka sasa hivi Halmashauri nyingi hazitoi asilimia kumi ya mapato yake ili kuboresha mitaji ya wanawake katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara kusukuma suala hilo la kuongeza mitaji, lakini bado usimamizi umekuwa ni duni na bila kumsaidia mwanamke kimitaji bado hujamkomboa mwanamke na kumpa sauti ya kuweza kujimudu katika maisha yake ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hiyo hata kama ikitolewa bado hairejeshwi. Ina maana suala zima la elimu ya utumiaji wa mikopo hiyo ni duni mpaka sasa hivi. Sasa kama wanawake wa Mijini pia hawarejeshi mikopo ina maana vijiji itakuwa ni mbaya zaidi, kwa sababu bado hawana taarifa za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabenki mengi yamekuwa na masharti magumu ambayo hayawezi kuwasaidia wanawake kupata mikopo hiyo na kuweza kujipatia mitaji. Hizo ndiyo changamoto ambazo Wizara inatakiwa kuziangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria nyingi bado hazimsaidii mwanamke kujitambua yuko wapi na anafanya nini na anatakiwa apate nini katika jamii. Uelewe wa mahusiano ya kijinsia kati ya wanaume na wanawake bado kabisa uko katika hatua ya chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa unyanyasaji wa kijinsia bado upo wa hali ya juu, kwa maana hiyo, dhana ile ya Wizara hii kubeba jukumu la mahusiano ya kijinsia inatakiwa ifanyiwe mkakati wa ziada ili jamii ielevwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upatikanaji wa taarifa zinazohusu wanawake na maendeleo ya jamii kijinsia bado ni duni sana katika maeneo mengi ya nchi yetu ya Tanzania. Wanawake bado wanakabiliwa na mazingira magumu ya usafiri vijijini, wanasafiri kwa muda mrefu kwa miguu wakibeba mizigo mizito sana kutoka mashambani, wakitumia teknolojia hafifu sana katika kulima na kuzalisha mazao

mbalimbali na hakuna viwanda vya kusindika mazao yao. Kwa hiyo, hizo zote ni changamoto za maendeleo ya jamii katika maeneo mbalimbali. Nilikuwa nategemea sana sasa hiyo iwe ndiyo mikakati ya Wizara kushirikisha Wizara nyingine na kuona namna gani tunaweza kujikwamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nafikiri kwamba, pamoja na kuanzisha hiyo mitandao mbalimbali itakayosaidia maendeleo ya jamii kwa jumla, katika maeneo mengi ya vijiji na katika Miji midogo yamekuwa bado na matatizo ya umeme. Kwa hiyo, tatizo la upatikanaji wa taarifa hizi utabaki katika maeneo makubwa tu ya Mijini. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani Mheshimiwa Waziri, anatakiwa kuwa na changamoto ya ziada ya kuhakikisha kwamba, mambo hayo yanawafikia wanawake na jamii yote kwa ujumla ili kuweka usawa huo wa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini sasa nafikiri iwe ni mikakati yetu ya kuhakikisha kwamba, tunaendelea mbele na siyo kurudi nyuma. Benki ya Wanawake ianzishwe haraka sana. Imekuwa historia ya muda mrefu toka Bunge hili lilipoanza tumekuwa tukiendelea kusikia Benki ya Wanawake, Benki ya Wanawake, lakini ni wakati muafaka Benki hiyo sasa ianze. Lakini mimi nilikuwa nafikiri kwamba, mikakati shirikishi ya kuwawezesha wanajamii kuingia katika maendeleo ya kijinsia iangaliwe upya na Wizara hii. Kwa mfano, tumekuwa na uanzishaji wa *SACCOS* nyingi za wanawake na za mchanganyiko, lakini Wizara haituambii namna gani *ita-support SACCOS* hizo ili ziweze kujimudu na kuendeleza maendeleo katika jamii yetu. Nadhani kwamba, Mheshimiwa Waziri aangalie kama kuna matatizo katika urejeshaji wa fedha zinazotolewa kupitia kwenye Halmashauri, apeleke fedha hizo zikae kama ni mitaji ya Vyama vya Akiba na Mikopo ambavyo tayari Wananchi wameshajijengea tabia ya kuweka na kukopa na hivyo kuwa waaminifu katika kurejesha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ili kuweza kufanikisha hayo, nadhani Wizara hii ipatiwe fedha za kutosha. Nilikuwa napitia kitabu cha bajeti cha mwaka 2002/2003, ukurasa wa kumi na kitabu hiki cha mwaka huu ukurasa nane, kuna Mpango wa kupeleka teknolojia rahisi katika vijiji, lakini Wizara mwaka 2002/2003 ilisema kwamba, ingetengeneza vijarida na kuvisambaza na mwaka huu itaendelea kutengeneza vijarida na kuvisambaza. Sasa nadhani Wizara inafanya hivi kwa sababu haina fedha za kutosha ama sijui kama kuna sababu nyingine tofauti. Mimi nadhani hakuna umuhimu toka mwaka 2002 mpaka mwaka huu 2004 tunafanya kazi ya kutengeneza vijarida na kuvisambaza. Kwa nini fedha hiyo ya kuvitengeneza sasa isingepelekwa katika kutengeneza bidhaa na zana rahisi za kufanya kazi katika maeneo yetu na hasa huko vijijini? Nafikiri hii ni kutokana na uhaba wa fedha, kwa hiyo, Wizara inashindwa kupanga mambo yake vizuri na kufanya kazi zake sawasawa na inajikuta inaishia katika matengenezo hayo ya vijarida na hivyobasi kuendelea kuvisambaza vijarida na kuwafundisha wataalam na siyo kuingia katika vitendo halisi vya kuongeza zana bora katika maeneo mbalimbali ya nchi ya Tanzania ili kuongeza maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tumeambiwa kabisa kwamba kuna vikosi vya ujenzi ambavyo vitapewa kipaumbele. Ukisoma taarifa ya mwaka 2003 ni sawasawa haina tofauti na taarifa hii ya mwaka 2004. Sasa mimi nasema kwamba, hebu

tuhame kutoka katika hayo maelekeo ambayo tulikuwa tumeyafanya toka nyuma tuingie katika utendaji halisi ili kweli kusimama na kuona tunaletaje maendeleo ya wanajamii wa nchi yetu hii ya Tanzania. Nadhani kuboresha Madawati ya Jinsia kututasaaidia sana. Lakini ni budi tutambue madawati hayo na Maofisa wa madawati hayo watakuwa wa wajibu gani na wanaelewa kwa kiasi gani namna nzima ya maendeleo ya jamii ya Watanzania na hasa katika suala zima la uwezeshaji jamii kutokana na tatizo kubwa la umaskini. (*Makofi*)

Namshauri Mheshimiwa Waziri, aone ni mkakati na changamoto ya pekee Wizara inayobeba, maendeleo ya jamii ichukue jukumu la kwanza la kuisaidia jamii kupambana na umaskini ama kwa kushirikiana na Wizara nyengine ama kwa kuwa na mikakati sasa shirikishi ya kiutendaji ambayo itabadi maisha ya Watanzania kutoka katika hali ya uduni kuja katika hali bora. Lakini ninaendelea kusema kwamba, Wizara sasa ipewe fedha za kutosha ili iweze kufanya kazi inayotakiwa na inayofanana hasa hasa na jina lenyewe la Wizara la kuleta maendeleo ya jamii. Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Maafisa Maendeleo ya Jamii, hatuna katika nchi ya Tanzania ni wachache sana na vitindea kazi vyao ni duni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE EDWARD N. NDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa upeo, kina na maudhi yake, naomba Wizara itafakari kwa kina zaidi agizo lake la kuanzishwa kwa Dawati la Jinsia katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni na ushauri wangu, Dawati linalostahili kuanzishwa katika kila sekta ni Dawati la Maendeleo ya Jamii kwa hoja zifuatazo: Kwanza, kila sekta inapashwa ielekeze mipango yake katika kurekebisha matendo/maamuzi yanayoibadilisha jamii kwa manufaa na maendeleo yake. Mfano, Sekta ya Ujenzi, kuelekeza barabara vijijini kwenye uzalishaji, kutabadilisha utaratibu na mfumo wa kulima kutokana na kuongezeka kwa mwingiliano wa jamii na kubadilishana uzoefu katika kilimo na Sekta ya Elimu, kuelekeza ujenzi endelevu wa shule bora vijinini kuanzia shule za awali, jamii itabadi lika katika mtazamo, maamuzi na matendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuelekea au kuzingatia kwamba, matendo ya jamii ndiyo kipimo sahihi cha maendeleo ya jamii husika, Dawati Muafaka katika sekta ni vyema likatambulika kama Dawati la Maendeleo ya Jamii. Nachelea kufikiria kwamba, kuliita Dawati la Jinsia, kunaweza kuamsha hisia ya kwamba, Dawati hilo ni fursa nyengine ya chanzo cha mjadala wa usawa wa jinsia na suala la maendeleo lisipewe msukumo. Elimu ya uwiano wa jinsia katika utekelezaji, uendeshwe na Wizara. Dawati liwe chombo cha kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maendeleo ya jamii yanayotekelizwa na sekta ilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo ni ushauri kwa Wizara hii ambayo ni Wizara mtambuka, ni kubainisha wazi katika sera na mipango yake, mkakati wa kubadilisha rasilimali mfu kuwa hai (*transformation of dead capital into live capital - Hernando Do Soto Initiative*). Itakumbukwa katika hili, Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliagiza kila Wizara iandae mkakati wa utekelezaji. Kwa bahati mbaya, hilo halikubainishwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuunganisha hoja hii ya pili na ile ya kwanza, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, itakuwa na fursa nzuri ya kupenyeza mikakati yake ya kufufua rasilimali mfu, ambazo zimesheheni ndani ya sekta isiyo rasmi vijijini, katika sekta mbalimbali kuitia Dawati la Maendeleo ya Jamii litakalokuwa limeanzishwa katika kila sekta. Pamoja na maoni hayo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu nzima ya Wataalam wa Wizara hii, kwa kuandaa hotuba na bajeti yenye matumaini. Naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 niliongea na Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuhusu matatizo yaliyopo katika Chuo cha Maendeleo Singa Kibosho Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo makubwa ambayo Mheshimiwa Waziri aliahidi kusaidia, ni juu ya maji chuoni hapo. Chuo hicho zamani kiliitwa *Msinga Farmers Training Centre* na wakati huo kilikuwa na mabomba ya maji pamoja na mali nyingine ambazo hazipo hivi sasa. Mimi sina mpango wa hizo mali nyingine zilizopotea, ila ni juu ya maji ambayo ili kukarabati au kujenga maeneo ambayo mabomba yaliibiwa au kuharibika, zinahitajika Sh. 8,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kwenye chuo hicho lilikuwa ni ukarabati wa majengo, jambo ambalo kwa kiasi fulani limefanikiwa. Tatizo lingine lilikuwa upatikanaji wa wanafunzi, jambo ambalo pia limetatuliwa, kwani wanafunzi ni wengi sana na kazi ni nzuri. Nampongeza Mkurugenzi aliyepo sasa, kwani anachapa kazi sana.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kumwomba Waziri juu ya maji ya bomba, ambayo awali yalikuwepo, kutenga walau Sh. 8m./= tu, nyingine nitaongea na Halmashauri yangu ili tujazie. Ahsante.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim P. Khan, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii nzuri, yenye mwelekeo wa kuinua hali ya akina mama na watoto kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nirudie kuwapongeza zaidi na zaidi Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa jinsi wanavyoindesha Wizara kwa mshikamano wa hali ya juu. Hali hii imekuwa mfano wa kuigwa na Wizara nyingine. Ni imani yangu kubwa kwamba, kwa mshikamano wao, ndiyo uliowawezesha Wizara hii

kuwa na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yao. Nawaombea Mungu, awazidishie kila lililo jema katika majukumu yao mazito kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitakuwa mchoyo wa fadhila kwa Serikali, jinsi inavyojitahidi kuchangia mfuko wa wanawake na vijana kwa Halmashauri zote nchini. Mchango huu umezidi kuongeza nguvu ya mfuko huu kwa lengo la kusaidia akina mama wanaojitahidi kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kwamba, Halmashauri nyingi zimeshindwa kuunga mkono juhudzi za Wizara hii za kuchangia mfuko wa wanawake, hali ambayo inachelewesha kuwapa nguvu wanawake katika kuondokana na umaskini. Naomba kauli ya Serikali katika udhaifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nishukuru kwa kuwa kila Halmashauri ina Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kwa kuwa Maafisa hawa walishasoma miaka mingi iliyopita, naiomba Serikali iwape kozi, semina na warsha mbalimbali ili kuboresha taaluma zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwakopesha akina mama fedha za kuendesha miradi yao. Tatizo ni kwamba, Serikali inasahau kutoa semina kwa akina mama, za namna ya kuendesha miradi, kubuni miradi na kuweka kumbukumbu za pesa kiasi kwamba, wanawake wanashindwa kurejesha mikopo. Kwa kuwa Wizara hii ni ya Wanawake, naomba jukumu hili lihamishiwe kwao badala ya kuwa chini ya TAMISEMI, ambao Wakurugenzi hawaoni umuhimu wa jukumu hili, kwani hawana uchungu na akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niipongeze Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kuvipatia Vyuo vya Maendeleo, fedha kwa ajili ya kukarabati majengo na kununua asasi za kuendeshea mafunzo katika vyuo hivyo. Mfano, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (*FDC*) Singida Mjini na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Msingi Wilayani Iramba. Kwa kweli vyuo hivyo sasa hivi vinavutia sana, hata utoaji wa taaluma umeboreka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara hii, kupeleka asasi zaidi mfano kompyuta, vyerehani, *photocopy machines*, vifaa vya ujenzi, vifaa vya useremala na kuboresha miundombinu, ili viweze kuendana na karne ya Sayansi na Teknolojia ya sasa. Kwa hiyo, kwa bajeti ya mwaka huu, naomba kipaumbele kwa Vyuo vyangu vya Maendeleo Mkoani Singida, mimi kama Mjumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Benki ya Wanawake, ambayo itakuwa ukombozi kwa akina mama ambao wamefunguka macho katika suala zima la uzalishaji mali, sambamba na akina baba. Naomba mikakati hii iongeze kasi kwa kila mkoa, ukiwemo Mkoa wa Singida ambao nao una wanawake wengi wenye kiu ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kuwakutanisha akina mama wote wenye bidhaa katika Sherehe za Sabasaba Kitaifa huko

Dar es Salaam, katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere. Hali ambayo inawasaidia sana akina mama kupata soko la bidhaa zao.

Mhesahimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kwamba, kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko la Wananchi, wakiwemo akina mama, ione umuhimu wa kujenga uwanja mwingine utakaotosheleza ongezeko hilo, kwani msongamano wa watu sasa hivi umekuwa mkubwa sana.

Mhesahimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru Mama Anna Mkapa, kwa jinsi anavyojitahidi kuwafadhili akina mama kutoka mikoani kushiriki katika Maonyesho ya Sabasaba Kitaifa, tukiwemo Waheshimiwa Wabunge Wanawake. Ninaomba shukrani hizi zimfikie na Mungu ambariki sana.

Mhesahimiwa Naibu Spika, sasa nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. HALIMA O. KIMBAU: Mhesahimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mhesahimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri ilioletwa mbele ya Bunge hili. Hivyo basi, napenda kwa kuanza kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mhesahimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa Mhesahimiwa Waziri, kwa kuweza kuwaongezea ujuzi mafundi 30 wa Vikosi vya Ujenzi. Shukrani maalum kwa kutoa mafunzo haya kwa wataalam wetu kutoka Kibaha, Bagamoyo, Kisarawe na Mafia. Natoa shukrani maalum kwani mara nyingi Wilaya ya Mafia huwa tunasahauliwa. Nashukuru sana.

Sasa jinsi gani tutawawezesha kutumia utaalam walioupata katika kusaidia maendeleo ya Wilaya zao, ni suala muhimu sana. Sina hakika kama kweli tunawatumia ipasavyo.

Mhesahimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Mhesahimiwa Waziri katika kumshukuru Mama Anna Mkapa, kwa jinsi anavyowasaidia wanawake kuititia mfuko wa *EOTP*. Mimi nimeshuhudia hatua waliyopiga akina mama. Nikiwa mmoja kati ya waliohudhuria maonyesho ya Biashara mwaka huu kwa mwaliko wa Mama Anna Mkapa, ambaye tunamshukuru kwa moyo wake wa kutukaribisha Wabunge Wanawake.

Mhesahimiwa Naibu Spika, nikifananisha mwaka 2003 na mwaka huu wa 2004, ni wazi kuwa hatua kubwa imepigwa na akina mama. Vifaa vyao ni bora zaidi na aina mpya ya vifaa vimeonekana. Tumeona jinsi gani akina mama wameweza kutumia hifadhi ya mazingira katika kujikwamua kiuchumi, utumiaji wa magugu maji kutengeneza fanicha, ni ushindi wa jambo hili. Jambo hili limeweza kuua ndege zaidi ya wawili. Kwanza, limeweza kupunguza magugu maji, limetoa ajira kwa vijana na wanawake. Lakini pia kutoa vifaa ambavyo wengi wetu tungeweza kutumia majumbani.

Mhesahimiwa Naibu Spika, kitu kingine kilichonivutia ni kuona mishumaa ya harufu mbalimbali na hata mishumaa inayotumika kwa kuua mbu. Mafuta ya mibono,

ambayo yanaweza kuwashia taa, pia imeweza kuonekana. Ushindi wa wanawake waliochukua wanawake wa Tanzania huko kwenye mashindano ya Nchi za Nje, haya yote ni mafanikio makubwa. Nawapongeza sana wote. Pamoja na kuwa jambo hili tunalirudia mara kwa mara, usichoke kusikia. Mfuko wa *WDF*, bado nia ya Serikali ni nzuri, lakini wenzetu wa Halmashauri hawatusaidii nya kutosha. Halmashauri nyingi zina madeni. Haya sasa ni madeni sugu. Mimi nashauri kwamba, tuishauri Serikali Kuu itoe fungu maalum kuwalipia Halmashauri hizo na wao wawe na mpango maalum wa kupata fedha hizo na kuanzia hapo, tuone jinsi gani Wizara husika na Mabaraza ya Madiwani wataandaa utaratibu bora zaidi wa kupata asilimia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa kuiomba Serikali ione umuhimu wa kuongeza fungu la maendeleo la Wizara hii, kwani ni dogo mno. Wizara hii ina majukumu mazito, lakini fedha ni kidogo. Sijui ni kwa nini. Najua mengi yamechangiwa na wenzangu, lakini bado tuna kazi kubwa ya kusaidia Wizara hii, kama kweli nia yetu ni kuwakomboa wanawake na watoto. Hatua tuliyofikia si ndogo, lakini haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote walio ndani ya Wizara. Tutaendelea kuwapa ushirikiano wakati wowote watakapotaka ushirikiano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia machache katika Hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kama ifuatavyo:-

Kwanza, naiona Wizara ina majukumu mazito, lakini haipewi fedha za kutosha. Bajeti ya Wizara hii haitoi taswira ya kazi halisi inayopaswa kufanyika. Mfano, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa, lakini vimeachwa vimeharibika hata havifanani kabisa na mahali pa mtu kupatia elimu/mafunzo kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisemee Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rubondo, Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera. Chuo hicho cha Rubondo, kinatisha na hakifanani na vyuo vingine, majengo ni machakavu, tena ya kizamani sana na hakivutii hata watu kupenda kusomea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Serikali imetoa kipaumbele kwa Shule za Msingi kuititia MMEM, basi Serikali ione njia muafaka ya kujenga upya na kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Bajeti yake ni ndogo mno.

La pili, ninalowapongeza na kuwaomba waongeze bidii ni Benki za Wanawake. Wanawake wameanza na *SACCOS*, ambapo wengi wameanza kuelewa na wanajiunga na *SACCOS*. Nashauri mtazamo uwe ni wa Benki ambayo wenye uwezo mkubwa wakope kwa wingi na wenye biashara na shughuli ndogo ndogo wajifunze kwa kukuza mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha kidogo wanazopatiwa wanawake zina mchango kidogo sana, kama upo kwa maendeleo ya kweli ya mwanamke anayetaka kujikwamua kimaendeleo na kujisajili katika kundi la wapambanaji wa kweli wa adui umaskini. Wanawake ni wachangiaji wakubwa katika uchumi wetu, lakini bila mitaji wataendelea hivi hivi na mitaji isiyokua na hivyo hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan na Watendaji wote katika Wizara hii, kwa jinsi wanavyoweza kufanya kazi pamoja. Mungu awaties nguvu na kazi yao ipate mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahia sana hotuba nzuri yenye vielelezo fasaha na jinsi aliyowasilisha Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro mbele ya Bunge letu Tukufu na hivyo, nampongeza sana pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim P. Khan, kwa ubora wa hotuba hii, naunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika sina cha kukosoa katika hotuba hii kwa sababu mambo mengi nilikwisha changia katika bajeti za huko nyuma. Mheshimiwa Waziri ameyaweka sawa, namshukuru sana na Watendaji wote Wizarani, Mikoani na Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba safari hii kwa Mheshimiwa Waziri, ni juu ya watumishi wanaokaribia kustaafu wakiwa na vyeo vya chini. Watumishi hao wapandishwe vyeo hata mwaka mmoja kabla ya kustaafu ili wapate mafao ya kustaafu, yenye unono kuliko ilivyo sasa au kipindi nilichostaafu mimi Mheshimiwa Asha Stima mwaka 1996. Nilipata mafao madogo kutokana na kutofikiriwa vyeo vya juu, ingawa tulistahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kuwa naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara yake, kwa kazi nzuri na ya kusifiwa wanayoifanya kwa Taifa hili. Naunga mkono yote waliyoyafanya, pia naunga mkono hoja ya Wizara yake mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri tu kwamba, katika kutekeleza majukumu yao mwaka wa fedha 2004/2005, wakumbuke ya kwamba, Chuo cha Maendeleo Msingi, kilichopo Iramba Mashariki, kinakabiliwa na matatizo mengi ya uendeshaji kama vile uchakavu wa majengo, ukosefu wa usafiri (gari), mashine ya kuvuta maji, ukosefu wa umeme na ukosefu wa fedha za kutosha za uendeshaji. Haya yote niliyoyaandika hapo juu, yanakwamisha maendeleo ya chuo chetu. Karibu miaka mine iliyopita, Mheshimiwa Waziri amekuwa ananiahidi kunipatia gari kwa ajili ya matumizi ya chuo hiki, lakini mpaka leo bado. Chuo hiki kipo mbali na maeneo ambako usafiri unapatikana. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na usafiri wa kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishaomba umeme toka Wizara ya Nishati na Madini juu ya kutoa umeme Kinampanda (km. 4) ufile chuoni. Wizara ilisema gharama yake ni Sh. 83.0m./=. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu wake na Watendaji, tuendelee kuwakumbusha wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini, wapeleke umeme Chuo cha Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuwapongea Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kazi nzuri wanayoifanya.

MHE. SAMUEL M. CHITALILO: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na Wataalam wa Wizara yake. Hotuba hii haina kasoro yoyote, ni nzuri na iko wazi. Na kwa mara ya kwanza nimeona hotuba yake ndio inaanza kwa kuwashukuru na kuwapongea viongozi wetu wa juu, yaani Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa na busara ya Mheshimiwa Waziri. Ningekuwa peke yangu ndiyo naweza kupitisha bajeti katika Wizara yake, ningesubiri akimaliza kusoma hapo, ningesimama na kusema kuwa hotuba yake inaungwa mkono kwa asilimia zote bila hata majadiliano. Lakini kwa kuwa ni mambo ya watu wengi, sawa itajadiliwa. Lakini ukweli ni kwamba, hotuba haina tatizo lolote, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo. Nawatakia Wizarani kwao kazi njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali walio chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yenewe inatafsiri sahihi, jinsi gani ilivyowekwa na ndiyo hivyo hivyo inavyoonekana umuhimu wake. Ni Wizara iliyomgusa kila mmoja katika jamii hii kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kauli inayosema kuwa kumwelisha mama (mwanamke) ni kuielimisha familia, lakini kuwaelimisha wanawake ni kuelimisha Taifa. Usemi huu ni sahihi na wala hauna walakini. Zaidi ya hilo, akina mama ndio mhimili mkubwa wa maendeleo ya kila Taifa, si Tanzania tu, bali hata dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha dhamira ya ulezi na uzazi kwa jamii, akina mama hao ndio wanaotupiwa familia za ama za mababa wanaojulikana na hata na za wale wasiojulikana. Jukumu hilo huwa ni lao. Kama hiyo haitoshi, ni wao wanaachiwa wagonjwa au walemovu wakati wa raha, shida na hata nyakati za vita. Ndio wao wabebao mzigo mkubwa. Hapana shaka haya yote yanaeleweka na kwa mtazamo wa

haraka haraka, Wizara hii ndiyo ina majukumu na ufuatiliaji wa karibu zaidi wa akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa ukaribu zaidi na Wizara kama hii ya Zanzibar, bila ya kujali kama suala hili ni la Ki-Muungano au laa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza vilevile Mheshimiwa Waziri na Watendaji Wakuu wa Wizara hii kwa azma yao ya kuanzisha chombo cha wanawake (Benki ya Wanawake). Ningeshauri tu kwamba, Benki hii iwe na mtazamo au mtandao wa Kitanzania, namaanisha ingelikuwa vizuri vilevile ikawa na tawi lake Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kwa bajeti zijazo, Wizara hii iongezewe fedha, kwani fedha walizopewa za chini ya Sh. 5bn./= ni kidogo mno, ukilinganisha na majukumu waliyogawiwa na kazi nyeti wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa taarifa yenu nzuri, yenye madhumuni ya kuinua jamii ya Watanzania. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa na juhudi za hali ya juu kwa kuruhusu Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi kutoa cheti. Ni changamoto kwa wanafunzi wanaosoma hapo, kutambulika baada ya kumaliza. Ombi langu kwa Wizara ni kutilia mkazo chuo hiki ambacho ni mkombozi kwa jamii ya Tanzania. Uboreshaji wa majengo, yaani Ofisi, mabweni na nyumba za Walimu, naomba ziboreshw, vitendea kazi kama magari yaliyopo yatengenezwe na ni vyema wakapatiwa usafiri mwingine, vilevile *OC* iongezwe kukidhi matumizi ya Ofisi na mishahara ya Watumishi iboreshw, kazi yao ni ngumu. Nina imani na Wizara hii, hivyo, nawaomba sana wakilie maanani Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi. Siyo siri, Wizara inafanya kazi kwa uwazi. Ni vyema nikaruhusu ombi lenu la Sh. 4,989,293,400/= mpewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza sana Wizara hii, kwa kazi nzuri inayofanya kuhamasisha uelewa mzuri wa wajibu na majukumu ya jamii ya jinsia zote, hivyo, naiunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda kuchangia machache yafuatayo: Wizara hizi mbili za Wanajamii Bara na Visiwani, wazidi kuboresha huduma zao

ziwafikie walengwa katika Majimbo na Tarafa/Wadi kwa kushirikiana na Wabunge/Wawakilishi na Madiwani waliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Wizara hizi kwa kushirikiana na wengine, wadhibiti elimu mbovu na vipindi ambavyo vinaharibu maadili na utamaduni wa jamii yetu kupitia Televisheni na Cinema, *videos* na kadhalika. Inasikitisha kuona kuwa baadhi ya vipindi vinavyoonyeshwa na vyombo vyetu vya habari na hata magazeti yanapotosha zaidi maadili kuliko kuelimisha na/au kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya vipindi vya *TV* vinavyoonyeshwa wakati watu wapo makazini, ambavyo vinawaharibu kabisa vijana wetu. Hivyo, sote tuwe macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nazidi kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri. Ahsante.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia maeneo yafuatayo: Kwanza, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwanza, napenda kuipongeza Wizara kwa kukipatia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chisalu, Wilayani Mpwapwa, Sh. 14,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizo, naomba Mheshimiwa Waziri, atembelee chuo hicho ili kuona maendeleo ya chuo. Pia naomba chuo hicho kipatiwe Walimu wa kutosha wa fani mbalimbali, fedha za matengenezo ya *tractor* na gari. Chuo hicho kina eneo kubwa la shamba, bila *tractor* watashindwa kulima shamba hilo. Shamba likilimwa lote, chuo hujitosheleza kwa chakula. Chuo kipatiwe huduma ya simu ili kuboresha mawasiliano, pia kuboresha huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chisalu, Wilayani Mpwapwa, kuna eneo kubwa na majengo ya kutosha, je, Serikali ina mpango gani wa kukibadilisha chuo hicho na kukifanya kiwe Chuo cha Maendeleo ya Jamii, ili wafundishwe Maafisa Maendeleo Wasaidizi (vyeti) na baadaye *Diploma*? Hii itasaidia kuongeza idadi ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, ambavyo ni vichache hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii Wasaidizi waliopo vijijini wapewe mafunzo ya mara kwa mara ili kuongeza taaluma yao. Pia wapatiwe vitendea kazi kama vile magari Wilayani, pikipiki, balskeli na kadhalika ili kurahisisha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanawake wengi hawana kipato cha kutosha, ipo haja kubwa ya Serikali kuongeza fedha za mikopo ili wanawake waanzishe miradi midogo midogo itakayosaidia kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote, kwa kazi nzuri wanayofanya. Nirudie tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa kukipatia Chuo cha Chisalu Sh. 14m./= kwa ajili ya ukarabati. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, kwa lengo la kuboresha, napenda nichangie maeneo yafuatayo: Mikopo kwa wanawake na vijana, inayotolewa na Halmashauri, asilimia kumi siyo tu hairudishwi wakati muafaka, bali wanaokopeshwa ni wale waliokuwa karibu na chungu na hawa wako mijini na siyo vijijini. Mikopo badala ya kuwafikia wale wenye shida, inakwenda kwa wenye fedha. Nashauri fedha hizo zipitie Benki au *SACCOS* ili kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha kwa wanawake na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya watumishi hasa wale walioajiriwa ili kutoa mafunzo ya ustadi, hususan umeme, ufundi magari, ufundi mchundo, ushonaji na kadhalika, kwanza mishahara yao ni ya chini ukilinganisha na mtaalam kama huyo na mwenzake ambaye amejiriwa na Wizara ya Ujenzi. Hali hii itasababisha wataalam hao kuihama Wizara. Tayari baadhi ya watumishi hao wangependa muundo wa vyuo hivyo uwe kama ule wa *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mbanga, haifai kabisa. Majengo yanahitaji ukarabati mkubwa. Chuo hakina vifaa vya kutosha vya kufundishia. Naomba Wizara ichukue hatua ili majengo haya yasibomoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namshukuru Katibu wa Wizara, Bi Hilda Gondwe, kwa kutembelea Wilaya ya Mbanga. Namkaribisha Mheshimiwa Waziri atembelee Wilaya ya Mbanga.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wao wote, kwa kuweza kuwasilisha hotuba yao hii mbele yetu, ambayo inasisimua na inaonyesha ina madhumuni ya kazi nzuri ambayo Wizara imekusudia kwa dhati kuelimisha na kuondoa matatizo yaliyomo ndani ya jamii zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wengi wamo ndani ya mitaa yetu, wanazurura bila ya kujua la kufanya kutokana na kukosa wazazi wa kuwashughulikia. Lakini siyo kweli kuwa watoto hao hawana wazazi, kwani wengi kati yao siyo wale waliofiwa na wazazi wao kwa maradhi ya UKIMWI. Wengi wao ni wale ambao wametelekezwa tu na wazazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Serikali kwa kupitia Serikali za Mitaa, kuwa na uangalifu zaidi ndani ya kaya moja hadi nyingine, ili kuwe na taarifa za watu walio wajawazito na muda wao wa kujifungua na kuelewa ujauzito huo ameupata kwenye ndoa au nje ya ndoa. Hiyo itatusaidia kumwelewa Baba wa Mtoto na Mama wa Mtoto. Hapo ndipo tutakuwa na chanzo cha kuhoji upotevu huu wa watoto na kuzidi kuenea mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wengi waliochukua mikopo walikawia kupata elimu na kufikiria hiyo ilikuwa ni sadaka tu kutoka Serikalini, ndiyo ukaona marejesho yanakuwa magumu. Kwa hiyo, ningeliishauri Wizara ifanye mapitio kwa wale wote waliopata mikopo, kama ni midogo tu mpaka Sh. 30,000/=, Serikali iwasamehe ili waweze kuishi kwa salama ndani ya maeneo yao. Kama ni zaidi ya hapo, basi watafutiwe njia ambayo si ya bughudha, ili waweze kulipa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningelimwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa ni mtendaji mzuri, aendelee kushirikiana na Waziri mwensiwe wa Wizara kama hiyo iliyoko Zanzibar, Mheshimiwa Samia Suluhi, ili waweze kushirikiana kwa hali ya juu katika kufanikisha ufanisi ulio bora, kwani Wizara hizi zina nia moja ya kuwaendeleza Watanzania wote waondokane na unyonge wa kipato na kujihisi wao ni mionganoni mwa Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara hii. Kila kukicha, Wabunge tunashuhudia mabadiliko ya msingi ya nchi hii katika kuendeleza jamii. Hongera sana. Haya matokeo yanatokana na juhudzi za Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *DAP* na Viongozi wote wa hapo Wizarani. Shukrani, Taifa hili linawategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la leo, mpenzi wako binadamu duniani, hata akiwa wa mwisho kumpenda, siyo adui wa mwisho kumchukia. Upendo na uadui, ni vitu tofauti. Hivyo, hupangwa safu mbalimbali. Ndiyo maana adui yako hapangwi kuwa na nafasi ya mpenzi wa mwisho katika orodha ya watu uwapendao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo, nimesoma jedwali la urejeshaji wa mikopo, hongera kwa takwimu hizi, lakini ninaomba sana mfuatilie, huenda vikundi vimeshalipa, lakini fedha zinakwamishwa na Maafisa kadhaa Wilayani. Hima/Shime Wizara ifuatilie kwa karibu sana suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayapongeza Mashirika ambayo ni Mabenki wala siyo ya Kiserikali, yanayokopesha wanawake nchini, lakini riba zichunguzwe, ni kubwa mno. Kwa mfano, mwanamke akikopa Sh. 100,000/= hutakiwa kulipa kati ya Sh. 25,000/= hadi Sh. 30,000/= kwa mwezi kwa miezi sita, sawasawa na kurudidha Sh. 180,000=/. Riba ni asilimia 80. Hii hali, umaskini hauondoki. Naomba muwahoji wanawake wanaokopa kwenye Mashirika hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna udhalilishaji wa watoto nchini kwa kuwafanyisha kazi ngumu, kubakwa na kufanyiwa matendo ya kinyama. Wizara ishirikiane na Polisi kuchunguza maeneo ya *Coco Beach*, jinsi watoto wanavyofanyiwa. Nilifuatilia *Radio Clouds* juu ya mtoto mmoja, naishia hapo, fuatilieni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita ya ukombozi wa wanawake, hii ni vita yetu wote. Naomba tushirikiane, isionekane kama ni vita ya wanawake peke yao. Tuungane twende bega kwa bega, siyo ana kwa ana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Madiwani Wanawake warudishwe haraka sana kwenye Kamati ya Mgao wa Mikopo Wilayani.

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo Tango ni Chuo pekee katika Mkoa wa Manyara, wenye Wilaya tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizokuwa zikitengwa kwa ukarabati ni kidogo sana, kiasi cha kuwaomba wadau mbalimbali wanaopenda kutumia chuo hicho kwa semina na mafunzo mbalimbali. Wameacha kufanya hivyo kwa ajili ya miundombinu chakavu. Matengenezo ya trekta hakuna. Hivyo, maeneo ya kilimo ya chuo, kukaa bure au kukodishwa kwa wananchi. Vilevile Chuo hakina gari wala pikipiki. Kwa sasa chuo hakina chombo chochote kinachofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii, Wilaya inafikiria kuiomba Serikali ili kubadili chuo hiki kuwa *VETA* ya Mkoa mpya na kukihamisha kwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo; je, Wizara ina maoni gani?

MHE. ANATORY K. CHOYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, kwa kujitahidi kutimiza matakwa yote ya wadau wote wa Wizara hii. Mchango wangu nauelekeza katika mambo makuu matatu.

Kwanza, fedha za mikopo ya akina mama, utaratibu unaotumika kwa sasa haulengi katika kumwondo au kumkwamua kutoka katika lindi la umaskini mwanamke. Mimi nimeona hivi kwa sababu mtindo wa sasa wa kugawa Sh.4,000,000/= bila vigezo maalum, hautaleta mabadiliko katika maisha ya wanawake ili kukidhi malengo na madhumuni ya mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nashauri kama tuzingatie ifuatavyo: Kwanza, jiografia ya Wilaya husika na hali halisi ya mazingira (aina ya miradi inayofaaa katika Wilaya). Pili, kiwango cha umaskini katika Wilaya. Tatu, idadi ya watu (*Population*),

mfano, Wilaya yenyé watu 400,000 kuipa Sh.4,000,000/= sawa na Wilaya yenyé watu 200,000. Nne, ukubwa wa Wilaya na vigezo vingine kama wataalamu wa Wizara watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, wapewe usafiri wa uhakika ili waweze kufuatilia miradi yote ya akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uongozi wa Vyuo vyá Ufundi na Bodi uandae mahitaji ya kila Chuo kwa kufuata vipaumbele (*priorities*) ili Wizara ijielekeze katika kutatua matatizo yanayolewaka, kwani mtindo wa sasa hautuelekezi katika kutatua au kupunguza matatizo halisi.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri na pongezi kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, naomba kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri, kwa barua ambayo Wizara yake imetupatia Shirika la *COEL*, linalojihusisha na kupambana na mauji ya vikongwe katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na kwingineko. Pamoja na barua hiyo kwa wafadhili lakini ni vyema Wizara ikatupatia fedha tulizoomba maana wafadhili hawajatoa chochote hadi sasa na tatizo bado linaendelea. Shirika la *COEL* liliomba kusaidiwa fedha Sh. 65 milioni ili kulipa uwezo wa kupambana na madhara haya ya mauji ya vikongwe. Nazidi kuiomba Serikali itusaidie maana kampeni ya *COEL* kuhusu madhara haya imeonekana kuwa na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja ya Waziri, Chuo chetu cha Maendeleo ya Wananchi Buhangija, hakikupewa fedha za ukarabati pamoja na kwamba, Waziri amewahi kutembelea hapo na kujonea hali halisi hasa ya mabweni. Naiomba Serikali ione uwezekano wa kutupatia fedha za ukarabati mkubwa katika kuboresha Chuo hicho. Pia suala la kiwanja cha shule litatuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya akina mama na vijana ni vyema fedha zikaongezwa. Fedha zinazotolewa ni ndogo mno na zinachangia kutupa lawama. Kuongeza fungu kulingana na wingi wa watu kutasaidia kuondoa umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Manispaa yetu ya Shinyanga ipewe gari ya Idara ya kufanya kazi maana wanazo kazi nyingi lakini hakuna usafiri wa kuweza kuwashamasisha akina mama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nyumba zinazolea watoto yatima wapewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Naibu Waziri na Mheshimiwa Shamim Khan, kwa kazi nzuri wanayoifanya Bungeni, kwa kujibu maswali yetu kwa usahihi kabisa, ninasema asante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana baada ya kubadili nembo ya Wizara hii kutoka Wanawake na Watoto na kuwa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nia ilikuwa nzuri sana, tafsiri imekuwa tofauti kabisa. Hii ni Wizara inayotegemewa sana na wanawake, lakini sasa huko Wilayani, kwenye Kata na Vijijini, Maafisa wa Wizara hii hawafanyi kazi za kuhakikisha wanawake wanawafikia huko waliko vijijini, kwa kuwaelimisha jinsi ya kupambana na umaskini. Afisa Maendeleo wa Wilaya anafanya kazi za Mipango badala ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Wizara hii ipeleke Waraka kwa Watendaji wao wawajibike, wanawake watapeleka wapi kilio chao cha kupata elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii iliweza kuwakusanya wanawake pamoja katika vyuo vyake na wakaweza kujifunza kwa vitendo katika kuendeleza vikundi vyao, sasa hivi vyuo viro, lakini wanawake hawana wahamasishaji tena na Watendaji husika kuweza kupewa Semina na mafunzo yoyote. Sasa hawa wanawake waende wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mama Anna Mkapa, kwa kujitaa sana kuwasaidia wanawake. Kupitia Wizara hii, naleta kilio cha wanawake wa Mkoa wa Mwanza, kwanza, wanaomba awatembelee ili wamwone na wazungumze naye, maana wanamwona tu katika mitandao ya TVT na ITV. Wanawake wanamhitaji. Pili, wanaomba maonyesho na Semina anazofanya awe anapeleka na Mikoa mingine, siyo kila mwaka Dar es Salaam ni wanawake wachache tu wanaweza kwenda Dar es Salaam, ni vipi sasa ataweza kubadilisha Mikoa kwa Mikoa ili wanawake wengi washirikishwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Wanawake wa Mkoa wa Mwanza wanaomba huu Mfuko wa fursa sawa kwa wote nao wakopeshwe. Mfuko huu ndiyo pekee utakaowasaidia katika kupunguza umaskini, naleta ombi kwako uweze kunifikishia kwa mama yetu Mama Anna Mkapa, kilio chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizidi kuwapongeza sana Waziri na Naibu, kwa kazi nzuri, tuko nyuma yenu ili tuweze kusimamia jamii, jinsia na watoto. Wizara hii ni kubwa na nyeti, lakini cha kusikitisha sana wanapewa fedha kidogo sana, hazitoshi hivi Sh.4,989,293,400/= zitafanya nini? Naomba Serikali izingatie sana hii Wizara inahusisha watu wote, inakuwaje wanaona ni wanawake tu, sio jamii nzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitafurahi kama Serikali itaandaa Bajeti ya dharura, ili Wizara hii ikidhi hoja za wanawake. Ukimwendeleza mwanamke, utakuwa umeiendeleza jamii nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa uanzishaji wa Benki ya Wanawake, hii Benki itawasaidia sana wanawake kwa kupitia *SACCOSS* zao. Tunawaombea sana mfanikiwe kuanzisha Benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa kuomba zaidi kwa Rais wetu, aweze kutuongezea nafasi za Watendaji Wanawake, asilimia tuliyonayo sasa ni ndogo, 31% haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate usafanuzi Jedwali la tisa, jina namba tano, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, namba 30 na 32, ukurasa 25 na 26 kwa nini ni wanaume au makosa ya uchapaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia na waongezewe fedha hazitoshi.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa niaba ya Wananchi wote wa Mwanga, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Asha Rose Migiro, kwa hotuba yake nzuri sana. Tumefurahishwa na malengo yaliyo katika mipango mizuri ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaelewa kuwa kazi hii nzuri ni matokeo ya timu nzuri iliyopo kwenye Wizara hii, ikijumuisha michango mahiri ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim Khan, Katibu Mkuu, Bi. Hilda Ausi Gondwe, Wakurugenzi na Maofisa wa juu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya Wizara kujenga uwezo wa kina mama kwa kuvisaidia vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa (*SACCOS*). Kwa mwaka huu wa fedha vyama vinne vya *SACCOS* katika jimbo langu vinaomba mikopo ya Sh.0.5 milioni (shilingi laki tano) kila kimoja. Vyama hivi ni *Songambele SACCAS* kilichoko Usangi, *Kimbakile SACCOS* kilichoko Kisangara, *Mwamko SACCOS* kilichoko Mwaniko na *Ugweno Kagongo Womens' SACCOS* kilichoko Lang'ata. Faida ya kuvisaidia vyama hivi ni kuwafikia wanawake wanaopambana na umaskini na uhakika wa fedha kurudishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi vya ujenzi vya Wilaya ni muhimu sana. Nawapongeza kwa kutoa mafunzo ya vikundi hivi kwa Wilaya chache. Kikosi cha Ujenzi katika Idara ya Maendeleo ya Jamii Mwanga ni kiungo muhimu sana katika kutekeleza miradi yetu ya MEMM, Majengo ya Maendeleo, Zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu kuwa katika mpango wa mafunzo kwa mwaka huu wa fedha (2004/2005), kikosi chetu cha Ujenzi Mwanga nacho kitapewa mafunzo na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutanguliza kuunga mkono hoja hii. Nawapa shukrani nyingi kwa kazi nzuri ya kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Watanzania tumetoka kwenye mila tofauti, Elimu na Dini zimebadilisha baadhi ya mila na kuleta usawa au kupunguza unyanyasaji kwa baadhi ya maeneo. Nakiri kusema maeneo yote ambayo bado yanazingatia mila kama unyanyasaji wa kijinsia na kuvunjwa kwa haki za kibinadamu, jambo hili linafaa kupigwa vita na Serikali yetu. Kwa hiyo, ingefaa kuwa na chombo cha kutafiti mila hizo potofu na kuanza kufuatalia kuzipiga vita, hata kuweka sheria za kuwasaidiwa wanaonyanyasika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri akipata nafasi, azungukie maeneo ya wafugaji akutane na akina mama wamweleze shida wanazozipata. Bado kuna mambo mengi ambayo hayastahili kufanya au kuwepo, lakini kwa kuwa ni mila, wameona kwamba, ni haki zifanywe eti tu kwa sababu ndiyo desturi za mila zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mikopo, Halmashauri zetu hawajawahi kukubali kutoa asilimia kumi tangu ipitishwe kwenye Bunge na kwa sababu hawawezi kutoa kwenye makusanyo ya Mapato wanayokusanya, napendekeza kwenye fedha zinazotumwa kwenye Halmashauri toka Serikali Kuu, zikatwe fedha hizo ili zipelekwe kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika nchi yetu maeneo ya wafugaji bado wako nyuma hasa wanawake, hawapewi nafasi ya kusoma au maendeleo ya aina yoyote. Naiomba Serikali iwasaidie wanawake hasa wale ambao wamesoma wamemaliza Sekondari, kwani wanapomaliza wazazi wanawarudisha nyumbani kwenda kuwaoza hata kwa wanaume ambao hawakwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi wa kike ambaye amemaliza shule hawezi kujitafutia shule aendelee kama mzazi wake hawezi hata kutafuta kazi au chuo. Kwa hiyo basi, nakuomba uwasaide wasichana wa Kimasai wanaomaliza Kidato cha IV na VI, wapate vyuo kwani wanateseka sana kwa mfano, wale wasichana waliomaliza *Form VI* waliotembelea Dar es Salaam, wengi wao hawatapata nafasi ya kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iokoe maisha yao kwa kuwapa nafasi waendelee. Nategemea Waziri atanijibu kwenye majumuisho yake.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Wazir, Naibu wake na Uongozi mzima wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza hotuba na naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia haya yafuatayo: Kwanza, mikopo kwa wanawake, Serikali inajitahidi kusaidia wanawake katika suala la mikopo lakini nashauri mikopo hiyo inayotolewa iende zaidi vijijini na wataalamu waende huko vijijini kutoa Elimu ya Biashara, baadhi ya wataalamu hawapendi kwenda vijijini kwa walengwa hivyo, hupelekeea wanawake kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu mikopo. Hupelekeea wanawake hao kutokulipa *installment* zao *properly* ili na wenzao wapate mkopo kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri Halmashauri zake za Miji na Wilaya, ziwapatie zile fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mabenki ya Wanawake. Inaonekana Halmashauri nyingi haziipi kipaumbele mikopo hii kwa wanawake (fungu la wanawake). Pili, matatizo ya watoto yatima na wale wanaotembea na wazazi wao kwa ajili ya kuomba misaada. Tatu, Elimu ya Ukimwi kwa Wananchi, madhara ya Ukimwi ni tishio kubwa hasa kwa upande wa wanawake. Napendekeza Serikali iendelee zaidi kuelimisha jamii juu ya janga hili la Ukimwi, hasa kwa wale wanawake wajawazito, ni vyema wanawake wakusanywe pamoja huko vijijini na kuelimishwa kwa maelezo na pia kuoneshwa sinema (*film*) maalum za matatizo kuhusu Ukimwi. Ni vyema kufanya hivyo maana si kila mtu (mwanamke) hasa vijijini kuwa anatambua athari zinazopelekea maradhi haya ya Ukimwi. Elimu ifike vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia moja.

MHE. JOHN E. SINGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri ya maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ipo kazi nzuri ambayo imefanyika ya kukarabati vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii. Vyuo hivi vilikuwa vinasikitisha mno, lakin amevirejeshea uhai. Napenda pia nichukue nafasi hii nimpongeze Katibu wake Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa mema yote ambayo wamewafikishia Wananchi wetu katika Majimbo yetu ili uhai huu uzidi kuonekana na kuwa na mwanga wa maendeleo kwa Wananchi wetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri afanye yafuatayo:-

Kwanza, Chuo cha Wananchi wa Same kilifanyikwa ukarabati mdogo, naomba akikamilishe kwa kukipatia ukarabati mkubwa. Chuo hiki kina uhaba mkubwa wa maji na hivyo kuathiri maendeleo ya Wanachuo na Wafanyakazi kwa kuzunguka kutafuta maji na wakati mwingine kukatisha mafunzo. Hali hii inazorotesha taaluma na mwamko wa Wanachuo na Wakufunzi katika maendeleo ya Chuo chao. Namwomba Mheshimiwa Waziri, awapatie kisima kimoja cha maji ikiwa ni pamoja na kukarabati tangi la maji lililochakaa na au linunuliwe jipya kwa sababu lililopo nadhani liko *beyond repair*.

Pili, Maafisa Maendeleo ya Jamii hawa wana uhaba mkubwa katika Halmashauri yetu ya Same. Wakati tukipanga bajeti ya kuwaajiri hawapatikani. Ili kuhimiza mchakato wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu, hawa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, mafunzo yao katika vyuo yazingatie kuongeza idadi yao. Kuwepo kwa Maafisa hawa katika Wilaya haitoshi. Ipo haja ya kila Kata kuwa na Afisa Maendeleo ya Jamii. Wizara ya TAMISEMI na Wizara yako ingeliona hili na

kushirikisha nguvu ili huduma ya maafisa hawa iwepo katika kila Kata na hivyo kuwa rahisi kuifikisha vijijini na katika vitongoji.

Tatu, Mikopo ya akina mama katika Halmashauri nyingi, imekuwa shida kurejeshwa hususani Halmashauri yangu ya Same. Wizara ingefanya uchunguzi ni kwa nini hili linatokea. Je ni kwa sababu labda wanaopewa mikopo hii wanalipishwa riba mara mbili, ile ya mkopo na ya *black box* ya anayetoa mkopo au ni kwa sababu wanaopewa mikopo hawajaelimishwa jinsi ya kutumia mikopo yao izalishe na kulipa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri na hotuba ya kufaa maendeleo ya watu wetu.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi na uwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole nyingi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, kwa kuondokewa na mpendwa wao. Natoa pole pia kwa Wabunge wenzetu wale wote waliofiwa na wazazi wao, watoto wao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Naibu wake, Shamim Khan, Katibu Mkuu, Bi. Hilda Gondwe na wataalam wote, kwa kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu kwani inahudumia jamii yote ya nchi ya Tanzania. Matarajio ya Wananchi ni kupelekewa elimu, maendeleo ya kutosha hasa vijijini. Aidha, bajeti iliyotengwa ya Wizara hii, haitoshelezi kwa maendeleo ya jamii kubwa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa mbali na kituo cha Arnautoglou, kulikuwa na vituo vingine hapo zamani kwa ajili ya wanawake katika kuwaleta mafunzo mbalimbali. Hivi sasa vituo hivyo ni vichache na hasa ukizingatia kuwa idadi ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam imeongezeka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara hii kwa kuendelea na mpango wa uanzishwaji wa Benki ya Wanawake, zinazokusudia kuendeshwa kwa mfumo wa Vyama vyta Ushirika (*SACCOS*). Ninaishauri Wizara hii sasa kwa nguvu na nia moja, waanze bila kuchelewa, kuwashamasisha wanawake katika kila mkoa, kwa kupititia Maafisa Maendeleo ya Jamii na pia kwa Viongozi wa Juu wa Wizara, kufuatilia kupititia mikoani ili wawahamasishe wanawake kuanzisha *SACCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Chombo cha Wanawake kipo mbioni kuanzishwa rasmi, nashauri Wizara hii ijitahidi pia kuanza mapema kuwaelimisha wanawake nchini ili watoe maoni yao na waelewe muundo na dhamira ya chombo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili chombo cha Wanawake kiweze kujiimarisha na kutoa huduma bora kwa wanawake wote, inapaswa chombo cha Wanawake kiweke ofisi zake katika kila Mkoa ambapo wahudumu kama vile Maafisa wa Maendeleo ya Wanawake watafikiwa kwa urahisi na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jedwali la Bajeti hii inasikitisha sana kuona kuwa bado Wilaya nyingi hazijarejesha mikopo. Huu umekuwa ni ugonjwa mkubwa. Endapo *SACCOS* nyingi zitaanzishwa, ugonjwa huu wa kutorejesha mikopo huenda ukajitokeza. Naiomba Wizara hii isikae kimya tu, ni lazima ihakikishe kuwa, inatengeneza mikakati kamambe kwa ajili ya ufuatiliaji wa mikopo hiyo isiyorejeshwa. Endapo Wizara haitatilia nguvu katika jambo hili, basi hata uwezo wa kutoa ushauri na kuratibu marejesho katika vikundi nya *SACCOS*, hautaimarika na lengo la kuanzisha Benki ya Wanawake litapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika ingelifa iwapo Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika Wilaya zao, watajitahidi sana, kufuatilia na kuwakumbushia wakopaji wajitahidi kurudisha mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Wizara imejitahidi sana siku zilizopita, kutoa Nishani kwa wanawake mbalimbali. Naomba Wizara hii iendelee kupekua vizuri na kwa makini, kwa kutumia vyombo nya siasa na ofisi mbalimbali, wataweza kupata majina ya wanawake wengi waliofariki na walio hai, ambao wameitumikia nchi hii katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja hii.

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa sasa wa kutoa fedha za mikopo kwa wanawake kwa kupelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya, umeonekana kuwa na kasoro kubwa hasa kwenye Wilaya ambazo zina Majimbo zaidi ya moja. Mgawanyo wa hizo pesa huzipendelea sehemu za miji au Majimbo yaliyoko karibu na Mijini na Majimbo mengine yaliyoko mbali na Mji huambulia kiasi kidogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fedha kwa ajili ya mikopo ya Wanawake na Vijana zigawiwe ki-Majimbo ili kusiwepo na kupunjwa Majimbo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wote wanastahili kusaidiwa mikopo hii na siyo wanawake wa mijini tu au wa Majimbo ya karibu na mijini tu. Kwa hiyo, naomba Wizara wakati inatuma fedha hizi za mikopo ya wanawake, ipeleke na maelekezo ya kiasi gani cha fedha kinapelekwa kwa kila Jimbo na taarifa hizi Wabunge tuelezwe. Bila kufanya hivyo, fedha hizo zitaishia mikononi mwa watu wachache, wenye kujipendelea au kuwapendelea marafiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Nanyumbu, kiasi cha mikopo hii ni kidogo sana na malalamiko ni mengi kutoka kwa wanawake kuwa hawapati mikopo hiyo wala hawaleezwi kama fedha hizo zipo. Ikiwa Wabunge watajulishwa juu ya fedha zinazokwenda kwenye Majimbo yao, basi itakuwa rahisi kuhamasisha akina mama

kukopa fedha hizo ili waweze kujiletea maendeleo. Aidha, itakuwa rahisi kwa Wabunge kuweza kufuatilia juu ya urejeshaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo mdogo, nami ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nianze kwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Aidha, naomba nichukue fursa hii maalum, kwanza, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kuwasilisha hotuba nzuri sana katika hali ya utulivu na kujamini, tena kwa ufasaha mkubwa. Pia niwapongeza sana Wasaidizi wake, wakiongozwa na msaidizi wake Naibu Waziri wa Wizara, Mheshimiwa Shamim Khan na Wasaidizi wao wote, kwa kuonesha umahiri wao mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi zangu, naomba kutoa pongezi maalum kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuchagua timu nzuri ya kuongoza Wizara hii na kuonyesha ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inayo nafasi kubwa kushirikiana na mwenzake kule Zanzibar, kwani huduma nzuri kwa jamii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi zetu mbili (Zanzibar na Tanzania Bara). Aidha, mimi nimepata faraja kubwa kushuhudia kuwa Wizara hii imekuwa kiungo kizuri kati ya Serikali Kuu na wenzetu wa Upinzani, jambo ambalo ni muhimu sana kwa Tanzania na Wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, masomo au mafunzo ya Maafisa Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana kwani kuna ukosefu au uchache wa wataalamu hawa amba ni watu muhimu katika maendeleo ya Wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya kuwaendeleza wanawake ni muhimu sana na ni jambo ambalo linahitaji sana mtazamo wa Wizara wa kuendeleza malipo au marejesho ya mikopo hiyo ili fedha hizi ziweze kuwanufaisha wengi. Aidha, mimi sina hakika kuwa utaratibu huu unawanufaisha kule Zanzibar na iwapo bado haujafika basi umuhimu wa makusudi uandaliwe, kuwafaidisha wenzao kule Zanzibar. Mimi nitashukuru sana kuona Benki ya Wanawake wote tena wa pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke katika jamii hii ya Tanzania ni mwenye umuhimu wa aina yake, kwani mimi nina imani na kuamini kuwa ni chanzo na chimbuko la utulivu na amani ya nchi hii, kwani wanawake wa Tanzania wana tabia ya kuwapa amani na faraja wanaume hasa kwa kuwa wanawake wamejaliwa kuwa na imani kwa wanajamii wa Tanzania. Aidha, wanawake wetu wamekuwa ni waalimu wa familia zetu.

Pamoja na Wizara hii kuwa kiungo cha maadili mema mionganoni mwa Mawizara mengine ya Tanzania, ninaomba sana katika bajeti ya mwakani (2005/2006), ziongezewa

fedha za matumizi yake ambayo mwaka huu imepewa fedha chache kutokana na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa kumwombea afya njema, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na pia nimtakie Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, afya njema katika kuiendesha Wizara hii kwa ufanisi mkubwa kiasi cha kuipa heba Serikali yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba tena kuunga mkono hotuba hii kwa ukamilifu.

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii.

Kwanza, nawapongeza sana Mheshimiwa Dr. Aisha-Rose Migiro, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamim P. Khan, pamoja na watendaji chini ya uongozi wa Bibi Hilda Ausi Gondwe.

Napenda pia kumpongeza sana Mwenyekiti wa Mfuko wa Fursa sawa kwa wote (*EOTF*), Mama Anna Mkapa, kwa mchango wake mkubwa wa kuwasaidia kina mama kujikwamua katika umasikini. Nazipongeza pia Wizara na Taasisi mbalimbali zinazoshirikiana na Wizara hii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichangie maeneo machache yafuatayo:-

Kwanza, mikopo ya akina mama (*WDF*), pamoja na utaratibu mzuri wa kutoa mikopo toka kwa Waziri bado inakuwa kero kwani Halmashauri nyingi hazitengi fedha hizi pamoja na kusisitiza sana katika vikao vya Halmashauri. Sasa je, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani endelevu wa kuzibana ili Halmashauri zitii utaratibu huu?

Pili, Wizara hii ni kubwa, pana na nyeti, ukizingatia inagusa sana Wanawake na Watoto ambao asilimia yao ni kubwa lakini pamoja na unyeti wa Wizara hii inaonekana Serikali hawaioni. Ni kwa nini bajeti yake ni ndogo sana? Tungeomba iongezewe fedha ili iweze kumudu kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo Handeni kinaendelea vizuri na ninashukuru Wizara kwa juhudzi zake za kukisaidia. Ombi maalum, Mheshimiwa Waziri bado Kitengo cha *Computer* hakijaanza kutokanana uhaba wa pesa za kununua vifaa vya kuboresha zile *computer* zilizotolewa na Mheshimiwa Mbunge wa Handeni zifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu bidhaa ambazo wanauzwa akina mama wakati wa maonesho. Wanapata msaada mkubwa toka *EDTF, SIDO, UNIDO* na kadhalika. Wanapata mafunzo mengi na wengi wameweza hata kufanya biashara nchi za nje. Lakini tatizo ni kuwa bidhaa nyingi zinafanana hivyo inakuwa tabu katika ushindani wa soko. Nashauri hawa Wajasirimali wabuni miradi mbalimbali inayotofautiana ili wawe na ushindani mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hotuba ya Waziri imeonyesha uwazi na dira katika mpango wake wa mwaka 2004/2005, basi naomba niwaombee kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunaikumbusha Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii ikidhi haja.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii bila shida yoyote. Kwa muda mrefu sana nimekuwa nikihoji na kuomba Serikali ifanye ukarabati wa jengo la bweni kwenye Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Munguri, lakini mpaka sasa ni miaka zaidi ya saba bado sehemu ya Bweni hilo haijkarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, katika vyuo ulivyovitaja ambavyo vitakarabatiwa 2004/2005 na Munguri kipo?

Pili, Serikali ina mikakati gani kuwaondolea kero wanawake wa vijijini ambao wana shida sana katika maisha yao, vikwazo hivyo ni pamoja na kusafiri masafa marefu kutafuta kuni na pia bado wanabebe mizigo mizito vichwani na migongoni, hususani wa vijijini, wanawake bado wanaumia macho kwa kuendelea kutumia kuni kwa kukosa majiko ya kisasa na umeme nuru na pia bado kliniki ziko mbali sana, kwa nini vituo vyta kliniki visiwekwe kwenye vijiji ili kuwapa nafuu wanawake na watoto, ni maelezo ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali haijazingatia kuweka katika Soko, baiskeli za kuwawezesha wanawake kuzitumia bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Mfuko wa Wanawake unaotolewa na Serikali wa Sh.4,000,000/= hazitoshii kabisa kubadilisha maendeleo ya vikundi huko Wilayani. Napendekeza kiwango hicho sasa kipande kiwe Sh.8,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nikushukuru kwa dhati wewe binafsi, kwa kuniruhusu ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika kuiunga mkono hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro. Naomba niseme kwamba, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, naomba kwanza, niwape pole ndugu, jamaa na marafiki wote waliofiwa. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu wote pahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, waliopata nafasi mbalimbali za uongozi na uwakilishi nje na ndani ya nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba, Mheshimiwa Waziri, ananishirikisha kikamilifu katika kuliendeleza gurudumu la Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Pia namshukuru sana Bibi Hilda Gondwe, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, pamoja na wataalam wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuliendeleza gurudumu hili. Naomba nisiwasahau Makatibu Muhtasi, wahudumu na madereva, kwa kufanikisha kazi zetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mbunge wa Misungwi, amezungumzia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi, anaomba usafiri, ameomba pia ufanywe ukarabati wa majengo lakini pia ameomba fedha za *OC* ziongezwe. Niseme tu kwamba, ni kweli Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi, pamoja na Vyuo vingine vya Maendeleo ya Jamii, kama vile Buhare na Rungeba, vinahitaji ukarabati wa majengo na miundombinu kwa kiasi kikubwa. Mwaka 2003/2004, kila Chuo kilipatiwa kiasi cha shilingi milioni 15. Lakini mwaka huu Wizara yangu imeongeza fedha hizo na kutenga jumla ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya kufanya ukarabati Vyuo hivi. Fedha hizi tunajua haziwezi kumaliza matatizo yote, lakini “haba na haba hujaza kibaba.” Wizara yangu itaendelea pia kuboresha hali ya usafiri na majengo, azma iko pale pale. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mishahara ya watumishi wa Chuo cha Misungwi, ni kweli uboreshaji wa mishahara ya watumishi wa Serikali ni zoezi linalofanywa kila mwaka na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na watumishi wamekuwa wakipandishwa mishahara kila mwaka. Kwa hiyo, zoezi hili lipo na litaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Lekule Laizer kutoka Jimbo la Longido, amezungumzia kiwepo chombo cha kutafiti mila potofu na kupiga vita mila hizo. Mheshimiwa Mbunge wazo lako ni nzuri sana, nakushukuru. Lakini pia naomba tu niseme kwamba, tayari Wizara imeanza kazi hiyo ikishirikiana na wadau wengine zikiwemo *NGOs*. Kwa bahati nzuri mwaka huu Wizara imetenga fedha ili kufuatilia suala hilo la mila potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Elizabeth Batenga amezungumzia masuala ya Bodi ya Vyuo akasema kwamba, hazikutani. Ni kweli ninaafikiana naye, lakini naomba tu nitoe taarifa kwamba, mwaka 2003 kati ya Vyuo 58 ni Vyuo 30 vilifanya vikao vya Bodi. Nafurahi kusema kwamba Chuo chake cha Gera nacho kilifanya kikao hicho cha Bodi. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba, tutaendelea kuwa pamoja katika kutekeleza azma hiyo. Pia amezungumzia masuala ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwamba, kuna haja ya kufanya utafiti kuona chanzo cha matatizo hayo. Nakubaliana naye kwamba, kuna haja ya kufanya hivyo. Mwaka 1998 Serikali kwa kushirikiana na *UNICEF*, ilifanya utafiti katika kubaini matatizo yanayowakabili watoto katika mazingira magumu na kuweza kutafuta njia za kuwasaidia.

Utafiti huo uliwalhusu watoto yatima wanaoishi mitaani, watoto wenye ulemavu, wanaofanya kazi za ajira, wanaoolewa na kuzaa katika umri mdogo. Utekelezaji wa matokeo ya utafiti huo unaendelea kushughulikiwa katika programu ya uhai, ulinzi na maendeleo ya mtoto katika ngazi za kijiji, Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Elizabeth Batenga amezungumzia kwa uchungu *NGOs* nyingi zinazoshughulikia watoto hawa zinatakiwa ziwaunganishe wazazi wao na siyo tu kuanzisha Vituo. Tabia zao zinatakiwa zibadilishwe. Watoto waunganishwe na wazazi wao ieleweke kwamba *NGOs* wanajali maslahi yao wenyewe. Mimi ninaomba nikiri hapa kwamba, *NGOs* nyingi zinafanya kazi nzuri sana kwa sababu ni wadau. Nisingependa kulidanganya Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali peke yake ingeweza kufanya lolote bila kuwashirikisha wadau na tuna mifano mingi halisi na hai jinsi *NGOs* zinavyofanya kazi pamoja na Mashirika ya dini. Kwa mfano, *TAMWA*, *TAWLA*, *AFNET* hapa Dodoma, *Save the Children of Tarime*, *Women Wake Up*, *TGNP*, *World Division, Network Against FGM* Moshi. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba, tusitoe blank statement kwamba, *NGOs* zote hazifanyi kazi. Iwapo kama kuna *NGO* una uhakika inababaisha au inababaika huko, basi tutakuwa tayari kupokea taarifa hizo ili tuzifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia pia masuala ya watoto yatima kuwarudisha majumbani kwao. Mimi ninaafikiana na Mheshimiwa Elizabeth Batenga mia kwa mia kwamba, kuna haja ya kufanya hivyo na ninaomba nitoe mfano mmoja tu wa Kanisa la *Menonites Tanzania*, Dayosisi ya Mashariki Jimbo la *Iringa Road* hapa Dodoma. Wao wamewakusanya watoto wa mitaani wanafundishwa, wanapewa sare za shule wanaenda shule, lakini jioni huwa wanarejeshwa kwa wazazi wao na kwa jamaa na ndugu zao. Kwa hiyo, mimi natoa pongezi kwa Kanisa hilo na ninatoa wito kwamba, ni vizuri watoto wasilundikwe sehemu moja, bali tufanye bidii kuwatafuta wazazi au jamaa. Namshukuru sana Mheshimiwa Elizabeth Batenga, kwa ushauri wake.

Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, amesema Wizara ishirikiane na Taasisi kama *TAMWA* ili kukemea vitendo vya ubakaji nichini. Naafikiana na Mheshimiwa Mbunge, tumefanya hivyo, tunashirikiana na Taasisi mbalimbali kama vile *UNICEF*, *TAWLA*, Kituo cha Msaada wa Kisheria cha Wanawake (*TGNP*) na nyinginezo ili kukemea vitendo vyote vya unyanyasaji dhidi ya wanawake ukiwemo ubakaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu itolewe kabla ya kutoa mikopo ni kweli naafikiana na Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah na ndiyo maana tunesema kwamba, tunapopeleka shilingi milioni nne katika kila Wilaya ile riba ya shilingi 400,000/= huwa tunawaachia wenyewe Wilayani, fedha zile ndiyo zinatumika kutoa elimu kwa hao watakaokopeshwa, naafikiana na wazo hilo. Halmashauri ambazo hazijarejesha mikopo zichukuliwe hatua. Tunawasiliana na Wizara ya *TAMISEMI* na ni wazo zuri.

Mheshimiwa Semindu Pawa, amezungumzia udhalilishaji wa watoto nichini, kazi ngumu za watoto, kubakwa, kufanyiwa vitendo vya kinyama, ametoa wazo kwamba,

Wizara ishirikiane na Polisi kuchunguza maeneo ya *Coco Beach* kuona jinsi watoto wanavyofanyiwa. Alifuatilia *Radio Clouds* juu ya mtoto mmoja. Mheshimiwa Semindu Pawa, nakushukuru sana kwa wazo lako na Wizara itashirikiana na Polisi ili tuweze kuchunguza maeneo ya *Coco Beach* na kuona maovu yanayotendeka pale. Lakini pia amezungumzia kwa uchungu udhalilishaji wa watoto upo katika baadhi ya maeneo ya mijini. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwemo Shirika la Kazi Duniani, inaratibu Programu Maalum ya kupambana na ajira mbaya kwa watoto hapa nchini. Programu hii inasaidia kwa kiwango kikubwa, kuondoa ajira mbaya hasa katika mashamba makubwa, kwenye migodi ya madini, kazi za nyumbani, biashara za mitaani na biashara ya ngono kwa watoto. Mheshimiwa Semindu Pawa naomba uridhike na majibu hayo. Vile vile Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, amezungumzia mikopo ya wanawake na vijana na yeye ameonyesha *concern* kwamba, mikopo hairejeshwi. Naomba tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, tumeleta mwongozo wa mikopo hiyo na kwamba, kuna *Area Loan Committee* na katika *Area Loans Committee* ile sisi pia ni Wajumbe. Sasa kazi ya *Area Loans Committee* siyo tu kugawa mikopo lakini pia kufuatilia mikopo. Kwa hiyo, mimi naomba kwamba tuwe pamoa katika ufuatiliaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa George Lubeleje, ametupongea Wizara kwa kukarabati majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Chisalu, tunapokea pongezi hizo kwa mikono miwili. Mheshimiwa Waziri amezipokea. Je, umezipokea Mheshimiwa Waziri? Amekubali. (*Makofi/Kicheko*)

Chuo cha Chisalu kupatiwa walimu wa kutosha wa fani mbalimbali. Tunaafikiana kwamba, kuna haja ya kufanya hivyo. Wizara mwaka huu imepata kibali cha kuajiri wakufunzi wapatao 25, ambao taratibu za kuwaajiri zimeanza kwa mwaka huu. Wizara inaahidi kukipelekea Chuo hiki mkufunzi mojawapo kati ya wakufunzi wa fani watakaopatikana. Kwa hiyo, Mheshimiwa George Lubeleje naomba uniachie shilingi yangu. Wizara kukiengesha Chuo cha Wananchi Chisalu fedha za kukarabati trekta na gari ili trekta litumike kulimia eneo kubwa la shamba na kukiwezesha chuo kujipatia chakula, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, mambo yakiwa mazuri tutakuwa nawe lakini azma iko pale pale.

Halafu amezungumzia tena kuwapatia huduma za simu kurejesewa mawasiliano. Wizara inavipatia Vyuo vyote vyenye simu fedha za kulpia gharama zake. Tunapeleka fedha kwenye Vyuo vyote siyo tu chuo hicho cha Chisalu. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu kuboresha huduma ya umeme, Chuo hiki kina *generator* la umeme na katika mwaka 2004/2005, Vyuo vyenye *generators* vimetengewa fedha za kuziendesha ili kuboresha huduma za umeme. Pia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu kubadilishwa ili kutoa mafunzo ya Maendeleo ya Jamii ngazi ya Cheti na baadaye *Diploma* ili kuongeza idadi ya Vyuo hivi nchini.

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu kinahudumia Wananchi wa Wilaya za Mpwapwa, Kongwa na Dodoma Mjini kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali

yanayotarajiwa kuwawezesha kujajiri, kuboresha utendaji wao na hivyo kujitegemea. Jukumu hili ni kubwa.

Mheshimiwa Lubeleje umezungumza mambo mengi kuhusu chuo hicho hicho. Kwa kuwa wanawake wengi hawana kipato cha kutosha ipo haja Serikali kuongeza fedha za mkopo ili wanawake waanzishe miradi midogo midogo. Mheshimiwa Lubeleje naafikiana nawe lakini naomba pia tukawasimamie Wakurugenzi wetu ili watimize agizo la Waziri Mkuu. Naelewa fedha hazitoshi lakini tukiwasimamia vizuri naona angalau wanawake wengi watapata mikopo hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondo Kaskazini anulizia Serikali ina mkakati gani wa kuwaondolea kero wanawake wa Vijiji ambao wana shida sana katika maisha yao. Kama alivyozungumza pia Mheshimiwa Jenista Mhagama. Wizara imeandaa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ambayo inaelekeza wadau mbalimbali namna ya ushiriki wao katika kuwaondolea wanawake matatizo. Aidha, Wizara itaendelea kuzishauri Halmashauri kutekeleza majukumu yao ya kupanga mipango na mikakati mbalimbali ya kuwaondolea wanawake kero na kuwaaletea maendeleo.

Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi inasikitishwa sana kuona watoto wadogo wakiandamana na wazazi wao mitaani ili kuomba misaada kutoka kwa jamii. Amesikitishwa sana. Suala la ombaomba linasababishwa kwa kiasi fulani na umaskini katika familia. Kwa vile ombaomba hawana makazi maalum ndiyo maana wanaonekana mitaani na watoto wao. Matatizo ya watoto kama hawa yameingizwa katika Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kupunguza umaskini (*Poverty Reduction Strategies*)

Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki anazungumzia kwa uchungu ubovu wa majengo ya Chuo cha Maendeleo Wananchi Mbinga. Naafikiana na yeche kwamba majengo sio mazuri na kwamba Wizara ilianza utaratibu wa kuimarisha majengo ya vyuo hivi kuanzia mwaka wa fedha 2001/2002. Katika mpango huo Chuo cha Mbinga kilipatiwa kiasi cha shilingi 5 milioni kwa ajili ya ukarabati mdogo wa majengo. Mungu akijalia tukipata fedha basi tutaendelea kukikumbuka Chuo cha Mbinga.

Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, anasema kutokana na kufanana kwa bidhaa zinazonyeshwa katika Maonyesho ya Saba Saba anatushauri kuwa wajasimali wabuni miradi mbalimbali inayotofautiana ili wawe na ushindani mkubwa. Ninaafikiana kwamba hakuna haja ya kupeleka kwenye mashindano au kwenye maonyesho bidhaa ya aina moja hata watazamaji watachoka na soko litakuwa halipo. Kwa hiyo ninazingatia wazo lake.

Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki amezungumzia maendeleo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msingi yanakwamishwa na uchakavu wa miundombinu na ukosefu wa usafiri, hivi chuo kikumbukwe katika bajeti hii. Wizara yangu inatambua kwamba kuna matatizo na katika bajeti ndogo kwa mwaka jana

tulimpatia kiasi cha shilingi 4 milioni mambo yakinunyookea basi tutawakumbuka ndugu zetu wa Iramba Mashariki.

Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi amezungumzia mikopo ya wanawake hairudishwi hasa Halmashauri ya Same. Wizara ifanye uchunguzi kwa nini hili linatokea. Ninaafikiana naye mia kwa mia kwamba kuna haja ya kufanya utafiti lakini naomba utafiti huo tufanye kwa pamoja kwa sababu inawezekana vikundi hivyo ni hewa, inawezekana kabisa katika Wilaya yako Afisa Husika hatoi elimu kabla ya kutoa mikopo. Kwa hiyo mimi nashauri twende turudi pale pale ili tutasaidiana. Wanawake wanaopewa mikopo hawapewi elimu.

Lakini nimesema mwanzoni kwamba tumeanza mtindo kuwa riba ile ya asilimia 10 inabakia pale pale Halmashauri na fedha zile ndiyo zinatumika kutoa elimu. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa pamoja tufuatilie kwamba fedha zile zinatumika kutoa elimu kwa kinamama wanaokopa.

Mheshimiwa Aridi Mwananche Uledi, Mbunge wa Nanyumbu anazungumzia upelekaji wa fedha za mikopo kwenye Halmashauri una kasoro kubwa hasa kwa Wilaya zenye Majimbo zaidi ya moja. Mgawanyo wa fedha hizi unapendelea mijini na Majimbo yaliyo karibu na Mjini. Mheshimiwa Mbunge naomba tu niseme kwamba sisi kwa upande wa Wizara huwa tunapeleka fedha moja kwa moja katika Wilaya. Najua mtakasirika na mtachukia lakini ukweli unabaki pale pale kwamba sisi ni Wajumbe katika *Area Loans Committee*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba basi ukiwa pale vikundi vikija tuanze kuvi-screen vizuri kwamba je kikundi hiki kinatokea wapi. Lazima uhakikishe kwamba fedha zinatawanywa mijini na Vijijini na kazi hii naona unaweza ukafanya wewe kwa sababu wewe ndio unaingia katika *Area Loan Committee*. Lakini bado naomba nitoe wito kwamba tusiwapendee tu wanawake wa sehemu moja na tukawasahau wanawake wa sehemu nyingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia mikopo igawiwe kufuata Majimbo ya Uchaguzi. Wazo lako ni zuri, lakini tukumbuke kwamba fedha zinapopelekwa lazima kuwepo na uwajibikaji na uwajibikaji upo kwenye Halmashauri. Ndiyo maana tumeona, kwamba fedha zipelekwe kwenye Halmashauri na Halmashauri zitagawa kufuatana na Majimbo ili *Financial Regulations* zifuatwe. Wabunge waelezwe kiasi cha fedha kinachopelekwa. Hilo naafikiana nanyi. Kwamba kuna haja mpate maeleo na tumekuwa tunafanya hivyo kila tukipeleka fedha kwenye Wilaya zenu ili nanyi mnapewa taarifa. Tutaendelea kufanya hivyo ili muweze kufuatilia.

Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum amezungumzia masuala mengi tu. Kwa upande wa mikopo ya wanawake Halmashauri hazichangii asilimia tano. Je, zinachukuliwa hatua gani. Mheshimiwa Mbunge, Halmashauri nyingi zimeanza kuchangia katika viwango tofauti, lakini Halmashauri nyingi tu hazijafikisha asilimia tano. Kwa hiyo nami natoa ombi au naagiza kwamba agizo la Waziri Mkuu litekelezwe ipasavyo ili wanawake wengi waweze kunufaika na

mikopo hii. Wizara ina mikakati gani ya kuongeza fedha za mikopo. Sawa, mikakati itawekwa mara tu hali ikituruhusu.

Maafisa Maendeleo ya Jamii wafanye jitihada maalum kuhamasisha watu wenye ulemavu kijiunga ili nao wanufaika na mikopo. Ninaafikiana na Mheshimiwa Margareth Mkanga kwamba tusiwabague akinamama wenye ulemavu. Wao ni wenzetu na wana haki sawa. Kwa hiyo ninaafikiana nawe na mlimsikia mwenyewe alivyopongeza Kigoma Vijijini na Morogoro Mjini kwa jinsi wanavyowasadida akinamama wenye ulemavu. Naomba basi Wabunge wenzangu na sisi tukifika kwenye maeneo yetu tusiwasahau wanawake wenye ulemavu maana ni wenzetu.

Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mbunge wa jimbo la Mwanga. Anazungumzia Kikosi cha Ujenzi na mafunzo ya ufundi cha Halmashauri ya Mwanga kipewe mafunzo rejea kwa mwaka 2004/2005. Kwa mujibu wa aya 75 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Wizara katika kipindi cha mwaka 2004/2005 itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa mafundi 60 wa vikosi vya ujenzi kutoka Wilaya 20. Kwa kuwa mafunzo ya kikosi cha Mwanga hawajapewa mafunzo hayo Wizara yangu itazingatia hoja ya Mheshimiwa Mbunge punde wakati wa kuteua Wilaya na majina ya mafundi husika utakapowadia.

Mheshimiwa Kissasi, Mbunge wa Dimani amezungumzia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Vijana, Ajira na Maendeleo ya Wanawake na Watoto washirikiane na wadau wengine. Tunafanya hivyo hususan katika kudhibiti elimu mbovu na vipindi vya *TV*, *Radio* na cinema, *video* na kadhalika. Vyombo hivyo vya habari vinatumwi vibaya kupotosha zaidi maadili ya familia kuliko kuelimisha na kujenga jamii. Vipo baadhi ya vipindi vibovu vya *TV* vinavyotolewa wakati wazazi, walezi wakiwa makazini ambavyo vinaharibu kabisa vijana wetu hatuna budi wote kuwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafikiana na Mheshimiwa Mbunge lakini pia naomba tu niseme kwamba vyombo hivi vya *TV*, *Radio* vinatusaidia pia. Lakini kuna baadhi ya vipindi ambavyo ni kweli na naafikiana nawe kwamba havifai. Sasa tumepokea ushauri tutashirikiana na wahusika hususan Tume ya Utangazaji, Ofisi ya Waziri Mkuu (Habari na Siasa). Nashukuru kwa mawazo hayo na wenyewe wanasilika wapo hapa.

Mheshimiwa Ngwatura tena amezungumzia maslahi ya watumishi hasa wale walioajiriwa ili kutoa mafunzo ya ustadi hususan umeme, ufundi. Kwanza mishahara yao ni ya chini. Amezungumzia kwamba tujaribu kurekebisha mishahara yao. Tayari baadhi ya watumishi hao wangependa muundo wa vyuo hivyo uwe kama ule wa *VETA*. Kwa kawaida viwango vya mishahara vya mafundi wote wa Serikali hutolewa kwa kulingana katika Wizara zote kwa kufuata ujuzi na elimu zao. Wenzetu wa *VETA* hupanga mishahara yao kama Wakala wa Serikali au Mamlaka inayojitegemea kulingana na nguvu ya soko. Hivyo aghalabu hutoa mishahara mikubwa kulinganisha na inayotolewa na Serikali Kuu. Sina uhakika sana kama mafundi wa Wizara ya Ujenzi wenye sifa, elimu na ujuzi ule ule wanalipwa mishahara zaidi ya ufundi kwa Wizara yangu.

Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga anaomba *SACCOS* zilizoko katika jimbo zifuatazo zipewe mkopo wa shilingi 500,000 kila mmoja. Songambele Usangi, Kimbatile Kisangara, Mwamko Ugweno, Tagongo *SACCOS* Lang'ata. Wizara yangu inatoa mikopo kwa wanawake kupitia Mfuko wa Maendeleo kwa Wanawake (*WTF*). Mkopo kupitia mfuko huu utaendelea kutoa fedha kwa utaratibu na kiasi kilichowekwa cha shilingi 4,000,000 kwa kila Halmashauri. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge avishauri vipindi hivi viwasilishe maombi yao kwenye Kamati ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Margareth Mkanga tena amezungumzia watoto wenyе ulemavu wananyanyaswa kwa upande wa elimu na baadhi wanazurura na kubakwa ovyo. Kuna haja ya kuangalia upya sheria zetu na mila potofu zinazogusa watoto hao. Sheria zipo za kuwalinda watoto wote na tunatarajia kurekebisha na kuunganisha sheria zote zinazohusu watoto. Sera za Maendeleo ya Mtoto tunayodurusu imazingatia matatizo mbalimbali yanayowakabili watoto wenyе ulemavu. Mwongozo wa utekelezaji wa sera pia utazingatia bayana matatizo ya watoto wenyе ulemavu hususan mila potofu zilizopo katika jamii. Halmashauri hazizingatii agizo la Waziri Mkuu, Naona nimezungumzia kwamba agizo liko pale pale na kwamba Wakurugenzi waendelee kutenga asilimia tano kwa ajili ya mikopo ya wanawake.

Mheshimiwa Singo, Mbunge wa Same Magharibi amezungumzia uhaba wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ya Same. Aidha, ingefaa wawepo hadi ngazi ya Kata ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna upungufu mkubwa wa wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zote ikiwemo Halmashauri ya Same. Hata hivyo hali hiyo inasababishwa zaidi na uwezo mdogo wa Halmashauri zetu kuajiri wataalamu hao katika ngazi zote zikiwemo za Kata na Kijiji. Hadi kufikia mwaka jana 2003/2004, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kilikuwa kinatoa wastani wa wataalamu 70 kwa mwaka. Aidha, Vyuo vya Buhare, Misungwi na Rugemba kwa pamoja vilikuwa vinatoa wastani wa wataalamu 150 kwa mwaka. Idadi hiyo ya wataalamu ni kubwa na kama wote wangekuwa wanaajiri hali isingekuwa kama ilivyo sasa. Kwa hiyo, wataalamu wako tatizo ni ajira kwa sababu hali za Halmashauri zetu bado sio nzuri.

Mheshimiwa Salama Khamis Islam amezungumzia Halmashauri hazifuatilii urejeshaji wa mikopo, Halmashauri hazitoi asilimia tano anashauri Halmashauri zichangie asilimia tano na zifuatilie mikopo. Benki ya Wanawake na namwachia Mheshimiwa kinara mwenyewe, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watto, atakuja kuzungumzia, uundaji wa chombo naye ataongelea Mheshimiwa. Kwa hiyo akija hapa Benki na chombo majibu yako tayari.

Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tutashughulikia tatizo la wanawake wazee Shinyanga. Tumepokea ushauri huo wa mikopo na naona maelezo niliyotoa ndiyo yale yale kwamba kuna haja ya kuwakopesha kufuatilia mikopo hiyo. Kwa upande wa hawa akinamama kwa kweli ni dhambi kabisa kuwa akinamama wazee just because wana macho mekundu. Jamani huu ni ukatili wa

hali ya juu, kwa nini umwue kwani wewe au mimi hatutazeeka na je, utapenda tukitendewa vile. Jamani jamani sheria ipo. Jamani ndugu zangu wa Shinyanga.

WABUNGE FULANI: Mwambie Mheshimiwa Derefa!!!!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Nimwambie Mheshimiwa Derefa eeh!!!.

Mheshimiwa Derefa umesikia?

MHE. LEONARD N. DEREFA: Ndiyo.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge wa Mbulu anazungumzia udogo wa fungu la fedha za ukarabati wa majengo. Mheshimiwa Mbunge nimekiri kwa kweli tuna udogo. Wengi wamezungumzia hapa mambo mengi na mambo yakiwa mazuri basi tutaweza kuleta fedha nyingi ili tuwe pamoja katika harakati. Umezungumzia masuala ya Chuo ambacho kina ukosefu wa gari Na pikipiki kwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tango. Tunajua haya yote lakini tatizo kama nilivyo sema na ninyi wenyewe mmezungumzia hapa hapa kwamba tatizo ni fedha. Wizara inakiri kwamba gari la Chuo cha Tango *Landcruiser STH 3124* ni bovu na linahitaji fedha nyingi za matengenezo. Makisio ya utengenezaji wa gari hii na mengine vyuoni yanafanyiwa kazi kufuatana na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, jibu langu liko pale pale. Mheshimiwa Mbunge naomba tuwe pamoja katika gurudumu hili pamoja na ufinyu wa bajeti lakini nchi hii ni yetu, vyuo hivi ni vyetu, wananchi ni watu lazima tutafute mbinu.

Naomba hapa niwashukuru Wakurugenzi ambao wanasa idiana na vyuo hivyo. Najua leo Kamati ya Maendeleo ya Jamii imeipongeza *FDC* ya Ifakara na pongezi hizo wanastahili kwa sababu Mkurugenzi hayupo mbali na chuo hicho.

Pia wameipongeza *FDC* ya Kilosa walikuwepo Mkoani Morogoro na wamejionea wenyewe. Kwa hiyo, mimi nawashukuru lakini hapa naomba sana nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa Mashishanga kwa sababu Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilivyofika Morogoro alikuwa na Kamati hiyo toka siku ya kwanza mpaka siku ya mwisho na alitoa maelekezo *on the spot* na mengi yametekelawa. Kwa hiyo, mimi namshukuru Mheshimiwa Mashishanga kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge kwa vile muda umenitupa mkono mimi sina mengi lakini naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo naomba kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii. Labda nitangulie kusema kwamba inawezekana tusiweze kujibu yote lakini wale ambao tutakuwa tumeshindwa kukamilisha majibu yao basi tutayaleta kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia hoja hii kwa kauli ni Mheshimiwa Jina Khatib Haji, ambaye aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa niaba ya Mwenyekiti, wa pili alikuwa ni Mheshimiwa Teddy Louise Kassela-Bantu, ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii. Wengine ni Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mheshimiwa Rhoda Lugano Kahatano, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Prof. Juma Mtupa Mikidadi, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama na Mheshimiwa Shamim Parkar Khan. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Khalid Uledi, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mheshimiwa Remidius Kissasi, Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, Mheshimiwa Khalid Suru.

Wengine ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Leonard Derefa na Mheshimiwa Prof. Alhaj Juma Kapuya. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao waliyooita kwa uwazi na kwa dhati natumaini sijamwacha Mheshimiwa Mbunge yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niishukuru sana Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Tunashukuru kwanza Kamati hii ilishauri Wizara yangu na kuchambua bajeti kabla hatujaileta hapa. Lakini vile vile niishukuru Kamati hii chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuweza kuridhia kwa kiasi kikubwa mengi ambayo yanatekelezwa na Wizara yetu. Lakini pia napenda kuwashukuru kwa maoni na ushauri waliota na napenda niahidi kwamba tutauzingatia na tutautekeleza. Napenda tu nizungumzie kwa ujumla na hapa nitaomba hili nitakalolizungumzia pia Waheshimiwa Wabunge wengine waliolizungumzia waweze kulichukua hivyo kwa ajili ya ufinyu wa muda. (*Makofi*)

Mojawapo lililozungumzwa na Kamati ni urejeshaji wa mikopo na labda niseme kwamba hili limekuwa ni tatizo Waheshimiwa Wabunge na nashukuru kwamba wengi mlionchangia mmeweza kutuhimiza tubuni namna ya kuongeza kasi ya urejeshaji. Mojawapo ya mambo tuliyoyafanya ni kuweka utaratibu ule mwongozo tuliotoa mpaka

hivi sasa umetusaidia sana na urejeshaji umepanda. Lakini kingine tunachokifanya Waheshimiwa Wabunge ni kuendelea kutoa mafunzo ili biashara ziwe endelevu na hivyo wale wanaokopa waweze kurejesha kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme pia kwamba utaratibu huu wa kuwekeana mikataba na Halmashauri umetusaidia sana na tumepokea maoni mengi na wengi wametutia shime kwamba utaratibu huo umesaidia kufuatilia urejeshaji. Lakini bado tutaendelea kufuatilia urejeshaji na tutaomba ushirikiano na Waheshimiwa Wabunge wakiwa kama ni Wajumbe wa Kamati za Mikopo tuwe pamoja katika kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia Chombo cha Wanawake na Benki ya Wanawake. Ni kweli kwamba imechukua muda mrefu kuunda vyombo hivi viwili Chombo na Benki hizo za Wanawake. Lakini wote tunafahamu Waheshimiwa Wabunge kwamba vyombo kama hivi ni vyombo ambavyo vinaweza kuhudumia wanawake walio wengi na Tanzania kwa ujumla. Kwa hiyo, Wizara yetu ilibidi ichukue muda kufanya mashauriano kushirikisha wadau wengi kabla hatujakuja na mfumo ambao sasa ndio uliopendekezwa. Lakini napenda niseme kwa kuwa maandalizi ya vyombo hivi viwili yamefikia katika hali ya juu tunategemea kwamba uamuzi utapatikana katika muda sio mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililozungumziwa na Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengi ni suala la kuimarisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Nakubali kwamba chuo hiki ni chuo muhimu sana katika kutoa wataalamu wa Maendeleo ya Jamii. Ni chuo ambacho sasa hivi kiko katika mfumo wa Taasisi ya Elimu ya Juu na kweli tunakabiliwa na changamoto ya kukiwezesha. Sasa tumepokea ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba tuweze kukipa chuo hiki vifaa vya mawasiliano. Hivyo kwa kweli ndivyo tunavyoazimia kufanya. Tunaweka utaratibu ambapo kutakuwa na mawasiliano ya *internet*. Lakini pia tunatarajia kununua vifaa vya kisasa vitakavyowawezesha wafundishaji kwa kutumia mbini hizo kwa mfano kutumia *Power Point*, kutumia *Projectors* hali kadhalika kuendelea na ukarabati wa miundombinu na fedha kwa ajili hiyo tayari zimeshachangwa. Tumepokea pia ushauri wa Kamati kwamba tuweze kuviimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kama nilivyosema katika hotuba yangu tutaendelea kufanya ukarabati huo na mojawapo ya mambo ambayo tunayoamua kufanya ni kuangalia namna ya kufanya ukarabati mkubwa sana katika baadhi ya vyuo kwa awamu ili ule ukarabati uwe na manufaa na uweze kuonekana. Hali kadhalika tumeshauriwa kuendelea kufuatilia fedha tunazopeleka kwenye vyuo. Hili tutaendelea kufanya na tunashukuru kwa ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengi wameonyesha masikitiko yao, wametoa kilio chao kuhusu ufinyu wa bajeti kwa Wizara yetu. Tunakubali kwamba hili ni jambo lililopo lakini labda niseme kwamba tatizo hili tayari sisi kama Wizara na Serikali kwa ujumla tumeliona na hivi sasa tuko katika utaratibu wa kuona ni namna gani Wizara yetu iweze kuongezewa fedha. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu hivi sasa Wizara imeandaa *Master Plan*.

Master Plan hii ni hatua ya kwanza muhimu sana ya kuweza kubainisha ni maeneo gani ya kipaumbele na hatua ya pili itakuwa ni kutafutia fedha mpango huo na tayari utaratibu kidogo umeanza. Ndani ya bajeti tumeweza kupata fedha kidogo, lakini tunategemea kwamba tutakapokamilisha mpango huu tutapata pia ushirikiano wa washiriki wetu katika maendeleo ambao tuko katika mazungumzo nao na tayari wameonyesha nia ya kuweza kutusaidia na ndiyo sababu katika ule mpango wa miaka mitatu, tumeanza na mpango wa mwaka mmoja ili katika kipindi hiki tuweze kujipanga vizuri zaidi na tayari ziko nchi tano ambazo tumezitaja katika hotuba yetu ambazo ni Ireland, Holland, Sweden, Netherlands na Italia ambao wameonyesha nia ya kuchangia kwa pamoja. Tunatumaini kwamba kadri tutakavyokamilisha mipango yetu ya maendeleo ndani ya Wizara kupitia *Master Plan*, tutaweza pia kupata fursa ya kuongeza bajeti yetu kwa fedha za ndani na za nje. Kwa hiyo, napenda kutoa shukrani na kuahidi kwamba tutaendeleza kasi ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha nyingi zaidi ili tuweze kutimiza majukumu yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, kwa hotuba yake na mambo fulani fulani ambayo ameyazungumzia. Labda niseme tu kwamba, kama tayari alivyokwishanisaidia Mheshimiwa Naibu Waziri, suala la uchangiaji wa Halmashauri ni suala ambalo limeagizwa na sisi tutaendelea na jitihada zetu za kuzihamasisha Halmashauri. Lakini labda niseme kwamba, kutohana na jitihada na kilio cha Waheshimiwa Wabunge, baadhi ya Halmashauri nyingi zimeweza kuchangia. Tutaendelea kushirikiana na zile chache ili tuhakikishe kwamba na wao wanatoa mchango wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ameonyesha nia ya kuzunga mkono Benki zitakapoanzishwa. Labda nichukue pia fursa hii kusema kwamba, kuna Waheshimiwa ambao wamesema ni vema tukazungumzia Benki na siyo Vyama vya SACCOS. Ni kweli hilo linawezekana, lakini mchakato wa kupata Benki uliainisha mawazo ya wachangiaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge na wanawake kwa uwakilishi kutoka Tanzania nzima na vile vile utafiti uliofanywa umeonyesha kwamba kwa kweli namna nzuri ya kuanzisha Benki hiyo ni kuimarisha Vyama vya Kuweka na Kukopa na hilo nadhani pia ni ambalo linatendeka katika baadhi ya Wilaya nchini mwetu. Tunategemea kwamba hapo tutakapofikia hatua ya kuimarisha Vyama vya Kuweka na Kukopa tutakuwa tumejiweka mahali pazuri pa kuanzisha Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie jambo ambalo pia limezungumziwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, anavyopenda kuona kwamba Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitumike kuwa Elimu ya Sekondari. Nadhani hili tayari tulikwishalivuka kwa sababu tunaona kwamba hivi sasa upo mpango, ulikuwepo mpango wa kuimarisha Elimu ya Msingi na sasa hivi tutaingia kwenye mpango wa kuimarisha Elimu ya Sekondari. Kwa hiyo, tukubali kwamba haitawezekana tuwe na mfumo mmoja tu wa kutoa elimu.

Ni sharti tuwe na vyuo ambavyo vitakuwa kama ngazi, wale wanaomaliza sekondari waweze kupata ujuzi zaidi na tunadhani hivi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinaweza vikafanya kazi hiyo vizuri zaidi. Kwa hiyo, haja kwa kweli ni kuviimarisha na siyo kuvibadilisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais; Utumishi, katika kuhakikisha kwamba Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wanaendelea kuajiriwa kila inapowezekana kuititia Halmashauri na pia kuititia Sekretarieti za Mikoa. Lakini labda niseme pia kwamba, ni kweli kada hii ya wataalam inakabiliwa na tatizo kubwa la vitendea kazi, lakini tunafurahi kusema kwamba hivi sasa kuititia Mpango wa Uboreshaji wa Serikali za Mitaa tumeanza kuona mwanga ambapo utendaji utaimarishwa hususan kwenye Sekretarieti za Mikoa na Wilaya na hivyo kuna mwanya wa kuhakikisha kwamba watendaji wake wote na hususan Watendaji wa Maendeleo ya Jamii wanaweza kupatiwa vitendea kazi na sisi Wizara yetu ikiwa ndiyo Wizara mama ya kada hiyo tutashirikiana na TAMISEMI katika kuhakikisha kwamba hilo linaendelea kutazamwa hasa katika Mfumo huu wa Uboreshaji wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumze kuhusu suala la fedha zilizotengwa kwenye Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Mheshimiwa Kasella-Bantu amezungumzia kwamba suala hilo ni kisingizio cha Uchaguzi Mkuu. Labda kwa ajili ya usahihi wa *record* zetu niseme kwamba, suala la ulinzi na usalama ni suala la msingi sana katika nchi yoyote na sidhani kwamba litategemea tu kuwepo na uchaguzi kwa sababu amani ni kitu cha wakati wote. Sisi wenyewe hapa Waheshimiwa Wabunge tunajua, tusingewenza kufanya kazi zetu hapa kwa utulivu kama huko nje tusingewenza kuhakikishiwa usalama wetu. Kwa hiyo, nadhani si vema kuchanganya mambo haya katika kipindi hiki tulichonacho. Nadhani ulinzi na usalama ni suala la kipaumbele kwa wakati wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia haja ya kuwa na hati miliki katika vyuo vyetu na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu amezungumzia hilo. Napenda niseme kwamba, katika hotuba yetu tumeeleza kuwa kwa mwaka huu wa fedha tunategemea kushughulikia hati za kumiliki ardhi kwa vyuo visivyopungua 20 kwa kuanzia. Lakini hususan kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Monduli, labda niseme kwamba kumekuwa kidogo na mkanganyiko kuhusu umiliki wa ardhi ya chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo hiki kinayo ardhi yake na kilikuwa na hati yake, lakini kama ambavyo tunafahamu kuna eneo lililomilikishwa KKKT na katika utaratibu wa kuhakikisha kwamba miliki hizo zinafanywa kisheria, ilibidi chuo kirejeshe Wizara ya Ardhi hati zake na hizo hati ni namba CT 12052 na 12053 ambazo zilirejeshwa Wizara ya Ardhi, lakini zinashughulikiwa tena kwa kuzingatia hiyo ardhi ambayo wamepewa KKKT na walipewa kabisa kwa kufuata uratatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba zilizoko ndani ya eneo la chuo, ni kweli kwamba kuna mgogoro kati ya chuo na Halmashauri, lakini hilo ni suala ambalo tunalishughulikia kwa sababu inasemekana zipo nyaraka zilizofanya nyumba zile ziwe

mali ya Halmashauri ingawaje zimo ndani ya eneo la chuo. Hilo ni suala ambalo tunalifuatilia ili tuweze kujua ukweli uko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nizungumzie kwa ujumla yale ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Mengine ameyazungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri na yapo ambayo yalikuwa ni ya kwangu kwa maana ya Chombo na Benki. Mheshimiwa Salama Khamis Islam amezungumzia hayo, lakini kama nilivyosema kwamba mchakato huo sasa hivi umefikia mahali pazuri na nadhani katika kipindi ambacho siyo cha muda mrefu sana tutaweza kuwa tumepeata uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Monica Mbega na Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud walizungumzia haja ya kuangalia upya hali ya wanawake ambao wameshindwa kurejesha mikopo baada ya kuwa walipewa mikopo hiyo bila ya mafunzo. Nadhani kimsingi Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba ni taratibu nzuri ya fedha kurejesha mkopo. Sasa kwa hawa ambao labda wamekumbwa na matatizo, nadhani tupokee ushauri uliotolewa kwamba tujaribu kuona watapewa masharti gani mepesi zaidi, lakini kimsingi waweze kurejesha kile ambacho walikopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rhoda Kahatano alitupa ushauri kwamba Wataalam wa Maendeleo ya Jamii waweze kupewa mbinu na stadi za kuwawezesha kuandika michanganuo mizuri kwa ajili ya kuwasaidia Wananchi. Tunashukuru sana kwa ushauri huo wa Mheshimiwa Rhoda Kahatano na tutautumia na kwa kweli ni vema Wataalam wetu wa Maendeleo ya Jamii wakawa na stadi hizo ili waweze na wao kuwasaidia Wananchi kuandika miradi yao kwa ufasaha na hivyo kujiweka katika hali nzuri ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, ametushauri kwamba Chombo cha Wanawake kitakapoundwa kiingizwe kwenye Katiba. Nadhani hilo ni wazo zuri. Tayari tumepeata mapendekezo kuhusu ni muundo gani chombo hicho kichukue na muundo uliopendekezwa ni Tume. Sasa itabidi tukae tuangalie Tume hiyo itaanzzishwa kwa utaratibu upi, kama ni wa kutajwa ndani ya Katiba au kwa namna nyininge hayo ni masuala ambayo wataalam wa sheria watatushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi ambaye amefafanua kwa ufasaha kabisa dhana ya maendeleo ya jamii. Tunakubaliana naye kwamba maendeleo ya jamii ni sharti yafikishwe kwa Wananchi na hapo ndipo tutakaposema maendeleo ya jamii yapo na ndiyo maana wataalam wetu wanapewa mbinu hizo za kuhakikisha kwamba kwanza wanafanya kazi ya uraghbishi ambayo ni kukaa karibu na wananchi kupanga nao na kutekeleza kwa pamoja. Tunashukuru kwa ushauri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khalid Suru ametuuliza kama Chuo cha Munguri ni kimojawapo kati ya vyuo vitakavyokarabatiwa. Labda niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba, katika vile vyuo sita ambavyo tumesema tutavikarabati Kikanda tumejiwekea vigezo.

Sasa vigezo hivyo ndivyo vitaamua ni chuo gani kichukuliwe. Lakini mojawapo ya vigezo hivyo ni kuangalia chuo kina wanafunzi wangapi, kinatoa kozi za aina gani, kina mvuto gani, kina kiwango gani cha kujitegemea na kadhalika. Haya ndiyo yatatuwezesha kuamua na kama chuo hicho kitakidhi sifa hizo na tutafanya hivyo wazi kabisa kupitia Mikoa, basi tutaweza kuviweka katika mpango huo wa awali. Lakini nia yetu ni kuvikarabati vyuo vyote, kinachogomba ni fedha na ndiyo maana tunakwenda kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Halima Kimbau kuhusu bidhaa mbalimbali. Tunashukuru sana kwa ushauri wake. Pia, ameshauri kwamba Halmashauri zirejeshe fedha kulingana na mkataba. Huo ni mwito mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo tunakushukuru kwa pongezi na tutaendelea na juhudi za kuendelea kuvipatia vifaa bora Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kama alivyosema kama vile kompyuta, vyerehani na kadhalika. Kadri hali itakavyoruhusu tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru pia Mheshimiwa Nyawazwa na tutafikisha salam zake kwa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa kwa jitihada anazozifanya. Mheshimiwa Nyawazwa amemshukuru kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Mwanza. Labda niseme tu kwamba, Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote ni Mfuko wa Udhamin, hautoi mikopo, lakini unapata misaada na nadhani tutafikisha ujumbe huo kwa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Faida Bakar kwa ushauri alioutoa kwamba ni sharti mikopo hii ilenge vijijini na kwa kweli ndiyo nia yetu na ndiyo maana mara kwa mara tunajaribu kufanya kazi kwa karibu na Halmashauri. Tumeupokea ushauri wake na vile vile tutaendelea kutoa elimu kwa vikundi vya wanawake ili waweze kutumia mikopo hiyo vizuri zaidi. Tunashukuru pia kwa ushauri wa Mheshimiwa Ruth Msafiri ambaye ye ye ameshauri kwamba mtazamo wa Benki usiwe wa ki-SACCOS. Kama nilivyozungumza ni kwamba, hayo ni mapendekezo tulipata, lakini bado tunadhani ni ushauri ambao tunaweza tukauangalia tena. Tunamshukuru pia Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah ambaye na ye ye ameomba Serikali izingatie sana suala la bajeti. Tuangalie bajeti hii iweze kuongezwa. Tunamshukuru na kama tulivyosema tayari tumechukua hatua za kuelekea huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Edward Ndeka ametaka dawati lisiwe la jinsia liwe la maendeleo ya jamii. Kwa kweli wataalamu maendeleo ya jamii tayari tunao kwenye Wilaya na tulitaka masuala haya ya jinsia yaingizwe katika kila mpango ili yaweze kufanya mipango yetu ya maendeleo iwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, ametupa changamoto nyingi, tunazichukua na labda niseme kwamba kwa Ulingo wa Beijing ni kweli tumefikia miaka 10 na tunafanya tathmini hiyo. Lakini kama

alivyosema, labda bajeti hii ni kipimo pia cha kuweza kuona tumefikia wapi katika Ulingo wa Beijing.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, tunawashukuru Mheshimiwa Anatory Choya na Mheshimiwa Leonard Derefa. Mheshimiwa Derefa amezungumzia mauaji ya vikongwe. Tunaungana naye kwamba ni sharti sisi kama jamii tushughulikie tatizo hilo na ameomba msaada kupitia Shirika ambalo mimi binafsi nalifahamu, linaloshughulika na suala hili. Labda nimhakikishie Mheshimiwa Derefa kwamba, tutaendelea kushirikiana ili tuhakikishe kwamba Shirika hili linapata usaidizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Leonard Derefa ameshauri pia kuwe na vigezo vya kutolea mikopo. Hilo nalo tutaliangalia kwa maana ya kuangalia wingi wa watu, kiwango cha umaskini na kadhalika. Haya yote tumeyapokea. Labda nichukue tena nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na kusema kwamba kama kuna yejote ambaye tutakuwa hatukumjibu kikamilifu basi tutarejea tena makaratasi yetu ili tuweze kuwajibu kikamilifu. Lakini matumaini yetu ni kwamba, haya tuliyoyasema yametosheleza na tunakushukuruni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 53 - WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO

Kifungu 1001 - *Administration and General* 834,250,900/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tutende haki kwa wenzetu waliosimama. Mheshimiwa Jumanne umesimama?

WABUNGE FULANI: Hapana.

MWENYEKITI: Nawaona Waheshimiwa watano. Haya Mheshimiwa Mama Janet Kahama.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nikiwa nataka kuzungumzia katika kifungu cha 1001. Kwanza nataka kumsifu sana Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya Wizara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki mimi bado nina dukuduku kukeketwa keketwa, keketwa. Hili neno litaisha lini? Kwa sababu ni muda mrefu sana sasa Wizara imeweka nguvu ikisaidiana na *NGOs* mbalimbali, lakini mpaka sasa hivi hatujaona kwa nini haiwafikii Wananchi. Tungeshukuru sana kama Wananchi wenye

ndani ya Vijiji wangefikiwa wakapewa kazi hii hata zaidi kuliko *NGO*. Nataka maelezo zaidi kutoka katika hiyo sehemu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo yafuatayo kuhusu hoja aliyotoa Mheshimiwa Janet Kahama. Ni kweli kwamba hivi sasa bado tunalo tatizo la ukeketaji. Tatizo hili ni la kijamii na kwa hiyo suluhisho lake haliwezi kuwa rahisi sana. Lakini labda nimuombe Mheshimiwa Janet Kahama akubaliane na takwimu za kisayansi kabisa ambazo tumezipata kupitia Sekretarieti za Mikoa ambazo zinaonyesha kwamba kiwango cha ukeketaji kimepungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 1996 tulikuwa na asilimia 12.9, lakini hivi sasa tuko kwenye asilimia 10. Kwa hiyo, kwa kweli juhudhi zilizofanywa na Serikali zinaonyesha kwamba ukeketaji unapungua. Labda nimuombe Mheshimiwa Janet Kahama aachie mshahara wa Waziri, lakini niahidi kwamba tutashirikiana naye katika kuhakikisha kwamba tunaongeza kasi ya kuihamasisha jamii iachane na mila hii yenye madhara. (*Makofi*)

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1001, nia yangu ni kupata maelezo tu. Katika kitabu cha jedwali na michoro ya Hotuba ya Bajeti ukurasa wa 19 inaonyesha kwamba idadi ya mafundi katika Vikosi vya Ujenzi Mikoa ya Kigoma, Lindi na Rukwa haina mafundi wa ujenzi. Ni sababu gani zilizofanya Mikoa hiyo kusahaulika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni katika ukurasa wa 30 na 34. Tukienda ukurasa wa 30 inaonyesha kwamba Mkoa wa Kigoma umejitahidi kurejesha fedha za mikopo tukiondoa Wilaya ya Kibondo ambayo imerejesha pesa na zimebakia kidogo. Lakini tukienda ukurasa wa 34 katika mgao wa fedha Mkoa wa Kigoma ukiondoa Halmashauri ya Mji wa Kigoma haikutengewa fedha za mikopo mwaka 2002/2003. Ni sababu zipi ikiwa sisi tumeweza kurejesha mikopo na mwaka uliofuata tumenyimwa pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 54 ni kwamba Wizara ina mikakati ya kutoa mafunzo ya UKIMWI katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, lakini Mkoa wa Kigoma, Chuo cha Kihinga hakipo katika mpango wowote wa kupewa mafunzo. Ni sababu zipi zinamfanya Waziri ausahau Mkoa wa Kigoma?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafundi wa Vikosi vya Ujenzi kwa upande wa Mkoa wa Kigoma kwenye baadhi ya Wilaya ni kwamba, katika baadhi ya Halmashauri vikosi hivi viliunganishwa na baadhi ya Idara. Kwa hiyo, kitu ambacho tumefanya hivi sasa ni kwamba tumefanya utafiti katika Halmashauri na tumetoa mwongozo kwamba Vikosi hivi vya Ujenzi na Ufundu virejeshwe katika hali yake ya kawaida. Sasa katika zile halmashauri ambapo vikosi hivi vilivunjwa, viliunganishwa na ujenzi wa barabara. Kwa hiyo, katika kuchukua taarifa, taarifa zilizopokelewa ni kwamba hivi vikosi vilikuwa havipo, lakini kilichotokea ni kwamba vilivunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaamini kwamba vikosi hivi ni muhimu sana katika miradi ambayo inahusisha nguvu za Wananchi. Kwa hiyo, tumetoa maelekezo kwamba virejeshwe na tunategemea kwamba katika Mkoa huo wa Kigoma hivyo ndivyo itakavyokuwa.

Kuhusu mikopo ni kwamba, mikopo ambayo tunaionyesha ya 2002/2003 ilikuwa inategemea urejeshwaji. Sasa katika ile ambayo tulitoa katika mwaka 2001/2002 inaonyesha fedha hizi zimerejeshwa. Sasa kwa wale ambao hawakuja kuzichukua kwa sababu tumeweka utaratibu waje kuzichukua.

Kwa hiyo, kama hawakufika kuzichukua kwa maana ya ku-sign ile cheki na mkataba ndivyo inavyotokea kwamba wanakuwa hawakupelekewa zile za 2002/2003.

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesahau suala langu la tatu kwamba ni kwa nini katika mafunzo ya UKIMWI Mkoa wa Kigoma umesahauliwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri bado hajaipata vizuri.

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 54 katika kitabu cha majedwali, idadi ya watumishi waliopata elimu ya UKIMWI na watakaopatiwa elimu ya UKIMWI mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza 2003/2004 Mkoa wa Kigoma haupo, 2004/2005 Mkoa wa Kigoma haupo, Chuo cha Kihinga hakimo. Ninaomba maelezo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha majedwali ukurasa wa 54 tulichonacho sisi kinaonyesha hawa ni watumishi waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2003/2004.

MWENYEKITI: Hiyo 54 unayosoma...

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, ni ukurasa wa 53.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya Watumishi waliopatiwa elimu ya UKIMWI mahali pa kazi kwa mwaka 2003/2004 ni kwamba tulikuwa tunatoa mafunzo haya kwa awamu. Kwa hiyo, katika awamu inayofuata ninaamini kabisa Mkoa wa Kigoma utakuwepo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, niliona mnashangaa shangaa Waziri kusoma majedwali, alikuwa anaimarisha hoja yake, anayo haki kabisa.

MHE. THOMAS NGawaiya: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi ya kwangu ni madogo kwa sababu Waswahili wanasema ‘mkono mtupu haulambwi’

fedha hamna. Lakini mwaka 2001 tulizungumza kuhusu matatizo ya Chuo cha Maendeleo kilichoko Singa na Waziri tulikuwa naye na tukaona kwamba kulikuwa na vitu. Hicho chuo mwanzo kilikuwa *Singa Pharmacy Training Centre*, sasa hivi ni Chuo cha Maendeleo ambacho kipo chini ya Wizara hii.

Kwa hiyo, kulikuwa na vitu vilivyokuwemo kama ng'ombe na kadhalika, lakini vikawa vimetoweka. Pia, ni pamoja na uchakavu. Ninaipongeza Wizara kwamba sehemu ya uchakavu imefanyiwa kazi, lakini kulikuwa na bomba za maji ambazo tulimlilia Waziri na akaahidi. Sasa leo hii ni mwaka wa tatu, bado nataka nimueleze Waziri kwamba zile bomba za maji zilizokuwa zimechukuliwa pale bado wale wanafunzi hawajapata, anatueleza nini kwa sasa katika bajeti hii ya mwaka huu kuhusu chuo hicho?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba ni kweli nilitembelea Chuo cha Msinga na tulikuwa na Mheshimiwa Ngawaiya na kama alivyo sema yeye mwenyewe yale masuala ya uchakavu tuliyashughulikia kwa kupeleka fedha za ukarabati, lakini kulikuwa na baadhi ya vifaa ambavyo viliibwa.

Nadhani haya mabomba yalikuwa ni sehemu ya vifaa vilivyoibwa na tuliona kwamba tatizo lilikuwa katika suala zima la ulinzi na ushirikiano wa chuo na jamii inayoizunguka.

Kulikuwa kama na aina fulani hivi ya njama ya kuchukua mali za chuo isivyo halali. Haya mabomba ninavyokumbuka ni kwamba, ilikuwa ni mojawapo ya yale ambayo yalikuwa yanahusishwa na vitendo vya jinai. Lakini kwa kuwa tunao mpango wa ukarabati kwa ujumla hili ni suala ambalo tutalizungatia katika awamu hii ya ukarabati inayofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda nimuombe Mheshimiwa Ngawaiya kwamba ashirikiane basi na viongozi wa pale kwenye chuo chetu na Wananchi kwa ujumla wakione chuo hiki ni cha kwao na hivyo wasikihujumu kwa kudokoa dokoa vitu. (*Makofii*)

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1001. Katika mchango wangu nimezungumzia kuhusu fedha kwa ajili ya mikopo ya wanawake. Nimeeleza kuwa fedha hizi zinapofika Wilayani kwa kweli *distribution* yake haiwi *fare*, maeneo ya vijiji yanaonekana kusahaulika. Kwa hiyo, wanaofaidika mara nyingi ni wale ambao wako mijini au karibu na mijini.

Sasa katika majibu niliyopewa, Mheshimiwa Waziri amesema sisi Wabunge tupo kwenye *Area Loans Committee*, Kamati ambazo zinasimamia ugawaji wa hizo pesa.

Lakini kwa Wilaya yangu na nina imani vile vile na Wilaya zingine Wabunge hawahusishwi kwenye hizi Kamati.

Je, Mheshimiwa Waziri atachukua jukumu gani la kuwaandikia watendaji hawa walioko kwenye Halmashauri jinsi ya kuwahusisha Waheshimiwa Wabunge kwenye hizo Kamati na kuhakikisha kuwa fedha hizi zinasambaa kote mijini na vijijini ili Wananchi wote waweze kufaidika. Naomba maelezo. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kuhusu suala alilolizungumzia Mheshimiwa Uledi. Kwanza kabisa niseme kwamba tulitoa mwongozo mwaka jana kwa Halmashauri zote kuhusu namna ya uendeshaji wa mikopo hii.

Kwanza kama tulivyosema kwenye hotuba ni kwamba tunaingia Mkataba na Halmashari. Lakini pili, tumetoa mwongozo tukieleza wazi kwamba Waheshimiwa Wabunge, wote ni wajumbe wa hizi kamati. Tulipofanya hivi tulikuwa tunafahamu kwamba Waheshimiwa Wabunge, ndiyo wako karibu sana na wananchi kwa hiyo, watakuwa kwenye hali nzuri ya kugawa mikopo hiyo.

Sasa kama kuna tatizo hasa katika Jimbo la Nanyumbu la Mheshimiwa Aridi Uledi, labda niseme kwamba tutalishughulikia tatizo hilo, moja kwa moja kwa kuwasiliana na Mkurugenzi ambaye ndiyo tunaingia mkataba. Lakini vile vile tumesambaza mwongozo kwa Waheshimiwa Wabunge, wote ili waweze kuona. Kwa hiyo, hilo naomba niliweke hivyo na niombe Mheshimiwa Aridi Uledi, atuachie hii shilingi na hilo suala la kuhakikisha kwamba Waheshimiwa Wabunge, wapo na kwamba mikopo inawafikia wananchi hasa walio wengi vijijini huo ni mwongozo ambao tutausisitiza kwa Watendaji wa Halmashauri. (*Makofî*)

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichangia kuhusu suala hili la mikopo na tumejibiwa hapa kwamba sisi ndiyo tuko kwenye Kamati. Mimi nadhani hii si sahihi sijaridhika kwa sababu sisi tunaiuliza hapa Serikali na tujibiwe hapa kwa sababu mimi kama nikiwa kwenye kamati hiyo, halafu tukashindwa kutekeleza nani atahoji? Sisi hapa tunauliza kama watu wenye wajibu wa kufuutilia mambo *over sight responsibilities* kwa hiyo, mimi kwa kweli nisingependa kuwa katika kamati hiyo, kwa sababu mambo yakiharibika hatakuwa mtu wa kuhoji. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, Waziri huna la kujibu, umeeleza tu kwamba hupendi kuwa kamati hiyo. (*MakofîKicheko*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	177,879,900/=
Kifungu 1003 <i>Policy and Planning</i>	209,164,100/=

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la *policy and planning* wakati nachangia na wakati Waziri anajibu hoja amekubali kabisa kwamba suala la kuanzisha Vyama vya Akiba na Mikopo ndiyo njia pekee ya kuelekea

katika uanzishaji wa Benki ya Wanawake. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie kwa vile Vyama vya Akiba na Mikopo vya Wanawake, vilivyoanzishwa tayari mpaka sasa ambavyo vinaelekea katika suala zima la uanzishwaji wa Benki ya Wanawake, Wizara itavisaidiaje ili viweze kusimama na kuendelea kufikia hiyo hatima ya uanzishaji wa Benki ya Wanawake? (*Makofî*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kuhusu suala alilolizungumzia Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba Wizara itasaidiaje vyama hivi vya Akiba na Mikopo katika kufikia hatma ya benki.

Labda niseme kwamba katika mapendekezo yaliyotolewa ya uanzishaji wa benki ni kwamba huu mtaji unaotolewa sasa na Serikali, Mfuko huu wa Maendeleo wa Wanawake umependekezwa ndiyo kutumika kama kianzio cha mitaji kwa vile Vyama vya Kuweka na Kukopa, ambavyo tayari viro na vile ambavyo kama vitakuwa vimeduwa vimeanzishwa basi vitakuwa vimeingiziwa fedha hizi kama mtaji. Hayo ni mapendekezo yaliyotolewa. Uamuzi wa mfumo huu wa benki itakapopitishwa nadhani hoja aliyozungumzia Mheshimiwa Jenista Mhagama, ndiyo ambayo Serikali inakusudia kuifuata. (*Makofî*)

*(Vifungu vilivyoanzishwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Training and folk Development Colleges* 1,305,962,900/=

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika kitabu hiki nilikuwa najaribu kutazama pesa zilizotengwa kwa ajili ya kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rubondo, katika Wilaya ya Biharamulo, ni chuo ambacho kimeanzishwa muda mrefu lakini majengo yake yamechakaa kupita kiasi na kiasi kwamba ambavyo pita pale unaweza pale usiamini kama chuo unapotea kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa najaribu kutazama fedha za ukarabati katika chuo kile sijazona. Sasa na kile chuo kinaendelea kufanya kazi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, anipe maelezo hicho chuo ana mpango gani nacho juu ya kukarabati na kuona ninakuwa katika hali nzuri?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo; Chuo cha Rubondo ni Chuo cha Maendeleo ya Wananchi. Tunavyo Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Chuo cha Rubondo ni Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na kama nilivyosema kwamba badala ya utaratibu tuliokuwa nao hapo awali wa kutoa fedha kidogo kidogo kwa mwaka huu wa fedha, tumeamua kwamba tutenge vyuo sita kwa kanda na tutaweka vigezo ambavyo vitatusaidia kuchagua ni vyuo gani vya kuanzia na tuna imani kwamba Chuo hiki cha Rubondo kwa kanda ile kinaweza kuwa mojawapo kama kimetimiza vile vigezo. Lakini labda niseme tunachokusudia kufanya ni kuanza

kwa awamu hiyo halafu tutakuwa na awamu ya pili na tunategemea katika hizo awamu mbili za mwanzo Chuo cha Rubondo kitakuwa kimojawapo. (*Makofi*)

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati anapojiandaa kufanya priorities zake atume watalaan wakiangalie kile chuo kinavyofanana ili watakuwa wanapanga fedha wawe na hakika kile chuo kinafananaje ili kuweza ku-risk kisije kikapoteza hadhi yake wakati kinasubiri fedha mwaka mwingine. (*Makofi*)

MWENYEKIDI: Ni ushauri ambao ametoa. Sijui kama unataka kuukataa Waziri?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huo naukubali na kwamba tutakitazama vizuri Chuo cha Lubondo tujue hali yake na tuone kama kiko kwenye hali mbaya zaidi labda hatua za dharura zinaweza kuchukuliwa au tutaona kiingie katika awamu gani. (*Makofi*)

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Mbanga kiko Mjini, majengo yake ni mabaya kuliko majengo yote katika Mji ule. Kinatia aiba. Sasa ametuambia mwaka jana alikuwa ametoa shilingi milioni tano. Hapa sioni kitu chochote je, anasemaje kwa mwaka huu? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Mbanga kama alivyosema Mheshimiwa Ngwatura ni kweli kwamba mwaka jana kilitengewa shilingi milioni tano na tulifanya hivyo kwa sababu ukarabati mdogo mdogo ulikuwa unakwenda kwa awamu. Kwa hiyo, kwa awamu hii ya pili tuliona huo utaratibu ambao tayari nimeshaueleza na tutaangalia kama tunavyosema kikanda kwa sababu Jimbo analotoka Mheshimiwa Ngwatura linaingia katika kanda fulani, mimi nina imani kwamba hiki Chuo cha Mbanga, sifa mojawapo ameitaja kiko mjini.

Katika vigezo tulivyojiweka tulisema kwamba hicho ni kigezo mojawapo kwamba vyuo vilivyoko mjini pia vinakuwa na mvuto mkubwa vinachukua wanafunzi wengi na tunadhani hiki Chuo cha Mbanga, kinawenza kikakidhi vigezo hivyo ambavyo tumeviweka. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2002 - <i>Community Development</i>	468,315,000/=
Kifungu 2003 - <i>Community Development College - Tengeru</i>	219,958,700/=
Kifungu 3001 - <i>Gender Development</i>	723,238,300/=
Kifungu 3002 - <i>Children Development</i>	182,800,400/=

(Vifungu vilivyojotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 53 - WIZARA YA MAENDELEO KYA JAMII, JINSIA NA WATOTO

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i>	100,000,000/=
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	237,993,200/=
Kifungu 2001 - <i>Training and Folk Dev. Colleges</i>	200,000,000/=

(*Vifungu Viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa nataka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusu Chuo cha Wananchi Buhangija kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri, alitutembelea na mimi nilikuwa naye na tukaona hali mbaya ya *dormitories* ya FDC pale Buhangija.

Lakini nimetazama kila mahali kwenye ile schedule sikuona mahali ambapo kuna hela za ukarabati, maana alituahidi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba labda hapa anieleza kwamba kati ya hizi milioni 200,000,000 ametenga kiasi gani kwa ajili ya Chuo cha Buhangija hasa katika ukarabati wa dormitories. Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kuhusu hoja aliyozungumzia Mheshimiwa Derefa, ni kweli kwamba nilifika katika Chuo cha Buhangija na tulijionea hali ilivyokuwa. Ni kutokana na hali ya baadhi ya vyuo hivi kikiwemo Chuo cha Buhangija, tuliona kwamba ni vema badala ya kupeleka fedha kidogo kidogo tupeleke fedha nyingi zaidi.

Hivi sasa ndiyo tupo katika kufanya maandalizi hayo ya ni vyuo gani tuanzie na tutatazama pia Chuo cha Buhangija, kuona kama na chenyewe kinaweza kikaingia kwenye hii awamu ya kwanza, lakini kikikosa awamu ya kwanza nina imani awamu ya pili Chuo cha Buhangija kitakuwepo. (*Makofi*)

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2002 - <i>Community Development</i>	100,000,000/=
Kifungu 2003 - <i>Community Development College Tengeru</i>	150,000,000/=
Kifungu 3002 - <i>Children Development</i>	30,000,000/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(Bunge lilirudia)

TAARIFA

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi, imeyapitia makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu liyakubali makisio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto
kwa Mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Naona hoja imetolewa na nimeona imeungwa mkono. Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, yamepitishwa rasmi na Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Shughuli za Bunge kuna tangazo moja, Mheshimiwa Maria Watondoha, anawatangazia Wabunge akina mama wote wabaki hapa kwa ajili ya mukutano baada ya kuahirisha shughuli hizi za Bunge. Baada ya tangazo hilo sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu Saa tatu Asubuhi.

*(Saa 12.44 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatatu
tarehe 19 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*